Nipashe
Alhamisi Agosti 1, 2019 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
ISSN 0856 • Na. 0579985
MWANGA WA JAMII
www.ippmedia.com
www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US



## Vijana JKT wamwagwa kufanya usafi jijini Dar

UKURASA 3




UKURASA 13

# Watu 16 wafa kwa kujiua kila mwezi


• **Daktari** bingwa ataja sababu, mapenzi ni chanzo kikuu... *Endelea uk. 2*



Vijana wa Jeshi la Kujenga Taifa, wakifanya usafi wa mazingira katika maeneo mbalimbali ya Jiji la Dar es Salaam jana, kuelekea Mkutano wa SADC unaotarajiwa kufanyika mapema mwezi huu. **PICHA: JOHN BADI**

## Maalim Seif aponza Polisi

UKURASA 3



## Marehemu 193 watumika kuchota mamilioni Tasaf

• **Wamo** pia madiwani, wenyeviti wa vijiji, wastaafu na watendaji... *Endelea ukurasa 2*

**MICHEZO** STRAIKA MWILI JUMBA ATUA YANGA UK.32

**MAONI, KATUNI** UK.6



Makamu wa Pili wa Rais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, Balozi Seif Ali Idd, akimtwisha ndoo ya maji mwananchi wa Mahonda baada ya uzinduzi wa mradi wa maji kwenye eneo la nyumba za polisi, zilizoko katika Jimbo la Mahonda, Mkoa wa Kaskazini Unguja jana. Katikati ni Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani, Mhandisi Hamad Masauni. **PICHA: WMNN**

# Watu 16 wajiua kila mwezi Tanzania

**Na Gwamaka Alipipi**

WASTANI wa watu 200, ambao ni sawa na watu 16 kwa mwezi, hujiua kila mwaka kutokana na sababu mbalimbali, imeelezwa.

Daktari Bingwa wa Afya ya Akili, Dk. Tumbwene Mwansinsya, aliyesema hayo jana kwenye uzinduzi wa kampeni ya upimaji afya na huduma mbalimbali kwa askari polisi na watumishi wa umma, jijini Dar es Salaam.

Mtaalamu huyo alitaja sababu nne zinazofanya watu kuchukua uamuzi wa kujiua, kubwa ikiwa uhusiano wa mapenzi.

Dk. Mwansinsya ambaye pia ni Mhadhiri wa Chuo Kikuu cha Aga Khan (AKU), amesema kwa sasa kuna ongezeko kubwa la sononа hali inayosababisha watu kujiua huku akisema idadi kubwa ya watu wanaojiua, chanzo ni uhusiano wa mapenzi kutokana na kugombana na mwenza wake au kusalitiana.

Alitaja sababu ya pili ni hali ya uchumi au utafutaji wa kipato na kwamba watu wengi wanachukua uamuzi wa kujiua kwa sababu wanakosa mahitaji wanayoyataka.

"Utakuta mtu anatafuta pesa kwa ajili ya kujikimu kimaisha au kuihudumia familia yake, lakini anakosa. Hali hiyo inamsababishia msongo wa mawazo na kuamua kujiua," alisema Dk. Mwansisya.

Dk. Mwansisya alitaja sababu nyingine ni mlolongo wa majukumu ya kila siku. Alisema mtu anakuwa na pilika pilika nyingi za kujipatia riziki akiwa mjini lakini anazikosa.

"Utakuta mtu anataka kununua gari au kujenga nyumba, akiona watu mjini wanaendesha magari mazuri, wanakula vizuri lakini yeye hana, inamsababishia kupata msongo wa mawazo na kuamua kujiua," alisema Dk. Mwansisya.

Sababu nyingine ni mtu kupata ugonjwa kama vile Ukimwi au ugonjwa mkubwa usioweza kutibika, hivyo kumsababishia kuwa na msongo wa mawazo na hatimaye kuchukua uamuzi wa kujiua.

Hata hivyo, alisema ugonjwa wa akili unatibika kwa mgonjwa kupewa dawa au ushauri.

Dk. Mwansisya alisema kwenye uzinduzi wa kampeni hiyo kuwa Aga Khan waliwapima wananchi magonjwa ya kurithi, shinikizo la damu, mapigo ya moyo, sukari na afya ya akili.

Akifungua kampeni hiyo, Mkuu wa Kamisheni ya Utawala na Menejimenti ya Utumishi Kamishna wa Polisi (CP) Benedict Wakulyamba, alisema kampeni hiyo inakwenda sambamba na utoaji wa elimu.

"Askari wote kuanzia maofisa mjitokeze kupima afya, wengi mnaogopa kupima, huduma za upasuaji mdogo zinatolewa hivyo tutumie fursa hii," alisema Wakulyamba.

Alilitaka Jeshi la Polisi kusambaza huduma hiyo ya upimaji mikoa mingine kwa kuwa ni msaada mkubwa katika utambuzi wa afya.

"Jeshi la Polisi lina zahanati kila mkoa bara na visiwani, vituo vya afya katika badhi ya maeneo na hospitali kuu jijini Dar es Salaam. Kuzinduliwa kwa kampeni hii kutasaidia jamii kufikiwa na huduma ya afya na utaratibu huu tunatakiwa kuuendeleza," alisema Wakulyamba.

Naye Mganga Mkuu wa Jeshi la Polisi, Dk. Charles Msenga, alisema kampeni hiyo iliyozinduliwa itawapa nafasi askari polisi na watumishi raia kupima sukari, shinikizo la damu, maambukizi ya homa ya ini, saratani ya shingo ya kizazi, saratani ya matiti, virusi vya Ukimwi na magonjwa ya kuambukiza.

# Marehemu 193 watumika kukomba mamilioni Tasaf

**Na Godfrey Mushi,** HAI

MKUU wa Wilaya ya Hai mkoani Kilimanjaro, Lengai Ole Sabaya, amebainisha upigaji wa Sh. milioni 324 zinazotolewa na serikali kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (Tasaf).

Miongoni mwa mbinu zilizobainika kutumika kufuja fedha hizo ni kuweka majina hewa ya kaya zinazopaswa kunufaika na mfuko huo.

Pia, imebainika mamilioni ya shilingi yameliwa kwa kudanganya yamelipwa kwa wanufaika 193 wa Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini unaotekelezwa na Tasaf ilhali watu hao walishafariki dunia.

Akizungumza jana na wanufaika wa mpango huo wilayani hapa, Ole Sabaya alisema katika upigaji huo ulioisababishia serikali hasara ya mamilioni ya shilingi, kamati maalum ya uchunguzi yenye wajumbe saba pia imewabaini watu wengine 304 ambao hawana sifa za kuwapo kwenye mpango wa kunusuru kaya masikini wananufaika na mpango huo.

Alibainisha kuwa marehemu 193 wanatumika kuchota kila mwezi Sh. milioni 44.5 kupitia mpango huo wa kunusuru kaya na watu wengine 516 wanaonufaika na mpango huo, taarifa zao hazijulikani na hawapo kwenye orodha ya watu wanaotakiwa kunufaika.

"Kama ambavyo kamati ilieleza, watu 193 wao wanaitwa wanufaika wa Tasaf, wameendelea kupewa fedha lakini wameshafariki dunia muda mrefu uliopita.

"OCD (Mkuu wa Polisi wa Wilaya) na Takukuru (Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa) njooni hapa, nawakabidhi orodha ya kwanza hii.

"Jambo la pili, tumekuta watu 516, hawa wapo kwenye orodha ya watu wanaopaswa kupewa mafao, lakini tumekwenda vijijini huko na kamati hii yenye vyombo vyote vya ulinzi na usalama, tumekuta hawa watu ni hewa na hawako huko vijijini.

"Kwa uchunguzi uliofanyika, tumekuta watu 304 na wamegundulika ni watu wenye uwezo mkubwa kabisa kuliko hata wengine tuliopo hapa.

"Tukagundua huko kuna watu wana ekari za mashamba ya miwa, wanaitwa wanufaika wa Tasaf. Tuna ushahidi wa ekari nne, wana magari watu hawa, wana nyumba za kupangisha na yuko

INAENDELEA UK.26

# Uhamiaji yachukua maelezo ya Kabendera

**Na Romana Mallya**

IDARA ya Uhamiaji imesema imeshachukua maelezo ya mwandishi wa habari za uchumi, Erick Kabendera ambaye wanamshikilia kwa uchunguzi kuhusu uraia wake.

Kamishna wa Uraia na Hati za Kusafiria wa Idara ya Uhamiaji, Gerald Kihinga, alisema wakati akizungumza na waandishi wa habari.

"Tulipata taarifa kutoka kwa wasamaria wema kuhusu utata wa uraia wake, baada ya idara kupata taarifa tulianza kuzifanyia kazi, hata hivyo Kabendera hajawahi kuhojiwa kuhusu uraia wake pamoja na kutumiwa barua ya wito mara nyingi," alisema.

Kihinga alisema idara yao kwa kushirikiana na Jeshi la Polisi ilimtafuta na kumpata na jana (leo) walikuwa naye wakimhoji kuhusu utata wa uraia wake.

Alisema uhakiki wa uraia wenye utata umekuwa ukifanywa kwa watu mbalimbali wakiwamo watu mashuhuri.

"Suala hili limekuwa kubwa kwa sababu Kabendera ni mwandishi wa habari, lakini tuna watu wengi ambao tunawahoji, ingekuwa maadili yanaruhusu ningewatajia watu tunaowahoji kwasababu wapo wengi hata nikiwasema hapa mnaweza kushangaa," alisema.

"Lakini hatujaweka wazi kwa sababu watu hawa siyo wakukimbia, wamekuwa wakitoa ushirikiano kila tunachowaambia walete wanaleta tofauti na Kabendera. Idara ya Uhamiaji imekuwa ikishirikiana na vyombo mbalimbali vya ulinzi na usalama katika kutekeleza majukumu yake, suala hili siyo geni," alisema.

Aliomba jamii kuendelea kutoa ushirikiano na kutoa taarifa mbalimbali pale wanapoona kuna utata wa uraia kwa mtu.

Kamishna Kihinga alisema, Kabendera hajawahi kukamatwa na hiyo ni mara yake ya kwanza. Kuhusu muda ambao watamshikilia, alisema itategemea na ushirikiano wa mhusika kwa sababu wanapomwita mtu na akatoa ushirikiano wa kupeleka wanavyovihitaji, uchunguzi huisha mapema.

"Kama hutupi ushirikiano suala hilo huchukua muda mrefu na wakati mwingine huwa tunavuka mipaka tunakwenda nchi nyingine kufanya uchunguzi, lini tutamaliza itategemeana na ushirikiano atakaotoa mhusika," alisema.

Alisema hadi jana walikuwa wameshachukua maelezo yake na taarifa ambazo walikuwa wamezikusanya ili waanze uchunguzi.

"Kuna baadhi ya vitu tulimwomba atuletee, ameahidi atatuletea leo (jana) kama atafanya hivyo atakuwa ameturahisishia sana uchunguzi wetu. Tunapomchunguza mtu hatuangalii rangi, sura, mamlaka aliyonayo au kazi, tunachunguza uraia," alisema.

Alisema wao wanatumia njia ya kumwita mtu ili kumhoji, lakini akikataa wanakwenda kumkamata na kwamba Kabendera aliwahi kutuhumiwa kwamba siyo raia wa Tanzania mwaka 2013.

Alisema amekuwa akiitwa mara kadhaa bila kufika kwa ajili ya mahojiano na walipokwenda kumkamata walivaa kiraia ili isiwe rahisi kwao kutambulika.

HABARI KITAIFA

# JKT waingia barabarani kufanya usafi

Na Mary Geofrey

SIKU mbili baada ya Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Paul Makonda kuagiza usafi wa mazingira kwa kila mkazi wa mkoa huo kwa ajili ya maandalizi ya kupokea wageni watakaohudhuria mkutano wa Nchi za Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (Sadc), Jeshi la Kujenga Taifa (JKT), limeanza kutekeleza agizo hilo.

Hata hivyo, baadhi ya wakazi wa jiji hilo wamekosoa hatua za kushurutishwa kufanya usafi kwa kusubiri ujio wa wageni badala ya kuwa utaratibu endelevu.

Jana Nipashe ilishuhudia vijana wa JKT katika maeneo mbalimbali ya Jiji la Dar es Salaam wakiwa wanasimamiwa na Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ), wakitekeleza agizo hilo kwa vitendo katika maeneo ya Mwenge, Msasani Namanga na Mikocheni.

Mwajuma Hassan mkazi wa Mwenge alisema kazi ya kufanya usafi ni jambo jema ingawa serikali ilitakiwa kujiandaa mapema kwa kuhakikisha maeneo yote ya jiji yana vifaa vya kuhifadhia taka na viongozi wenye dhamana wanasimamia kikamilifu.

"Tunaweza kusema serikali inafanya vizuri kuhamasisha wananchi kufanya usafi, lakini usimamizi kwenye jiji usiwe kwa ajili ya matukio kama hili, bali ufanyike wakati wote. Badala ya kutumia nguvu kazi ya JKT kusafisha jiji ambalo lingetakiwa kusafishwa na wananchi wenyewe na kuliacha lifanye shughuli za kujenga taifa," alisema Mwajuma.

Alisema wananchi wanapaswa kuzingatia kanuni za usafi kuanzia nyumbani, mitaani na maeneo yote ya jiji na kuhakikisha maeneo yote ya bustani yanayotunzwa wakati wote badala ya kuachwa.

Naye Omary Kazimoto Mkazi wa Tabata Magengeni, alisema lengo la mkuu wa mkoa huo ni nzuri isipokuwa, mpango mkakati wa utekelezaji wake siyo sahihi kwa kuwa ulitakiwa kuwa mpango endelevu.

Alisema yalitakiwa yafanyike maandalizi ya muda mrefu badala ya kutumia nguvu kwa sababu

INAENDELEA UK. 26



Mwonekano wa sehemu ya daraja la reli ya SGR litalopita juu kutoka Ilala hadi Stesheni ya Dar es Salaam linavyoonekana likimaliziwa kujengwa maeneo ya Shaurimoyo kama linavyonaswa na kamera ya Issa Michuzi, jana.

## Anayedaiwa kujinyonga aliandika wosia mzito

Na Romana Mallya

MKURUGENZI Msaidizi wa Miradi inayotekelezwa na Umoja wa Ulaya (EU) kupitia Wizara ya Fedha na Mipango, Leopold Lwajabe (56), aliyekutwa amejinyonga mkoani Pwani, aliacha wosia ofisini kwake, imebainika.

Kamanda wa Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam, Lazaro Mambosasa, aliwaambia waandishi wa habari jana kuwa Jumatatu ya wiki hii, wafanyakazi wenzake waligundua kuwa Lwajabe aliacha 'notebook' kwenye meza yake ofisini ikiwa na ujumbe wa mgawanyo wa mali zake.

"Lwajabe ambaye ni mkazi wa Kinyerezi, aliacha 'notebook' juu ya meza ofisi kwake ikiwa na ujumbe wa mgawanyo wa mali zake kwa familia yake na kwenye msiba wake ametaka wachinjwe ng'ombe wanne," alisema.

Kamanda Mambosasa alisema Julai 26, saa 2:00 asubuhi, zilipokewa taarifa kutoka kwa Mwenyekiti wa Kijiji cha Mgoza, Kiparang'anda wilaya ya Mkuranga, Mohamed Said (68) kuwa kuna mwili umeonekana kijijini hapo.

"Mwenyekiti huyo aliarifu kuwa kuna mwili wa mwanamume

INAENDELEA UK. 8

# Maalim Seif aliponza Jeshi la Polisi

Na Waandishi Wetu

NAIBU Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Hamad Masauni, amelitaka Jeshi la Polisi litafakari uwapo wake baada ya kuruhusu mwanachama mpya wa ACT-Wazalendo, Maalim Seif Shariff, kufanya mikutano ya kisiasa visiwani Zanzibar kinyume cha maagizo yaliyotolewa.

Masauni alitoa kauli hiyo juzi jioni wakati wa uzinduzi wa mradi wa maji kwenye eneo la nyumba mpya za polisi zilizoko Mahonda, Unguja. Alisema katika kipindi cha hivi karibuni alikuwa akifuatilia mitandao ya jamii na kushuhudia Maalim Seif akipokewa kwa maandamano maeneo ya Tumbatu.

"Nilipoulizwa nikaambiwa ameweka magunia, ndiyo majibu yaliyotolewa, huyu mzee siyo kiongozi wa chama chochote cha siasa, maelekezo yaliyotolewa na yanayoendelea kusimamiwa hadi sasa ambayo alitoa Amiri Jeshi Mkuu wa Nchi (Rais John Magufuli), akayazungumza Waziri wa Mambo ya Ndani ya nchi (Kangi Lugola) na mimi nikayasisitiza.

"Kutokana na kazi kubwa ambazo serikali zetu mbili ya Muungano na ya Mapinduzi Zanzibar zinazifanya, wananchi sasa hivi wanahitajika kufanya shughuli za maendeleo na waliopewa dhamana ya wananchi kusimamia kutekeleza waliyoahidi. "Tunatarajia mikutano ya hadhara ifanywe na viongozi waliochaguliwa kihalali na wananchi katika majimbo yao, hayo ndiyo maelekezo ya serikali.

"Amiri Jeshi Mkuu alishaagiza, Waziri alishaagiza na mimi naibu wake niliongezea nguvu. Leo (juzi) nataka kuacha maswali hapa, bahati mbaya kamishna wa polisi hayupo hapa, lakini ujumbe utamfikia. Ninauliza - je, mnamwogopa, mnadharau na kukebei maelekezo ya viongozi?" Masauni alihoji.

Kiongozi huyo alisema lazima nchi iongozwe kwa misingi ya nidhamu na askari wa Jeshi la Polisi walijifunza jambo hilo na kuapa.

"Haiwezekani maelekezo ambayo yanalenga kujenga misingi ya amani na utulivu katika nchi na maendeleo yachezewe. Haya ndiyo maswali nimeacha mjitathmini, mnipatie majibu. Sidhani kama jambo hilo litabaki kama lilivyo hivi sasa, ninazungumza kwa upendo," alisema.

**KONGAMANO LAVUNJIKA**

Wakati Masauni akitoa maelekezo hayo, kongamano la maridhiano ambalo lilifanyika jana visiwani Zanzibar lilivunjika majira ya saa sita mchana kutokana na Maalif Seif aliyekuwa kiongozi wake, kutakiwa kuripoti kwa Jeshi la Polisi. Mkurugenzi wa Mawasiliano wa ACT-Wazalendo, Salim Bimani, aliambia Nipashe jana kuwa wakati wakiwa wanaendelea na kongamano hilo, walifika maofisa wa Jeshi la Polisi na kuwataka walivunje.

Alidai maofisa hao pia walimtaka Maalim Seif kufika Kituo cha Polisi Madema kwa ajili ya mahojiano. "Wakati Maalim Seif akijiandaa kwenda polisi, akapigiwa simu kuwa asiende tena," Bimani alisema. Hata hivyo, Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mjini Magharib Unguja, Thobias Sedeyoka, alidai jeshi hilo halijavunja wala kuzuia kongomano hilo.

"Sisi Jeshi la Polisi hatujazuia wala kuvunja kongamano maana hiyo ni mikutano yao ya ndani, labda walikuwa washamaliza muda wao wa kufanya kongamano lakini wasisingizie kuwa tumevunja," alisema, Kongamano hilo lilikuwa maalum kuadhimisha siku ya maridhiano. Julai 31, 2010 wananchi wa Zanzibar walipiga kura ya maoni kuchagua mfumo wa serikali ya umoja wa kitaifa uanze kutekelezwa baada ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2010.


MASETO COMPANY LIMITED

**NOTISI/TANGAZO LA MNADA**

Kwa idhini tuliyopewa na **FIRST NATIONA BANK (FNB), MASETO AUCTIONEER & DEBT COLLECTOR LTD** tunatangaza kuuza dhamana za wadaiwa sugu walioshindwa kulipa mikopo yao katika Benki tajwa hapo juu kama watashindwa kulipa madeni yao ndani ya siku 14 tangu kutolewa kwa tangazo hili. Minada hii itafanyika kama inavyoonesha hapa chini;

| S/N | JINA LA MTEJA | UMILIKI WA DHAMANA | AINA YA DHAMANA NA MAHALI ILIKO | TAREHE NA MUDA WA MNADA |
|---|---|---|---|---|
| 001 | JAMES SEIF SUNGURA | JAMES SEIF SUNGURA | NYUMBA YENYE HATI MILIKI NO. 136879, L.O. NO. 530401, KIWANJA NO. 2607, BLOCK C, GOBA KUNGURU AREA – KINONDONI MUNICIPALITY | PRIVATE SALE |
| 002 | PAULINE FRANCIS KASSI | PAULINE FRANCIS KASSI | NYUMBA YENYE HATI MILIKI NO. 18150 LR MWANZA L.O. NO.254655, KIWANJA NO. 204, BLOCK F, NYEGEZI AREA – NYAMAGANA MWANZA | 15/08/2019 SAA 04:00 ASUBUHI |
| 003 | MWIKWABE CHALICHA MATIKU | MWIKWABE CHALICHA MATIKU | NYUMBA YENYE HATI MILIKI NO. 60941 LR MWANZA NO. 415133, KIWANJA NO. 166, L.O. NO. 403104, BLOCK J, BUSWELU KASIKAZINI - MWANZA | 16/08/2019 SAA 04:00 ASUBUHI |
| 004 | DIOMEDES R RUTABANZIBWA | DIOMEDES R RUTABANZIBWA | NYUMBA YENYE HATI MILIKI NO. 18200, LR MWANZA, KIWANJA NO. 192, L.O. NO. 238623, BLOCK C – NYASAKA AREA - MWANZA | 16/08/2019 SAA 08:00 MCHANA |

**Masharti ya Mnada**

1. Dhamana itauzwa kama ilivyo na mahali iliko.
2. Mnunuzi atatakiwa kulipa siku hiyo hiyo ya mnada asilimia 25% ya bei iliyofikiwa.
3. Malipo ya asilimia 75% yalipwe ndani ya siku kumi na nne (14) kukamilisha malipo yote, kushindwa kufanya hivyo mnunuzi atakuwa amepoteza malipo yote ya awali ya asilimia 25% na mnada utarudiwa tena.
4. Gharama za kuona, kukaguwa, kuhamisha umiliki, na zingine zinazoambatana au ufanana na hili ni juu ya mnunuzi.

**KWA TAARIFA ZAID WASILIANA NASI KUPITIA ANUANI HIZI:**
**MKURUGENZI MTENDAJI,**
**MASETO AUCTIONEER,**
**P.O BOX 75087,**
**DAR ES SALAAM**
**+255 765 999 000 AU +255 787 288 442**

215353902

HABARI KITAIFA

## Madiwani wataka serikali kunusuru zao la pamba

**Na Gurian Adolf,** KATAVI

BARAZA la Madiwani la Halmashauri ya Manispaa ya Mpanda mkoani Katavi, limeiomba serikali kuchukua hatua za haraka kutafuta masoko ya zao la pamba ili kunusuru wakulima ambao wamekaa miezi mitatu sasa bila kuiuza wakisubiri soko.

Pia, wajumbe hao wameiomba serikali isiangalie hali ya ushindani wa biashara wa kuongeza Sh. 100 hadi 200 kwenye kila kilo moja ya pamba bali waruhusu kuuza ili wakulima waweze kupata fedha za kujikimu.

Ombi hilo lilitolewa jana na baadhi ya madiwani katika kikao cha robo ya nne ya mwaka ya baraza hilo lililofanyika chini ya Meya wa Manispaa hiyo, Willy Mbogo.

Madiwani hao walipitisha azimio la kuiomba serikali ichukue hatua za kutafuta masoko ya zao la pamba haraka kutokana na taarifa mbalimbali zilizotolewa na madiwani kwenye baraza hilo kuwa wakulima wamekosa mnunuzi wa zao hilo mkoani humo.

Diwani wa Kata ya Makanyagio, Haidari Sumry, alisema wapo baadhi ya wakulima wa mkoa huo waliamua kulima pamba na kuacha mahindi wakitegemea kuwa wakiuza watanunua mahindi kwa ajili ya chakula.

Alisema hali hiyo imewafanya wakulima wa pamba

INAENDELEA UK. 8

# Katibu Mkuu CCM aonya wanaojipitisha Ilemela

**Na Mwandishi Wetu,** MWANZA

KATIBU Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Dk. Bashiru Ally, amesema hatashangaa Mbunge wa Ilemela jijini Mwanza, Dk. Angeline Mabula, akipita bila kupingwa ndani ya chama hicho katika uchaguzi mkuu ujao kutokana na kazi kubwa aliyoifanya kwa maendeleo ya wananchi wa jimbo hilo.

Dk. Bashiru alisema hayo juzi kwenye Uwanja wa CCM Kirumba jijini katika mkutano ulioandaliwa kwa lengo la kuelezea utekelezaji wa ilani ya CCM katika jimbo hilo.

Alisema hakuna haja kumnadi tena Dk. Mabula kwa kuwa anazo sifa zinazomwezesha kutetea kiti chake na yeyote anayetaka kuwania nafasi katika jimbo hilo, ajue kiti hicho kishakaliwa pamoja na kata zake 19.

"Ole wake anayetaka kupita mlango wa nyuma, chama kina utulivu, sitashangaa Dk. Mabula akipita bila kupingwa," Dk. Bashiru alionya.

Kiongozi huyo wa CCM aliwataka wabunge wa chama hicho kuhakikisha wanafanya ziara za kutatua kero za wananchi na kufanya vikao kwenye majimbo yao vinginevyo hawatakuwa na ulinzi wakati wa kinyanganyiro cha kupendekeza majina ya kuwania nafasi hizo.

Alisema kipaumbele kitatolewa kwa wabunge waliokuwa wakichapa kazi wakati wa ubunge wao.

Alidai kuna tofauti kubwa ya kimaendeleo wakati jimbo hilo

INAENDELEA UK. 8



Meya mpya wa Manispaa ya Ilala, Omar Kumbilamoto, akihutubia Baraza la Madiwani baada ya kuchaguliwa, jijini Dar es Salaam jana. Kumbilamoto, kabla ya uchaguzi huo, alikuwa ni Naibu Meya wa Manispaa hiyo. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Samia atahadharisha uharibifu mazingira Rufiji

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MAKAMU wa Rais, Samia Hassan, amesema kuna mzigo mkubwa wa kutunza mazingira katika mradi mkubwa wa uzalishaji umeme Rufiji ili kuhakikisha maji yanatiririka na hayazuiliki kwa shughuli yoyote.

Kauli hiyo aliitoa jana jijini hapa alipokuwa akifungua Jukwaa la maendeleo endelevu kuhusu usimamizi bora wa misitu kwa upatikanaji wa rasilimali maji endelevu lililoandaliwa na Taasisi ya Uongozi.

Alisema ni lazima kujipanga vizuri ili maji yaweze kutiririka kuanzia vyanzo vya juu vya eneo hilo na yasizuilike popote.

"Sote tunajua mabwawa ya maji makubwa yanayozalisha umeme ni kwa maendeleo yetu, na tunajua mradi mkubwa wa uzalishaji umeme Rufiji utategemea mtiririko endelevu wa maji kutoka vyanzo vikuu ikiwamo mito na madakio ambayo yanaanzia kwenye misitu na maeneo mengine," alisema.

Alibainisha kuwa mwaka juzi alikuwa na kampeni ya utiririshaji maji katika mto Ruaha kutokana na hali yake kuwa mbaya kwa kipindi hicho.

"Tulienda kuangalia upande wa mbuga ya Ruaha hali ni mbaya mno nilikuta kitu ambacho sijawahi kuona duniani, sijawahi

INAENDELEA UK. 8




## HABARI KITAIFA



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa akiongoza kikao cha utekelezaji wa haraka wa maagizo ya Rais Dk. John Pombe Magufuli, kuhusu mradi wa kufua umeme wa Mto Rufiji, kilichofanyika, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: OWM**

# Tasac yaondoa hofu kampuni za wakala wa forodha

**Na Salome Kitomari**

SHIRIKA la Uwakala wa Meli Tanzania (Tasac), limesema kuwa idadi ya kampuni za wakala wa forodha imeongezeka kwa zaidi ya asilimia 20 ikilinganishwa na mwaka 2018.

Hiyo ni kwa mujibu wa tangazo lililotolewa na Mkurugenzi Mkuu wa Tasac kwenye Nipashe jana, kuhusu utekelezaji wa Sheria ya Uwakala wa Meli Tanzania namba 14 ya mwaka 2017.

Taarifa hiyo ilisema uwapo wa shirika hilo hautasababisha madhara ya urasimu katika utoaji wa huduma, watumiaji wa bandarini kupungua, kampuni za forodha kufungwa, msongamano wa shehena bandarini na kutokuwapo kwa usawa miongoni mwa watoa huduma.

Vile vile, Tasac ilisema matokeo ya utekelezaji wa sheria ni pamoja na kuimarisha usalama, mazingira, afya za Watanzania na mapato ya taifa kwa kuruhusu shirika hilo kushiriki katika utoaji huduma zenye maslahi mapana kwa taifa.

Kwa mujibu wa taarifa hiyo, lengo ni kuzuia udanganyifu, uwasilishaji wa nyaraka na taarifa zisizo sahihi

INAENDELEA UK. 8

## Watakiwa kutumia lebo za vifungashio zilizohakikiwa

**Na Mwandishi wetu**

MKURUGENZI Mkuu wa Taasisi ya Kudhibiti Ubora wa Mbegu (Tosci), Patrick Ngwediagi, amewataka wakulima kutumia lebo iliyowekwa kwenye vifungashio kwa njia ya elektroniki kuhakiki ubora wa mbegu ikiwamo kukaguliwa na taasisi hiyo.

Kauli hiyo aliitoa juzi jijini Dar es Salaam wakati akisaini mkataba na Shirika la Mawasiliano Tanzania (TTCL), kupitia mpango wa kilimo tija wakulima watatumia huduma hiyo bure kupata taarifa ya ubora wa mbegu nchini.

"Tosci ni mamlaka inayosimamia udhibiti wa mbegu nchini, tunataka kuondoa ulaghai kwa wale wanaoghushi nembo za taasisi kusambaza mbegu zisizo na ubora, kupitia TTCL mkulima anaweza kutumia simu ya aina yoyote kutuma ujumbe kwetu kupata uhakika wa mbegu aliyoinunua kama imekaguliwa," alisema Ngwediagi.

Akifafanua zaidi alisema lengo la mkataba huo ni kuwawezesha wakulima kuwa na uhakika wa mbegu husika kama zimekaguliwa na Tosci kupitia mtandao wa TTCL.

Naye Mkurugenzi Mkuu wa TTCL, Waziri Kindamba, alisema shirika lake ni la kizalendo na kwamba kwa maelekezo ya Rais Dk. John Magufuli, wakulima wa Tanzania wajielekeze kwenye kilimo tija.

"Kilimo tija kinaanzia kwenye mbegu bora na mkulima lazima awe na uhakika kwa kupitia TTCL wakulima watapa nafasi kutuma ujumbe mfupi kupitia namba zitakazowekwa kwenye lebo ya vifungashio vya Tosci ili kujiridhisha," alisema Kindamba.

## Wataalamu wa viwango vya maji nchi 31 wakutana Dar

**Na Joseph Mwendapole**

WATAALAMU wa masuala ya viwango kutoka nchi 31 za Afrika wamekutana jijini Dar es Salaam kujadili na kuainisha viwango vya majisafi na taka, kwa lengo la kupitisha kiwango kimoja kitakachotumika kwa nchi zote za Afrika.

Akizungumza Dar es Salaam jana, Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Viwango Tanzania (TBS), Dk. Yusuf Ngenya, alisema mkutano huo umekutanisha wataalamu kutoka nchi wanachama wa Shirika la Viwango la Afrika (ARSO).

Kwa mujibu wa Dk. Ngenya nchi hizo zipo katika hatua za kutengeneza kiwango kimoja kitakachotumika katika upande wa majisafi na uchakataji wa majitaka.

Alisema kuna njia na hatua nyingi za kutengeneza kiwango kimoja, ikiwamo uainishaji viwango vyote na kupata kiwango kimoja kitakachotumika.

"Kila nchi ina viwango vyake vya ubora, lakini katika mkutano huu wa leo (jana) umekutanisha wadau wote wanachama wa ARSO, ili kuhakikisha tunapata kiwango kimoja kitakachotumika katika majisafi na taka kwa nchi zote za Afrika," alisema Dk. Ngenya.

Dk. Ngenya alisema kuna faida kubwa kwa nchi za Afrika kutumia kiwango kimoja, hususan kwa upande wa wafanyabiashara wa hapa nchini wanapopeleka biashara zao kwenye nchi nyingine za Afrika zikiwa na nembo za TBS, kwa kuwa hawezi kupata usumbufu wowote.

"Ili kwenda vizuri katika biashara na kuondoa vikwazo mbalimbali kwa wafanyabiashara, inabidi viwango hivyo vifanyiwe uainishaji na kuwa na kiwango kimoja kitakachokubalika sehemu zote," alifafanua Dk. Ngenya.

INAENDELEA UK. 8



MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Wafanyabiashara usafirishaji binadamu wakomeshwe

**MAPEMA** wiki hii serikali ilitoa taarifa ya kuwapo kwa baadhi ya watu wanaofanya biashara ya kusafirisha binadamu kwa kuchukua watoto wenye ulemavu na kuwapeleka nje ya nchi kuwa ombaomba.

Taarifa hiyo ilitolewa katika maadhimisho ya kitaifa ya Siku ya Kupinga Biashara Haramu ya Usafirishaji Binadamu, iliyofanyika juzi. Serikali imeonya wanaofanya biashara hiyo haramu, mwisho wao umefika na kuwataka wafute shughuli nyingine.

Takwimu zilizotolewa katika maadhimisho hayo zimeonyesha kuwa kipindi cha miaka mitatu kuanzia 2016, wadau wameokoa jumla ya waathirika 390. Kati yao wanawake ni 373 na 320 walikuwa chini ya umri wa miaka 18.

Biashara ya usafirishaji binadamu imeshamiri duniani na walengwa wakubwa ni wasichana na watoto ambao hudanganywa kwenda nje ya nchi kutafutiwa ajira, lakini kinyume chake wamekuwa wakipata mateso makubwa na wengine huishia kutumikishwa kingono.

Wengine hupata mateso ya kupigwa na kunyimwa chakula na baadhi yao hupoteza maisha.

Kuibuka kwa biashara haramu ya usafirishaji wa binadamu dhidi ya watu wenye ulemavu wa miguu kwa ajili ya kuwatumikisha kama ombaomba kwenye mitaa yenye mkusanyiko wa watu au barabara zenye foleni, ni ukiukwaji mkubwa wa haki za binadamu. Kibaya zaidi wanaondolewa kwenye nchi yao na kupelekwa nchi ya kigeni ambayo hata kupata msaada ni vigumu.

Watu hao wanahitaji kusaidiwa sio kutumikishwa kwa kukaa barabarani na kupigwa jua kuanzia asubuhi mpaka jua linapozama, pengine bila kupata chakula.

Ni jambo linalotia faraja baada ya serikali kugundua watu wanaofanya biashara hiyo na kufanya mawasiliano na mamlaka za Kenya ili kuwarejesha watoto watatu wa Kitanzania waliookolewa nchini humo wakiwa wanatumikishwa kama ombaomba, wawili kati yao wakiwa na ulemavu.

Serikali imeonya mtu yeyote atakayemchukua mtoto au kumdanganya na kumfanya mtumwa ama wa kumbebea dawa za kulevya, kuuza pombe, kufanya uhalifu mwingine wowote pamoja na danguro, kuacha mara moja.

Imegundulika pia kuwa baadhi ya watu huwachukua binadamu wenzao na kwenda kuwatumikisha kwenye mashamba, viwandani na wengine nyumbani.

Kwa Tanzania mikoa iliyotajwa kuongoza kwa utumikishaji wa biashara hiyo kuwa ni Dar es Salaam, Mwanza, Kigoma, Geita, Dodoma, Singida, Shinyanga, Tanga na Morogoro.

Katika kipindi cha miaka minne kuanzia mwaka 2016, Jeshi la Polisi lilifanya upelelezi wa matukio 50 ya aina hiyo dhidi ya watuhumiwa 76 na 60 walipatikana na hatia na kuhukumiwa kulipa faini au kutumikia kifungo.

Kati ya hao wanawake ni saba. Waathirika wa biashara haramu ya binadamu wengi ni wanawake wenye umri kati ya miaka 16 hadi 26 ambao hupelekwa nchi za India, Thailand, China, Indonesia na Malaysia kwa ajili ya kutumikishwa ukahaba.


Wanaopelekwa kutumikishwa kazi za ndani hupelekwa nchi za Oman na baadhi Uarabuni ikiwamo Irak.

Kamati ya Kitaifa ya Kupambana na Biashara imesema mwaka 2018/19, wahalifu waliokamatwa ni 36, kesi zilizofikishwa mahakamani ni 33, waathirika waliookolewa ni 147. Kati yao 141 walikamatwa Tanzania na sita nje ya nchi.

Wananchi wanatakiwa kutoa taarifa kwa vyombo vya ulinzi na usalama kila kunapokuwa na kiashiria cha biashara hiyo ili kuondoa tatizo hilo nchini.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Meneja Matangazo:** Kauthar D'souza, 0767 223311
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




Muungwana Lazima Nilonge



Na Sabato Kasika

# Huduma bure ugonjwa huu isisubiri maadhimisho

**HOMA** ya Ini (Hepatitis B), ni miongoni mwa magonjwa, yanayoelezwa kuwa hatari na inazidi kuongezeka, huku wananchi wakiwa hawana uelewa wa kutosha kuhusu homa hiyo.

Kaimu Mkurugenzi wa Kinga, Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Janeth Mghamba anasema, kwa sasa kiwango cha homa ya ini kimefikia asilimia 4.5.

Lakini bahati mbaya, hakuna uelewa wa kutosha miongoni mwa jamii kuhusu ugonjwa huo na sasa wizara yenye dhamana, imeweka mikakati ya kupunguza maambukizi mapya ya homa ya ini kwa asilimia 90 ifikapo mwaka 2030.

Dk. Mghamba alitamka Jumapili iliyopita kwenye maadhimisho ya Siku ya Homa Duniani, ambayo kitaifa yalifanyika mkoani Dodoma, akielezea mikakati hiyo ya serikali.

Wakati serikali ikiwa na mikakati ya kuwaokoa Watanzania dhidi ya ugonjwa huo, ipo haja ya kuangalia uwezekano wa kutoa huduma hiyo bure kama ilivyo kwenye ugonjwa wa Kifua Kikuu na Ukimwi.

Hatua hii pamoja na utoaji wa elimu kwa jamii kuhusu homa ya ini, inaweza kusaidia kuokoa maisha ya Watanzania wenye hali ya chini na wasio na uelewa kuhusu ugonjwa huo unaotajwa kuwa ni hatari.

Kwa mfano, kongamano la madaktari na wauguzi lililofanyika hivi karibuni katika Hospitali ya Taifa ya Muhimbili, Dk. John Rwegesha, alibainisha kuwa vipimo kwa hospitali za binafsi ni kubwa.

Daktari huyo bingwa wa homa ya ini, anasema, kipimo tu ni Sh 500,000 hadi kupona unaweza kufikia hata Sh. milioni mbili, hali ambayo inaweza kumuwia vigumu mtu wa maisha ya kawaida kumudu gharama hiyo.

Hivyo, kwa hali kama hiyo, kuna haja ya kuangalia uwezekano wa kutoa huduma hiyo bure kwenye hospitali za umma kutokana na ukweli kwamba Watanzania wengi hali zao kimaisha ni za kawaida.

Suala la upimaji lisiwe hadi wakati wa maadhimisho ya Siku ya Homa Ini Duniani tu bali liwe endelevu kwa ajili ya kubaini zaidi ukubwa wa jinsi lilivyo na kukabiliana nalo kadri inavyowezekana. Kusubiri hadi maadhimisho ya siku hiyo ndipo vipimo vifanyike bure, sidhani kwamba njia hiyo inaweza kusaidia kumaliza tatizo, bali uandaliwe mkakati maalum wa kuhakikisha huduma hiyo inatolewa bure wakati wote.

Katika maadhimisho ya mwaka huu, zipo baadhi ya hospitali zilizotoa bure huduma ya kupima homa ya ini zikiwamo za Taasisi ya Saratani Ocean Road na Hospitali ya Benjamin Mkapa, jijini Dodoma.

Mkurugenzi wa Hospitali ya Benjamin Mkapa, Dk. Alphonce Chandika, anasema watu zaidi ya 400 walijitokeza kupima na 13 waligundulika kuwa na ugonjwa huo, na akashauri elimu itolewe kwa Watanzania wengi.

Taasisi ya Saratani ya Ocean Road, ilipanga kuchunguza virusi vya homa ya ini kwa watu 1,000 kuanzia Julai 28 hadi 31 mwaka huu bila malipo, ikiwa sehemu ya kuadhimisha Siku ya Homa ya Ini Duniani. Mkurugenzi wa Idara ya Kinga na Huduma za Saratani, Dk. Crispin Kihesa, anasema kwa kawaida huwa wanafanya kipimo cha ugonjwa huo kwa Sh. 10,000, lakini katika maadhimisho wakaamua kupima bure.

Dk. Kihesa anasema, hatua hiyo imechukuliwa ili kwenda sambamba na kaulimbiu ya maadhimisho ya Siku ya Homa ya Ini Duniani, ambayo ni 'wekeza kwenye mapambano ya homa ya ini'.

Nikirejea kwenye hoja yangu, ni kwamba dawa za kifua kikuu zinatolewa bure na pia kufumbaza virusi vya Ukimwi nazo hutolewa bure, ndio maana nikasema hata dawa za homa ya ini nazo zitolewe bure.

Wakati huduma ikitolewa bure, elimu itolewe kwa wingi ili kuwafanya Watanzania wawe na uelewe mpana, ambao utawasaidia kuwa makini dhidi ya ugonjwa huo unaotajwa kuwa tishio. Wataalam wa afya ni kwamba mtu anaweza kupata maambukizi ya homa ya Ini, na asionyeshe dalili yoyote, na kwamba watu wengi hawaonyeshi haraka dalili za maambukizi kwa kipindi cha awali cha ugonjwa huo.

Dalili nyingine za ugonjwa huo huonekana pale umekolea mwilini, huku ngozi na macho vikiwa na rangi ya njano, na wakati mwingine hata mkojo huwa wa njano, kukosa nguvu, kichefuchefu na kutapika.

Wanataja dalili nyingine kuwa ni homa, tumbo kuuma upande wa juu kulia, na kuumwa kichwa, huku baadhi ya watu wenye ugonjwa huo wakishindwa kufanya kazi na hata wengine kufariki dunia.

# BARUA MJADALA

## Wajasiriamali tuwe wasafi

**Mhariri,**

*NIMEAMUA kutoa neno gazetini, nikiwa na mtazamo kwa linalonikera kutoka kwa ndugu zangu wafanyabiashara wadogo.*

*Ni jambo linalotia moyo sana kuona Rais wetu Dk John Magufuli, ametuwekea mazingira chanya sisi wadogo katika namna ya kufanya biashara zetu.*

*Kuna jambo moja kwamba tulifunguliwa jamii ya Machinga na wengine wadogo kuwa huru katika kufanya biashara zetu pasipo bugudha.*

*Sasa imeenda mbali kwa kuingia hatua ya pili, kwamba tumeandaliwa vitambulisho maalum tusibugudhiwe katika nyendo za biashara tulizo nazo.*

*Kama ulivyo usemi ukishikwa nawe shikamana, jambo zito liko katika hoja kwamba hapa jijini Dar es Salaam, tunakofanya biashara, tunaendesha shughuli zetu katika mazingira yasiyoridhisha kiafya.*


*Unakuta watu wanaendesha ujasirimali wa kuuza ama mihogo, maandazi au bila hata ya kuzifunika. Hii maana yake nini? Sisi haitusaidii, wala hata kuisaidia serikali yetu katika mapambano haya ya kiafya na mazingira.*

*Nadhani tuanze kuibadilika kuweka bidhaa zetu katika mazingira nadhifu na yanayoendana na kanuni za usafi, katika katika namna inavyotakiwa.*

*Hivi inagharimu kiasi gani katika kupata kifaa safi na mfuniko wake unawekaji bidhaa hizi katika mazingira safi?*

*Wakati tunatetewa na kupiganiwa, nasi tuonyeshe mshikamano kwa serikali kufuata kanuni kama vile za afya na usalama mwingine unaotusaidia sisi na serikali, pia tunakuwa tunapunguza gharama.*

**Shabani Mash,**
**Kisukuru, Dar es Salaam.**




# 'Big up' Dk. Mwakyembe safari ya kumjulia hali Jellah Mtagwa

**Na Peter Orwa**

NALAZIMIKA kuanza na tamko "Ndaga fijo Mwalafyale." Samahani muda na nafasi haitoshi kufafanua, zaidi ya kuwasaidia kwa wale 'wajanga' maana yake 'ahsante mfalme fulani...'

Kwanini hivyo? Naam! Kwa nafasi yako hapo ofisini na kule jimboni Kyela unatosha kuwa 'Mwalafyale' japo sina uhakika sana na ukoo wako. Pia, haipingiki ninapogeukia taaluma, wizara ulizotumikia, ulikotokea na ajira ya ujanani 'unatosha' katika heshima hiyo.

Siishii hapo. Nakuongeza dozi ya pili "Ndaga fijo Nnyambala." Naam! Hapo 'wajanga' siwafafanulii. Nikuambie tu 'unafiti' bila ya chenga.

Nimeanza wajibu wangu kwa 'ndaga fijo' au asante kila kona, nikiiga ulivyo ustaraabu na mila yako, kwani si Uyole, Kiwira, Busokelo, Ushirika, Itungi, Itunge hadi Matema.

Kwanini nianze kukusifu tena kinyumbani mapema hii? Naam! Umenigusa wewe mwandishi wa habari na mwanasheria uliyebobea darasani, ambaye leo una dhamana ya kutusimamia sisi na wanamichezo, namna ulivyoguswa na kinachomkuta kijana wa Hayati Mzee Tabu Mangara kupitia timu ya Pan African.

Leo inatimu miaka 10, Jellah Mtagwah, ambaye ana umri wa babu sasa, anasumbuliwa na maradhi yu kupooza akiugua katika maficho ya makazi yake, Manzese jijini Dar es Salaam.

Huko nyuma baada ya kutumikia ajira katika kiwanda kimoja katika Barabara ya Nyerere jina lake lilipoanza kutoweka mbele ya uzao wa digitali, wapenzi wa soka tuliobahatika kumfahamu na mashabiki wa mambo ya zamani, tulianza kusikia simulizi ya matatizo kiafya hadi makuu ya leo.

Mwanafunzi huyu wa zamani kutoka Shule ya Sekondari Mzumbe, huko Morogoro kulikochonga kipaji chake cha soka hata kukamweza juu kisoka ana mengi sana kubeba sura ya kitaifa.

Shirika la Posta Tanzania ambalo wakati huo ilikuwa 'kila kitu' katika mawasiliano ya maandishi katika zama hizo za analogi, picha ya Jellah Mtagwa ilihalalishwa kutumika katika stempu zama hizo za "salamu zikufikie kama mchanga wa bahari..."

Pia, ukirejea katika timu yake aliyodumu nayo katika misimu mingi ya ligi, kazi yake inajulikana sana. Hata ukidukua siri ya timu ya Pan African, ambao iliundwa na vijana na waasi wa mtaa wa Jangwani, ana mchango mkubwa wa ufanisi uliompa heshima Mzee Mangara.

Pan Africa, waliojikita katika jezi za manjano na bluu, walibuni mtindo wa kiufundi maarufu 'off side trick' kwa kila mshambuliaji anajikuta 'amezidi' bila ya kupenda. Walizitesa sana timu nyingi, wakiwamo wazazi wao wakazi wa Jangwani.

Hapo ndiko alikopatikana katika nafasi ya mlinzi wa katikati katika ubia wa karuibu na Injinia Leodgar Tenga, wao walishibana mithili ya pacha wa sauti kiatika muziki wa dansi.

Nikudokolee tu ile tabia yao ya aina yake uwanjani, akiwa na Tenga, mmoja wao anasonga mbele kushambulia, mwingine anabaki lindoni. Haijapata kutokea jamani!

Hapo ulinzi kulia na kushoto mianya ilizibwa na Jafari Abadulharman na Mohamed Hashim Mkweche, nyuma yao golini amekaa Juma Pondamali 'Mensah' na anayeunganisha katikati kusonga mbele na kulilinda goli, mbia wao Mohamed Rishard 'Adolf.'

Naamua kukumbuka hayo, baada ya kufurahishwa na uamuzi wa Dk. Mwakyembe juzi kutambua kazi nzuri ya Jellah na wenzake na matatizo yanayowapata wanasoka hao ambao hasa ni wa uzao wake kiumri; haijazidi wala kupungua.

Rais, Dk. John Magufuli, alishaonyesha mfano wakati fulani hata akampatia Peter Tino shilingi milioni tano za papo kwa hapo. Huyu ni mwenzao Jellah, aliyetumikia safu ya ushambuliaji ya timu ya Taifa na Pan African.

Alikuwa wazi kuhusu mchango wao katika soka la Afrika, walipoonyesha mazito nchini Nigeria, ambako Pan African inajulikana kuitesa klabu ya Ibadan Shooting Stars.

Niseme Dk. Mwakyembe kupitia kitendo chako, katika hatua ya haraka inabeba wasifu wenye sura kuu sita. Mosi umewajibika vilivyo kama waziri mwenye dhamana na michezo nchini.

Pili, umeendeleza dhana ya uwajibikaji katika sauti anayoipaza Rais Dk, Magufuli, tena wewe ukiwa katika safu ya 'first eleven.' Kwa kifupi tumeiona 'hapa kazi tu' ofisini kwako katika eneo hilo la soka kwa maveterani.

Niende mbali, Dk. Mwakyembe, umewajibikia taaluma yao, kwani suala la haki za binadamu ni moja ya maeneo ninayoamini zimekushiba; nadharia zimekujaa kichwani, vitabu na majarida kabatini, una sifa ya uwakili wa sheria na ulishakuwa waziri mwenye dhamana katika mtaa huo.

Najua pia u- mcha Mungu katika hilo, unawajibikia kile kinachotamkwa katika maandiko 'kuwasadia waziojiweza' huku la mwisho ni mdau wa soka ukitoa mchango wako katka mchezo huo.

Nilipiga makofi nilipokushuhudia katika runinga juzi siku ukionyesha kusikitika na kuguswa na masahibu yanayomkuta Jellah, ukaahidi 'kufanya kitu' na 'utarudi kumtebelea baada ya wiki.'

Hiyo safi sana ikisikika inatoka kinywani kwa waziri, mwanasheria, mdau wa soka na mcha Mungu, hasa mhitaji alipolalama kutopata msaada au kufutawa kwa mfano wako.

Naamini ziara yako ni mwanzo wa mafanikio ya kukomboka kiafya kwa Jellah Mtagwa 'age mate' wako.

## KABWELA

**Na Fadhili Mohammed**




## WASILIANA NASI:

TUNAKARIBISHA BARUA NA MAONI YA MSOMAJI, UNAWEZA KUTUMA KUPITIA KWA MHARIRI S.L.P. 31042, DAR ES SALAAM AU mhariri@nipashe.co.tz

# Anayedaiwa kujinyonga aliandika wosia

INATOKA UK. 3

ukiwa umening'inia kwenye mti wa mwembe. Polisi walifika eneo la tukio na kuukuta. Uchunguzi wa awali ulibaini kuwa eneo la tukio hapakuwa na viashiria vyovyote vya kujitetea wakati wa tukio.

"Mwili haukuwa na jeraha lolote isipokuwa shingoni kulikuwa na kamba ya nailoni aliyotumia kujinyonga. Mwili wake ulishushwa na kufanyiwa upekuzi na kwenye mfuko wa kulia wa suruali zilikutwa Sh. 90,000 na mfuko wa kushoto Sh. 98,000 na saa ya mkononi," alisema Mambosasa.

Kamanda Mambosasa alisema mfuko wa nyuma kulikuwa na pochi ndani yake iliyokutwa Dola 10 za Marekani na kitambulisho cha mpigakura.

"Wananchi waliitwa kuutambua mwili huo lakini hakuna aliyemfahamu. Baada ya hapo, mwili ulichukuliwa na kuhifadhiwa Hospitali ya Wilaya ya Mkuranga kwa utambuzi na uchunguzi wa daktari na kufungua jalada la kosa la kujinyonga," alisema.

Mambosasa alisema upelelezi uliendelea ikiwa ni pamoja na kuwatafuta ndugu wa marehemu. Alisema Jumatatu ya wiki hii saa 5:00 asubuhi, walipatikana ndugu, Meneja Beichumira ambaye ni mwalimu mkazi wa Babati, mkoani Manyara na mfanyakazi mwenzake, Jonathan Herman.

"Wote kwa pamoja waliutambua mwili na kueleza kuwa Julai 25, saa 12:00 asubuhi, Lwajabe alitoka nyumbani kwake kwenda ofisini akiwa na dereva wake na baadaye alimtuma dereva amfuatie simu yake aliyokuwa ameisahau nyumbani kwake Kinyerezi," alisema na kuongeza kuwa simu hiyo ilibainika ilikuwa imefutwa kila kitu.

Alisema baada ya dereva huyo kuondoka kwenda Kinyerezi, Lwajabe alitoweka ofisini na kwenda kusikojulikana hadi Julai 26, alipogundulika akiwa amejinyonga huko Mkuranga.

"Hata hivyo, taarifa kutoka kwa mfanyakazi mwenzake zinasema kuwa Lwajabe alikuwa amepunguza kasi katika utendaji jambo ambalo si kawaida yake na hata kazi za muhimu alikuwa akimpa msaidizi wake azifanye," alisema. Kwa mujibu wa Mambosasa, mwili wake umehamishiwa Hospitali ya Taifa ya Muhimbili (MNH) kwa uchunguzi zaidi. Alisema licha ya kifo chake kusababishwa na kujinyonga, chanzo hicho bado kinachunguzwa.

# Samia atahadharisha uharibifu mazingira Rufiji

INATOKA UK. 4

kuona kama wanyama wanaweza kupanga foleni kunywa maji na wanamtegemea tembo ambaye anachimba shimo ndio wanakunywa machozi yalinitoka,"alisema.

Alisema baada ya kuona hali hiyo alilazimika kuandaa kampeni maalum kwa kushirikiana na taasisi mbalimbali ikiwamo Shirika la Wanyapori (WWF) na ndani ya miezi sita hali ilirejea kuwa nzuri kwenye mto huo.

"Nilikuta hali nzuri viboko wanaogelea, sasa ni kule juu kunakotegemea kumimina maji kwenye mradi wa matrilioni tunaotekeleza sasa Rufiji una mchango mkubwa wa kutiririsha maji," alisema.

Samia alisema wakati fedha nyingi zinatumbukizwa kwenye mradi huo wajue kuna mzigo mkubwa wa kutunza mazingira kuanzia vyanzo vya juu ili viweze kutiririsha maji na yasizuilike popote.

"Iwe kwa kilimo au shughuli yoyote ile tujipange vizuri tutumie rasilimali hizi ili maji yatiririke,"alisema.

Alifafanua kuwa mto Ruaha Mkuu ni tegemeo kubwa kwa ustawi wa wanyamapori na uzalishaji umeme kwenye mabwawa ya Mtera na Kidatu.

Alizitaka taasisi na mamlaka husika kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo kuongeza jitihada ya kusimamia ipasavyo rasilimali maji na misitu.

Alieleza kuwa Tanzania ina jumla ya hekari milioni 48 za misitu na takwimu zinaonyesha kuwa kiasi cha upotevu wa misitu kwasasa ni kikubwa na bila kuweka jitihada misitu itapotea.

Vile vile, alisema takwimu zilizotolewa na Chuo Kikuu cha Kilimo Sokoine cha Morogoro mwaka 2017 zinaonyesha kiwango kimefikia hekta 469,420 kwa mwaka, sawa na ongezeko la hekta 100,000 ndani ya miaka miwili.

"Hali kama hii siyo rafiki kwa upatikanaji endelevu wa rasilimali maji, kutoweka kwa misitu kunasababisha hasara kubwa kwa uchumi wetu,"alisema.

Aliagiza wadau wa mazingira kutekeleza Sheria, Kanuni na maandiko ili kuhimiza utunzaji wa rasilimali misitu na kurahisisha upatikanaji wa rasilimali za maji.

Akimkaribisha Samia, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, George Simbachawene alisema Rais John Magufuli amempa kazi ambayo aliitaka.

"Mazingira ni sehemu ambayo ilikuwa inaniuma sana, na sikudhani kama siku moja nitapata nafasi ya kuisimamia,"alisema.

Hata hivyo alisema rasilimali zinazoingia kwa ajili ya kuokoa mazingira nchini ni nyingi na zinapitia kwa wadau mbalimbali, lakini matokeo kwa jamii ni madogo.

Simbachawene alisema vyanzo vya maji vinaharibiwa kutokana na kukosa usimamizi huku akisema ripoti ya hali ya mazingira nchini itatolewa mwaka huu na anajua haitakuwa nzuri.

Awali, Ofisa Mtendaji Mkuu wa Taasisi ya Uongozi, Prof. Joseph Semboja, alisema jukwaa hilo litajadili uendelevu wa sekta ya maji na misitu nchini kwa kuwa zinategemeana na zinahitajika kutunzwa.

# Wataalamu wa viwango vya maji nchi 31 wakutana

INATOKA UK. 5

Vile vile, alisema kwa upande wa majitaka kutakuwa na kiwango kimoja cha kuyachakata ili yaweze kutumika tena kufanyiwa shughuli nyingine.

Kwa upande wa Katibu Mtendaji wa Shirika la Maji Afrika (AMCOW), Dk. Canisius Kanangire, alisema kuna umuhimu wa kuwapo kwa kiwango kimoja cha ubora kwa majisafi na uchakataji wa majitaka kwa nchi za Afrika.

Alisema kuwapo kwa kiwango kimoja kutasaidia kutambua majisafi na kuhakikisha yanakuwa na ubora mzuri wa kuzuia magonjwa mbalimbali kwa binadamu.

"Kuna umuhimu wa kuwa maji yaliyobora kwani watu wanakufa kwa sababu ya kunywa maji yasiokuwa salama au kuyatumia katika matumizi mbalimbali ikiwamo nyumbani na viwandani," alisema Kanangire.

Naye Meneja wa Habari na Vielelezo wa ARSO, Philip Anyango, alisema maisha ya watu ni muhimu kuliko kitu chochote, hivyo suala la maji salama haliepukiki.

Alisema katika Malengo ya Maendeleo Endelevu suala la maji ni lengo la sita, hivyo uwepo wa majisafi na salama kwa watu ni muhimu kwa afya zao.

# Katibu Mkuu CCM aonya wanaojipitisha Ilemela

INATOKA UK. 4

lilipokuwa chini ya Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema) na sasa linavyoshikiliwa na CCM.

Kwa upande wake Dk. Mabula ambaye pia ni Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, alisema jimbo lake kwa sasa limepiga hatua kubwa kimaendeleo katika sekta za elimu, afya, maji, miundombinu, uzalishaji na mifugo, viwanda na biashara pamoja na utamaduni na michezo kulinganisha na miaka iliyopita. Dk. Mabula alisema jimbo hilo limefanikiwa kujenga zahanati mbili mpya alizozitaja kuwa ni Buganda na Lukobe, Hospitali ya Wilaya na vituo vya afya vya Lumala na Nyamazogo.

Mbunge huyo wa Ilemela alisema katika sekta ya elimu wamefanikiwa kujenga shule mpya za sekondari za Kayenze, Angeline Mabula na Kisundi.

Aliongeza kuwa wamejenga pia shule za msingi mbili za Kayenzena Ihalalo aliyojengwa kwa msaada wa Serikali ya Korea Kusini.

# Madiwani wataka serikali kunusuru zao la pamba

INATOKA UK. 4

katika mkoa huo kukata tamaa ya kulima zao hilo kwa msimu ujao kutokana na kukosekana kwa soko na hivyo kutoanza maandalizi ya msimu ujao.

Alisema kutokana na kutonunuliwa kwa pamba hiyo kumeanza kuwafanya wakulima kuanza kuuza pamba yao kwa baadhi ya wafanyabiashara kwa bei ya Sh. 600 hadi 700 kwa kilo ili fedha hizo ziweze kuwasaidia kununua mahindi ya chakula. Diwani wa Kata ya Kasokola, Crisant Mwanawima, alisema wakulima wa zao hilo walihamasishwa na viongozi wao kulima zao hilo kama mbadala wa zao la tumbaku.

Alisema hali hiyo ya kukosekana kwa mnunuzi wa pamba kwa wakulima kutasababisha msimu ujao wa kilimo kuwa na kazi ya ziada ya kuwahamasisha tena wakulima kulima zao hilo ambalo ni jipya katika mkoa huo.

Naye Meya wa Manispaa ya Mpanda, Willy Mbogo, alisema tatizo la kukosekana kwa mnunuzi wa zao hilo ambalo lilitangazwa kuanza kwa ununuzi wake tangu mwezi Mei na uzinduzi kufanyika kitaifa katika Wilaya ya Tanganyika mkoani Katavi, imekuwa ni changamoto kubwa kwa wakulima kwa kukosa mnunuzi.

Alisema lengo la serikali ni kumsaidia mkulima, lakini zao hilo limekuwa kero kwa wakulima kwa kuwa wamekosa fedha za zao hilo hadi sasa na halmashauri pia zinakosa mapato ya ndani.

# Tasac yaondoa hofu kampuni za wakala wa forodha

INATOKA UK. 5

kwa mamlaka mbalimbali nchini.

"Sheria imeainisha bidhaa na meneo ya huduma ambazo zitafanywa na Tasac pekee kutokana na kuwa na maslahi mapana kwa umma ili kuepuka dhana ya Mdhibiti kuwa mshindani katika soko," alisema na kuongeza:

"Bidhaa kama madini, makinikia na mitambo yake, silaha, nyara za serikali. Maeneo ya biashara ambayo hayakuainishwa kuwa ya Tasac pekee yanaendelea kufanywa na sekta binafsi."

Tangazo la mwanzoni mwa mwezi huu (Julai 31) lilitolewa kwenye vyombo vya habari na Tasac, lilitaja mizigo hiyo ni pamoja na madini, mchanga wa madini (makinikia) mashine, vifaa, bidhaa mbalimbali, mafuta, silaha, wanyama hai na nyara za serikali.

"Kuanzia Machi 4, mwaka huu, Tasac utaanza kutekeleza jukumu la lake la kisheria la kuondosha na kusafirisha mizigo bandarini katika maeneo ya madini, makinikia, mashine, vifaa, bidhaa na bidhaa nyingine zihusuyo madini na mafuta," lilifafanua tangazo hilo.

Kwa mujibu wa tangazo hilo, Tasac inawajulisha wadau na umma kwa ujumla kuwa kuanzia tarehe hiyo hakuna msafirishaji au mpokea mizigo au taasisi yoyote itakayoruhusiwa kufanya tangazo lolote jipya kwa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) kwa lengo la kufanyakazi ya uondoshaji mizigo iliyotajwa kwenye kifunga cha 7 cha sheria hiyo.

Pia, mawakala wa usafirishaji na uondoshaji wa mizigo bandarini na wafanyakazi wao au wawakilishi wao watatakiwa kukabidhi kwa Tasac nyaraka zote za usafirishaji na uondoshaji mizigo bandarini kwa mizigo iliyotajwa ili kuiwezesha Tasac kuendelea na kazi hiyo.

Tangazo hilo lilifafanua kuwa mtu yeyote ikiwamo mawakala wa meli, wafanyakazi wa Bandari wa majini na nchi kavu na taasisi nyingine za serikali, hawatatakiwa kufanyia kazi nyaraka au kazi yoyote ambayo haijafanywa na Tasac.

Lilieleza kuwa iwapo mtu yeyote atafanya kazi hiyo ambayo imetajwa kisheria atachukuliwa hatua kwa kuwa itakuwa ni kosa la kisheria kufanya kazi ambayo siyo yake.

Ilisisitizwa kuwa wadau wote na umma kwa ujumla wanaombwa kutambua utekelezaji wa kazi hiyo utakaofanywa na Tasac utakuwa wa kisheria.

## HABARI KITAIFA




Katibu Tawala wa Mkoa wa Simiyu, Jumanne Sagini (wa pili kulia), akipokea mfano wa hundi ya Sh. milioni 30, kutoka kwa Meneja wa NMB, Kanda ya Magharibi, Sospeter Magese, kwa ajili ya udhamini wa maonyesho ya Nanenane yatakayofanyika mkoani humo kitaifa, katika hafla iliyofanyika jana. **PICHA: NMB**

# Wafanyabiashara wa Kichina wapatiwa elimu sheria ya ajira

**Na Beatrice Shayo**

CHAMA cha Waajiri Tanzania (ATE) kwa kushirikiana na Jumuiya ya Wafanyabiashara wa nchini China na Tanzania wametoa mafunzo ya elimu ya sheria za ajira na uwekezaji ili kusaidia kutatua changamoto kwa wafanyabiashara wa China waliowekeza Tanzania.

Akizungumza katika mkutano huo, Mkurugenzi Mtendaji wa ATE, Dk. Aggrey Mlimuka, alisema ATE wamekuwa wakiandaa mikutano ya aina hiyo mara kwa mara ili kujadili na kutoa elimu kuhusu sheria za kazi na ajira nchini ikiwa ni moja ya juhudi za kuboresha mazingira ya kufanya biashara kwa wawekezaji kutoka China ili kuongeza uzalishaji na ushindani wa kibiashara.

Alisema wameamua kufanya hivyo kwa sababu bado kuna kampuni ya wawekezaji na wafanyabiashara wa China ambao hawafuati taratibu za ajira na kazi nchini hivyo mafunzo hayo yatawasaidia kuongeza uzalishaji na ushindani wa kibiashara.

"Kama ilivyo kwa wafanyabiashara wengine hapa nchini, Jumuiya ya Wafanyabiashara kutoka China bado wameendelea kukumbana na changamoto nyingi zinazohusiana na uwekezaji, masuala ya kodi, utekelezaji wa sheria za kazi na ajira, ajira za wafanyakazi, mikataba, taratibu za usitishwaji wa mikataba, saa ya kazi, likizo, vibali vya kufanya kazi kwa wageni na nyingine nyingi zinazoendana na hivyo sisi ATE kwa kushirikiana na wadau wetu tumeona ni vyema kuandaa mkutano huu ili kujadili na kutafuta ufumbuzi wa changamoto hizo," alisema Dk. Mlimuka.

Aliiomba serikali kuendelea kuboresha mazingira ya kufanya biashara nchini ili kuwavutia wawekezaji wengi zaidi kutoka ndani na nje ya nchi ili kukuza uchumi wa taifa.

China na Shirikisho la Vyama vya Wafanyakazi la Norway (NHO), jana wamefanya mkutano wa kujadili fursa za uwekezaji nchini kwa wafanyabiashara kutoka nchini humo na changamoto za kibiashara wanazokutana nazo katika uwekezaji wao.

Mkutano huo umejumuisha wadau mbalimbali kutoka Kituo cha Taifa cha Uwekezaji, Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Idara ya Uhamiaji, Ofisi ya Kamishna wa Kazi na Shirikisho la Vyama vya Wafanyakazi Tanzania (TUCTA).

# TTCL, Mahakama zasaini mkataba wa bil. 4.2/-

**Na Hellen Mwango**

MAHAKAMA Tanzania imesaini mkataba wa Sh. bilioni 4.2 na Shirika la Mawasiliano nchini (TTCL), kwa ajili ya mradi wa kusambaza na kuunganisha Mkongo wa Taifa ikiwamo katika majengo 157 ya mahakama.

Mradi utakao unganishwa na mtandao huo ni Mahakama ya Rufani 1, Mahakama Kuu 16, Mahakama Kuu Maalumu (Specialized Divisions) 4, Mahakama za mkoa 29, Mahakama za Wilaya 112 na Mahakama za Mwanzo 10/zenye majengo ya kisasa na kufanya idadi kuwa 157 kwa kuanzia.

Mkurugenzi wa Tehama wa Mahakama, Enock Kaleghe, alisema mradi huo ni mpango mkakati wa miaka mitano wa Julai 2015 mpaka Juni, 2020 wa kuongeza ufanisi katika mtiririko wa shughuli za mahakama.

"Mkataba huu mradi wake una thamani ya Sh. 4,170,643,125.21, utatoa huduma za aina mbili, zitapatikana huduma za mtandao wa ndani yaani 'Data' pamoja na Intaneti katika mahakama zilizotajwa," alisema Kaleghe.

Alisema kwa kuzingatia usalama na usalama wa shughuli za mahakama ikiwamo kuunda mtandao utakaunganisha pamoja na mtandao wa serikali.

Alisema pamoja na mambo mengine, mahakama itakuwa na maboresho na mazingira wezeshi ya kubadilishana taarifa kati ya mahakama na taasisi, wadau katika mfumo mzima wa utoaji haki nchini.

Mkurugenzi Mkuu wa TTCL, Waziri Kindamba, alisema mkataba wa mradi huo ni historia kwamba mahakama imekuwa na uzalendo kwa kukubali shirika lake kutoa huduma hiyo.

Alisema huo ni uzalendo kwa kuwa watasaidia kukuza na kuongeza uchumi kupitia shirika lake.

"Kazi yetu ni kutoa huduma kabla ya muda ili twende na kasi ya kuwarudisha Watanzania kwenye mtandao wao kama mjuavyo nyumbani kumenoga," alisema Kindamba.

Naye Mtendaji Mkuu wa Mahakama nchini, Hussein Kattanga, alisema mradi huo hatua ya kwanza utachukua muda wa wiki 14 na mradi mzima ni miezi 24.

# Ukarabati MV Victoria, MV Butiama waridhisha

**Na Elizabeth Faustine, MWANZA**

KAZI ya ukarabati wa meli mbili za MV Victoria na MV Butiama inayoendelea katika Bandari ya Mwanza Kusini zimewatia moyo uongozi wa Bodi ya Shirika la Wakala wa Meli nchini (Tasac).

Mwenyekiti wa Bodi ya Tasac, Profesa Thadeo Sata, alitoa taarifa hiyo alipozungumza na waaandishi wa habari baada ya kukamilika kwa ziara ya kukagua maendeleo ya ukarabati wa meli hizo zinazotegemewa kuanza safari mwezi Machi, 2020.

Prof. Sata alisema lengo la ziara hiyo iliyoongozwa na uongozi wa kampuni ya meli MSCL ni kuhakikisha viwango vinavyohitajiwa kwa usalama wa vyombo hivyo katika kuvikarabati vinakuwa sawa.

Naye msimamizi wa miradi hiyo kutoka kampuni ya meli Mhandisi Abel Gwanafyo, alisema ujio wa bodi hiyo ni faraja kwao na kwamba watahakikisha kuwa wanafanyia kazi yale yote waliyowaelekeza.

"Viongozi hawa wamefanya ziara Kanda ya Ziwa katika kutekeleza moja ya jukumu lao kubwa la kuhakikisha kuwa viwango vinavyohitajika kwa usalama vinakuwa salama," alisema.

Mhandisi Gwanafyo alisema mpaka sasa kontena 37 kati ya 56 zilizokwama katika Bandari ya Dar es Salaam, zimewasili huku zilizosalia kuendelea kuja katika bandari hiyo.

Mradi wa ukarabati wa meli ya MV Victoria unaoigharimu serikali Sh. bilioni 22, unahusisha uwekaji wa injini mpya, jenereta mpya, mitambo ya nguvu, pamoja na vyombo vya uongozaji na uokoaji na mpaka sasa ukarabati wake umefikia asilimia 37.

Ujenzi wa meli ya MV Butiama unaogharimu Sh. bilioni tano nao unaendelea na mpaka sasa umefikia asilimia 22.5 chini ya mkandarasi Sekyung kwa kushirikiana na STX engine wanaendelea na kazi na punde meli hiyo itarudi kuanza safari zake kati ya Nansio Ukerewe kama ilivyokuwa inafanya kabla ya meli hiyo kuharibika mwaka 2010.

Septemba 3, 2018, Rais John Magufuli alishuhudia utiaji sahihi wa mikataba minne ya ujenzi wa meli mpya, ujenzi wa chelezo, ukarabati mkubwa wa meli ya MV Victoria na MV Butiama kazi ambayo tayari inaendelea chini ya usimamizi wa kampuni ya huduma za meli MSCL.

# Mjane afurahia kumiliki ardhi yake

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

MAMA mjane Zipora Sultani (65), mkazi wa Kata ya Kitangili Shinyanga Mjini ambaye ana watoto sita, amefurahia kumiliki ardhi yake tena hekari 20 ambayo alidai kutaka kudhulumiwa na majirani zake kanisa la AICT Kitangili, waliokuwa wanadai eneo hilo ni la kwao na wanataka kujenga kanisa jingine kubwa.

Alisema mwanamke anapofiwa na kuachiwa mali, ndugu pamoja na jamii inayomzunguka huanza kuzitamani mali hizo na kuanza kupanga njama za kumpokonya kwa kuonekana mwanamke ni kiumbe dhaifu asiyejua sheria, lakini kwake yeye ilikuwa tofauti alipigana na kufanikiwa kumiliki ardhi yake.

Zipora alizungumza hayo juzi kuwa ardhi hiyo hekari 20 alikabidhiwa na baba yake mzazi na kuachiwa wosia kuwa ataigawa kwa wajukuu zake wajenge nyumba na kipindi alipokuwa na mume wake hapakuwahi kutokea mgogoro wowote, lakini alipofariki ndipo kukaanza mgogoro wa kutaka kupokonywa ardhi hiyo.

"Mgogoro huu wa kutaka kupokonywa ardhi ulianza mwaka 2007, nilishangaa naletewa hati ya mashtaka nyumbani kwangu ya kuitwa kwenye Baraza la Ardhi la Kata nikiambiwa niachie ardhi ya kanisa, nilishtuka na kuchanganyikiwa na nilipofika nikaona kuna dalili za kushindwa sababu wenzangu wana pesa," alisema Zepora.

"Baada ya kuona dalili hizo ikabidi nitafute wasaidizi wa kisheria kutoka Shirika la PACESHI la hapahapa Shinyanga mjini, ambao huwa wanatoa msaada huo bure ndipo wakanisaidia na hatimaye kufanikiwa kumiliki ardhi yangu tena mwaka jana, na tayari imeshapimwa na nipo kwenye harakati za kutafuta hati," aliongeza.

Naye meneja mradi wa huduma msaada wa kisheria John Shija kutoka Shirika hilo la PACESH Shinyanga Mjini, alisema baada ya kuletewa malalamiko hayo na mteja huyo mama mjane, ikabidi wafuatilie kwanza historia ya ardhi hiyo na kubaini ilikuwa ya baba yake mzazi Zipora, mzee Sultani Masibuka.

Alisema baada ya kubaini hilo, ikabidi wawaite pande zote mbili upande wa kanisa pamoja na mjane huyo, na kutafuta suluhu kati yao ikiwa hata kesi hiyo haikupaswa kusikilizwa na Baraza la Ardhi la Kata bali ilipaswa kwenda Mahakama Kuu.

Shija alifafanua kuwa ili kesi hiyo ipate kufunguliwa kwenye Mahakama Kuu ina hitajika Sh. milioni 100, na kulitaka kanisa kama linahitaji ardhi ya mjane huyo wamlipe fidia Sh. milioni 100 na wakishindwa wamwachie ardhi yake.

Pia alisema wakienda mahakamani watashindwa ndipo kanisa hilo likamwachia mjane huyo ardhi yake.

Kwa upande wake Mchungaji wa Kanisa la AICT Kitangili, Joramu Kifotumo, alikiri kanisa kuingia kwenye mgogoro wa ardhi na mjane huyo na kubainisha ulishamalizwa na machungaji aliyepita, Daudi Kaji, ambaye alishatangulia mbele za haki, hivyo kutokana na yeye kuwa mgeni hawezi kuuzungumzia zaidi.

# Wananchi Chita Melela waishukuru Tarura

**Na Erick Mwanakulya,** MOROGORO

WANANCHI wa Kata ya Chita Melela iliyopo katika Halmashauri ya Wilaya ya Kilombero, mkoani Morogoro, wameishukuru serikali kupitia Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini (Tarura) baada ya kutatuliwa kero yao ya muda mrefu kwa kujengewa daraja la chuma (Mabey Bridge), lililopo Mto Kihansi linalojengwa chini ya ufadhili wa Shirika la Maendeleo ya Kimataifa la Uingereza (DFID).

Wananchi waliojitokeza kushuhudia ujenzi wa daraja hilo linalojengwa na wahandisi wa Tarura, wakisaidiana na Mhandisi mshauri Ebenezer Mollel, pamoja na mtaalamu wa ufundi, John Hinderer, kutoka Kampuni ya Mabey Bridge ya nchini Uingereza.

Wakielezea furaha yao kuhusu ujenzi wa daraja hilo, wananchi hao waliishukuru serikali ya awamu ya tano kwa kuwajengea daraja hilo linalowasaidia kusafirisha bidhaa zao na kupata huduma mbalimbali za kijamii.

Walisema awali walikuwa wanatumia mtumbwi kuvuka mto kwa umbali takribani kilomita 1.5. Diwani wa Kata ya Chita Melela, Chelele John, alisema serikali inastahili kupongezwa kwa kuwa daraja hilo ni kiungo muhimu katika uchumi wa kata yake pamoja na Halmashauri ya Wilaya ya Kilombero kutokana na vyanzo vya mapato katika Kata za Mlimba, Chita, Mgeta, Mangula pamoja na Mchombe, vitakusanywa kwa urahisi kutokana na uwepo wa daraja hilo.

"Tulikuwa tunatumia mtumbwi kuvuka mto na wananchi walipata adha kubwa katika kijiji chetu kwa kuwa kufikia huduma za kijamii ilikuwa changamoto kubwa, leo hii naona wahandisi wa Tarura wapo hapa katika ujenzi wa daraja hili, hii inadhihirisha kuwa wakala upo katika kuhudumia wananchi ipasavyo nasi tunawaunga mkono," alisema.

Naye, Mratibu wa Tarura Mkoa wa Morogoro, Mhandisi Godwin Mpinzile, alisema daraja la chuma la Mto Kihansi limewekwa baada ya kutengeneza Barabara ya Chita Melela yenye urefu wa kilomita 11.5 na litakuwa mkombozi kwa wananchi wa Chita kutokana na shida wanayoipata wakati wa mvua na kwamba Tarura itaendelea kuikarabati barabara hiyo hadi kuunganisha Kata ya Mlimba ili kuwarahisishia wananchi kufanya shughuli zao za kila siku.

Daraja la kisasa la chuma (Mabey Bridge), ambalo limegharimu zaidi ya Sh. milioni 700 ni moja kati ya kazi za Tarura katika kuboresha barabara na kufanya matengenezo pamoja na ujenzi wa madaraja ili kuwawezesha wananchi kufanya shughuli zao za kiuchumi.

Daraja hilo linalenga kutatua kero ya kudumu kwa wananchi wa Chita Melela kutokana na madaraja ya hapo awali kusombwa na maji pale mvua zinaponyesha na linatarajiwa kuzinduliwa hivi karibuni.



Mama mjane Zipora Sultani akionyesha eneo lake la ardhi hekari 20 alilotaka kudhulumiwa na kanisa la AICT Kitangili mjini humo. **PICHA: MARCO MADUHU**

# Mabehewa 1,165 yasafirishwa Uganda, Sudan Kusini

**Roso Jacob,** MWANZA

KUPITIA ushoroba wa kati kwa njia ya reli na meli kwa kipindi cha mwaka mmoja tangu njia hiyo ifunguliwe mwaka jana, mabehewa 1,165 sawa na tani 45,720 yamesafirishwa kwenda nchini Uganda na Sudani Kusini.

Njia hiyo ilifunguliwa Juni 24, 2018 kwa kusafirisha mabehewa 19 kutoka Bandari ya Mwanza kwenda Potbay nchini Uganda tangu usafiri huo ulipokwama kwa kipindi cha miaka 10 iliyopita.

Kauli hiyo ilitolewa jana na Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Isack Kamwelwe, wakati wa hafla ya kuutangaza ushoroba wa kati, iliyofanyika katika Bandari ya Kusini, jijini Mwanza na kusafirisha mabehewa ya msaada wa chakula kwenda Uganda na Sudan Kusini.

Waziri Kamwelwe alisema kati ya mabehewa hayo, 874 yalikuwa ya Mpango wa Chakula Duniani (WFP), ambalo limechangia kwa asilimia 75 ya mzigo wote.

Kutokana na hali hiyo, Waziri Kamwele alisema, serikali ina mpango wa kujenga meli kubwa ya mizigo itakayokuwa inahudumia nchi za Uganda na Sudan Kusini kutokana na ongezeko la mahitaji ya huduma hiyo kwa wananchi wa nchi hizo.

Waziri Kamwelwe alisema kwa sasa serikali inamiliki meli moja (Wagon Ferry) ya MV Umoja yenye uwezo wa kubeba mabehewa 19 kwa wakati mmoja.

"Serikali ina mpango wa kujenga meli nyingine ya kubeba mabehewa 50 kwa wakati mmoja sawa na tani 3000, kwa sasa imefikia hatua nzuri ya utekelezaji wa mradi huu," alisema Kamwele.

Naye Kiongozi wa WFP tawi la Tanzania, Michael Dunford, alisema kutokana na umuhimu huo, WFP ina karabati mabehewa 40 yatakowezesha usafirishaji huo.

Alisema kwa kipindi cha mwaka 2017/2018 WFP ilisafirisha tani 37,000 kwa gharama ya Dola za Marekani milioni 2.5 za chakula kupitia Reli ya Kati ya Tanzania kwa kushirikiana na Shirika la Reli Tanzania (TRC).

Naye Waziri wa Viwanda, Innocent Basungwa, ambaye alihudhuria hafla hiyo, alisema kuimarika kwa mifumo ya njia za usafirishaji nchini iendane na kasi ya uwekezaji wa kuanzisha viwanda vingi nchini.

Naye Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, John Mongella, alisema kuwapo kwa ushoroba huo kunafungua fursa mpya kwa wananchi na wafanyabiashara wa mkoa wa Mwanza.



Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Simanjiro, Yefred Myenzi, akizungumza juu ya kuanza kwa zoezi la uboreshaji wa daftari la wapigakura, ambapo wametenga vituo 149, katika mkutano uliofanyika wilayani humo Mkoa wa Manyara juzi. **PICHA: GIFT THADEY**

# Barua ya mtendaji yazua taharuki

**Novatus Makunga,** BABATI

WANANCHI wa kijiji cha Vilima Vitatu wilayani Babati, wamekumbwa na taharuki baada ya serikali wilayani hapa kuwataka kuondoka katika makazi yao ya sasa ikidaiwa ni maeneo ya malisho ya mifugo.

Wananchi hao wamewaonyesha waandishi wa habari barua ya kuwataka kuondoka iliyoandikwa Julai 24, mwaka huu na kutiwa saini na Ofisa Mtendaji wa Kijiji hicho, Hasna Shaban.

Gidajuli Gwaidanyi, mmoja wa wakazi wa kijiji hicho, alilalamikia kitendo hicho kwa madai ya kwamba imekuwa usumbufu kwao kwa kuwa kabla ya kuletewa barua hiyo, waliondolewa katika eneo la Malamboi na kupelekwa Vilima Vitatu.

Alisema wanashangazwa na hatua hiyo ya serikali ya kuiomba kuheshimu uamuzi wa Mahakama ya Rufani Tanzania dhidi ya kesi yao ya madai namba 77 ya mwaka 2012, iliyowapa haki ya kuendelea kuishi ndani ya eneo hilo. "Hatua hii ya serikali ya kutupatia barua za kututaka kuondoka eneo hili, inashangaza kwani tunaishi kihalali, hivyo tunaiomba serikali Mkoa wa Manyara kuheshimu uamuzi wa Mahakama ya Rufani," alisema.

Naye Mnyaugi Sosoo, alisema katika eneo hilo ambalo wamepewa amri ya kuondoka, wamekuwa wakiishi na mifugo yao kwa muda mrefu sasa.

Alisema kuwa eneo ambalo wanataka kupelekwa lina ukame wa hali ya juu na halifai mifugo wala binadamu kuishi hapo.

"Kitendo kizima cha kutaka kutuhamisha kinafanywa kibabe sana kwani Ofisa Mtendaji wa Kijiji amekuwa hataki mazungumzo na mtu yeyote yule, huku akitutisha kwamba ni lazima tuhame tu," alisema Gidamshoto Malishi.

Mwenyekiti wa Kijiji hicho, Belela Erasto, aliiomba serikali wilayani Babati kukaa meza moja na wananchi hao ili kutatua mgogoro.

Akizungumza kwa simu, Ofisa Mtendaji wa Kijiji hicho, Shaban, alikiri kuandika na kusambaza barua hizo, ambazo zinatokana na agizo kutoka kwa Mkuu wa Wilaya ya Babati, Elizabeth Kitundu.

Kwa mujibu wa Kitundu, wamiliki wa maboma 31 katika kijiji cha Vilima Vitatu wanatakiwa kuhamia katika kitongoji cha Mfurang'ombe ambacho hakiko mbali na eneo hilo.

Hatua hiyo ya kuandikiwa barua imekuja baada ya familia hizo zilizopewa amri ya kuhama kuchomewa nyumba zao na kulazimika kulala nje mapema mwezi huu.

# Farm Africa yawaunganisha wakulima

**Na Jaliwason Jasson,** MANYARA

SHIRIKA la Farm Africa mkoani Manyara limewaunganisha wakulima na wadau wenye zana bora za kilimo na kuwanoa ili kuwasaidia kutoka kwenye kilimo cha mazoea na kwenda kile cha kibiashara kwa maendeleo yao na taifa. Wakulima hao walikutanishwa juzi katika Kijiji cha Endasak wilayani Hanan'g kwa ajili ya maonyesho ya zana bora za kilimo ambazo zina uwezo mkubwa wa kuwarahisishia kazi ya kulima na wakafaidi matunda ya sekta hiyo.

Mkulima kutoka Kijiji cha Masakta, Lilian Macha, alisema baada ya kuziona zana za kilimo na kufundishwa namna ya kuzitumia, wamezipenda na watazitumia kuboresha kilimo chao na kuinuka kiuchumi.

"Naamini nitatoka katika lindi la umaskini kutokana na vifaa hivyo kuwa bora ambavyo vina ubora zaidi kwa kuwa vinafanya kazi ya kupanda na kuweka mbolea kwa wakati mmoja," alisema.

Macha alisema kabla ya kuipata elimu hiyo, wakulima wengi walikuwa wanatumia zana za kilimo ambazo zinahitaji mtu akienda kupanda awe na watu wengi wa kumsaidia, hivyo kumsababishia gharama kubwa za kupanda na kuvuna.

Kutokana na kuwapo kwa zana hizo za kisasa, alisema kwa sasa anaona kazi itakuwa nyepesi kwa kuwa kwa kiasi kikubwa kazi zilizokuwa zinafanywa na vibarua zitafanywa na mashine za kupandia, kuvunia na kuwekea mbolea.

Aidha, alisema amevutiwa na mashine ya kuchakata chakula cha mifugo hasa kuku, kwa kuwa yeye ni mwathirika wa kupoteza kuku wengi aliokuwa anawafuga na gharama za chakula zilikuwa kubwa na akawa ameshindwa kuzimudu.

"Kwa sasa baada ya kuona na kufundishwa namna ya kutumia mashine ya kuchakata chakula cha mifugo, naenda kufufua mradi wangu wa kuku," alisema.

Mkulima kutoka Kijiji cha Kwaraa, Donatus Bura, alisema amevutiwa na mashine ya kupandia ufuta na ile ya kupulizia dawa, hivyo anakwenda kuzitumia ili kuongeza tija lakini akasema wasiwasi wake uko kwenye zana zingine za kupandia kuwa haelewi zikiharibika atakwenda kuzitengeneza kwenye karakana ipi.

Mwenyekiti wa Chama cha Msingi cha Gallapo, Lohay Langay, alisema iwapo wakulima wataipa nafasi teknolojia, watafanya mapinduzi ya kilimo na kutoka kwenye umaskini. "Miaka 10 iliyopita wakulima walikuwa wanatumia pembejeo duni, lakini kwa sasa wamebadilika kinachotakiwa ni kupewa elimu ya kila mara," alisema.

Langay alisema atakaporudi kwenye maeneo yake atafanya mabadiliko katika shughuli zake ili kuzalisha kwa wingi na kwa ajili ya kilimo cha biashara na atawapatia elimu juu ya zana za kisasa wakulima wenzake ili waokoe gharama za kutumia vibarua wengi na kupoteza muda.

# Hospitali ya Simanjiro sasa karibu kukamilika

**Na Cynthia Mwilolezi,** SIMANJIRO

MKUU wa Wilaya ya Simanjiro mkoani Manyara, Zephania Chaula, amesema hospitali mpya ya wilaya hiyo iko kwenye hatua nzuri baada ya majengo saba kufikia hatua ya kukamilika.

Chaula alisema hayo jana alipokuwa akizungumzia maendeleo ya ujenzi wa hospitali hiyo huku akisema awali wilaya hiyo haikuwa na huduma hiyo na kusababisha wagonjwa wasafirishwe hadi Arusha au Kilimanjaro.

Alisema baada ya kufikia Juni 30, mwaka huu, baadhi ya majengo yalikuwa hayakukamilika na Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Seleman Jafo, aliongeza muda hadi juzi, majengo hayo yawe yamekamilika.

"Nimpongeze Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Simanjiro, Yefred Myenzi, kwa kusimamia ipasavyo mradi huu wa hospitali kwani hivi karibuni itaanza kazi baada ya vifaa tiba na watumishi kuwapo," alisema Chaula.

Pia alimshukuru Rais John Magufuli kwa kutoa Sh. bilioni 1.5 za ujenzi wa hospitali hiyo mpya ya wilaya kwa kuwa awali jamii ya wafugaji na wakulima wa eneo hilo walipata wakati mgumu kupata matibabu wakitoka kwenye zahanati na vituo vya afya.

"Watu wengi walipoteza maisha yao kwani wagonjwa walikuwa wanasafiri zaidi ya kilomita 200 ili kwenda Kilimanjaro au Arusha kufuata hospitali ya rufani ya Mount Meru lakini sasa watakuwa wanahudumiwa hapa," alisema Chaula.

Mbali na hospitali ya wilaya, alisema zahanati saba zinaendelea kujengwa katika vijiji mbalimbali kusogeza karibu huduma za matibabu na afya kwa jamii.

Mkazi wa Kata ya Langai, Solomon John, alisema hospitali hiyo imejengwa kwenye kata yao hivyo jamii ya eneo hilo ijipange kupokea wageni na kuchangamkia fursa mbalimbali.

Alisema wageni wengi watakuwa wanatembelea kwenye eneo hilo pia watumishi wataishi hapo hivyo fursa za biashara nazo zitajitokeza kwa wagonjwa na watakaofika kuwasalimia.

# Waziri ashtukia mchezo mchafu Tanesco

**Na Paul William,** SAME

WAZIRI wa Nishati, Dk. Medard Kalemani, amewaonya watumishi na viongozi wa Shirika la Umeme Tanzania kwa kuwauzia wananchi nguzo kwa bei kubwa kuliko gharama halisi.

Pia amesisitiza kuwa utamaduni ambao umejengwa na watumishi wa shirika hilo kwamba wananchi wanapaswa kulipia nguzo za umeme si sawa na kwamba ununuzi wa nguzo si jukumu la wananchi bali wanatakiwa kupelekewa huduma ya umeme.

Dk. Kalemani alitoa ufafanuzi huo jana wakati wa hafla ya uwashaji wa umeme wa mradi wa Wakala wa Nishati Vijijini (REA) kwa wananchi wa kata za Kalemawe katika Wilaya ya Same na Kigonigoni, wilayani Mwanga.

"Nionye hasa nyie mameneja wa Tanesco, acheni tabia ya kuwarudisha wananchi wanaofika katika ofisi za shirika kulipia gharama za kuunganishiwa umeme mkisingizia kukosekana kwa nguzo. Ununuzi wa nguzo si jukumu la wananchi. Wao wanatakiwa kupelekewa huduma ya umeme," alisema.

Alifafanua kuwa jukumu la ununuzi wa nguzo si la mwananchi bali ni serikali, hivyo wananchi hawapaswi kuelezwa kwamba hawawezi kuunganishiwa umeme kwa sababu hakuna nguzo.

"Gharama za nguzo ni 100,000 na wala si 200,000 wakati gharama za mwananchi anayotakiwa kulipa ili kuunganishiwa umeme ni 25,000 ambayo haiwezi hata kununua nguzo moja. Mkisema hakuna nguzo wananchi walipie, mtawafanya wananchi wakimbie kwa kuhofia gharama.

"Hivyo, sitaki kusikia meneja yeyote awe wa wilaya au mkoa anayemrudisha mwananchi aliyekwenda kulipia huduma ya kuunganishiwa umeme, kisa hakuna nguzo," alisema.

Awali, akiwasilisha taarifa ya utendaji kazi, Meneja wa Tanesco Mkoa wa Kilimanjaro, Mhandisi Mahawa Mkaka, alisema hali ya usambazaji umeme mkoani hapa imeendelea kuimarika kutokana na utekelezaji wa miradi ya kusambaza umeme vijijini na miradi mbalimbali inayotekelezwa na shirika hilo.

Mkaka alisema mpaka sasa vijiji 453 kati ya 519 vimeshapelekewa umeme sawa na asilimia 87.28 na kwamba matarajio ni kufikia vijiji 493 sawa na asilimia 95 ifikapo Desemba, mwaka huu.

Naye Mkuu wa Wilaya ya Same, Rosemary Senyamule, alisema katika Kata ya Kalemawe kulikuwa na uhitaji mkubwa wa umeme hasa katika Zahanati ya Kalemawe ambako kuna wajawazito wanaojifungua nyakati za usiku ambao wamekuwa wakipata adha kubwa kwa kukosa mwanga wa kutosha.

## Wataalamu afya wapigwa msasa

**Na Godfrey Mushi,** SIHA

MRADI wa mwaka mmoja wa kuboresha mpango wa afya ya jamii katika Wilaya ya Siha ambao unafadhiliwa na Chuo cha Tiba cha Morehouse cha Marekani, kupitia Taasisi ya Ubora Tanzania, umeanza kutekelezwa kwa kuwapiga msasa wataalamu wa afya kutoka vijiji 12 vya Kata za Karansi na Makiwaru.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Siha, Valerian Juwal, akifungua mafunzo kwa wataalamu hao, alisema anaamini tija katika maeneo hayo itaonekana katika utoaji wa huduma.

"Napenda kutoa wito kwa wahudumu na wataalamu waliopatiwa mafunzo haya kuhakikisha kuwa wanatumia ujuzi waliopata kwa manufaa ya wananchi waliokusudiwa hususani wanawake, watoto na makundi mengine maalumu katika jamii," alisema.

Mganga Mkuu Wilaya ya Siha, Dk. Andrew Method, akizungumza na wataalamu hao, aliahidi kuendelea kusimamia ufanisi wa mafunzo hayo kwa lengo la kuhakikisha huduma za afya katika wilaya hiyo zinaendelea kuwa bora na zinatolewa bila upendeleo wowote.

Halmashauri ya Wilaya ya Siha ina vijiji 60 ambavyo vitanufaika na mpango huo utakaotekelezwa kwa awamu mbalimbali.

Mafunzo yatafanyika kwa siku nne na yatafikia ukomo leo kwa washiriki 24 kutapatiwa elimu ya uboreshaji wa huduma za afya vijijini.

Chuo hicho na Halmashauri ya Wilaya ya Siha, viliingia mkataba wa kutekeleza mradi huo kuanzia mwaka jana, hadi Desemba 31, mwaka huu.

Miongoni mwa mambo yaliyokubaliwa na chuo hicho pamoja na Shirika la Ubora Tanzania ni kwamba litawapeleka kuwanoa wataalamu wa upasuaji, uboreshaji wa lishe bora kwa jamii na namna ya kuzuia maambukizi ya magonjwa mbalimbali.



Wahandisi kutoka Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini (Tarura) wakiendelea na ujenzi wa daraja la chuma (Mabey Bridge), lililopo Mto Kihansi, Kata ya Chita Melela katika Halmashauri ya Wilaya ya Kilombero, mkoani Morogoro jana. **PICHA: TARURA**

# Wadanganya ustawi kuwa ni yatima

**Na Mwandishi Wetu,** HAI

BAADHI ya watoto yatima wanaochukuliwa na maofisa ustawi wa jamii katika Wilaya ya Hai, mkoani Kilimanjaro na kupelekwa kwenye vituo binafsi vya kulea watoto, wamegundulika kupelekwa humo kimakosa kutokana na kuwa na ndugu na jamaa wenye uwezo wa kuwahudumia.

Ofisa Ustawi wa Jamii wa kituo cha kutunza watoto cha Kao la Amani, Elizabeth Tarmo, amefichua ujanja unaofanywa na baadhi ya watu, kudanganya maofisa ustawi kwamba watoto hao hawana ndugu.

Tarmo alikuwa akizungumza juzi na ujumbe wa viongozi wa tawi la Klabu ya Yanga lililoko katika Mji Mdogo wa Bomang'ombe, Hai ambao walikwenda kukabidhi misaada mbalimbali kwenye kituo hicho cha kulelea watoto yatima.

"Kwa mfano katika kituo hiki, kinalelea watoto yatima wapatao 48 na mwaka jana tulipokea watoto 24 kutoka idara ya ustawi wa jamii, ila baadaye idara hiyo ilifanya utafiti na kugundua kwamba baadhi ya watoto hao wana ndugu na jamaa ambao wana uwezo wa kuwalea, isipokuwa wasichana wawili ambao wamekosa ndugu.

"Mwaka huu, tumepokea watoto sita kutoka idara hiyo na wamebaki wawili baada ya ndugu na jamaa zao kuja kuwachukua ili kwenda kuwalea. Wengi wa watoto hao walikuwa wametoroka nyumbani kutokana na mazingira magumu ikiwamo unyanyasaji wa kinjisia," alisema.

Kabla ya makabidhiano hayo ya misaada ya kibinadamu kama mchele, sabuni na daftari vinavyofikia gharama ya Sh. 400,000, mwenyekiti wa tawi hilo, Samweli Gataya, alisema nafsi zao zimesukumwa kutoa msaada huo ili kuendelea kuikumbusha jamii kuwa bado ina wajibu wa kusaidia watu wenye mahitaji, hasa yatima na wanaoishi katika mazingira magumu. "Iko haja kwa wananchi wenzetu hasa wenye uwezo kiuchumi, mashirika ya kiraia na taasisi za umma, kujitokeza kuwasaidia watoto yatima na wale wanaoishi katika mazingira magumu ili kupunguza changamoto zinazowakabili kwa sasa," alisisitiza Gataya.

Aidha, alisema pia tawi hilo limetembelea Hospitali ya Wilaya ya Hai kuona wagonjwa na kutoa zawadi mbalimbali kama njia mojawapo ya kutafuta heri, mbali na masuala ya burudani.

AFYA NA MAZINGIRA

ALHAMISI AGOSTI 1, 2019



Ukurasa 18

**Wajawazito wenye kisukari hatarini kujifungua njiti**



Ukurasa 17

Watafiti: Ongezeko hili la joto halijapata kutokea



Ukurasa 14

**Rekodi dunia miti mipya milioni 350 siku moja**



# Daktari afunguka hatari ya afya kukimbizia mtoto kituo cha malezi

Ukurasa 19

## Rekodi dunia miti mipya mil.350 siku moja

**Addis Ababa,** ETHIOPIA

ETHIOPIA imejigamba kuweka rekodi ya dunia kupanda miti mingi zaidi, kwa kuweka ardhini miche milioni 350 ndani ya siku moja.

Ni mradi unaosimamiwa moja kwa moja na Waziri Mkuu, Abiy Ahmed, katika vita ya kukabili uteketezaji miti, unaoendana na athari ya hali ya hewa na kukaribisha ukame.

Kutokana kasi hiyo, kuna baadhi ya ofisi zilifungwa kutoa fursa kwa watumishi wa umma ya kufanikisha mradi huo, Waziri Mkuu Abiy, aliendesha kampeni katika maeneo 1,000 nchi nzima.

Ni hatua inayochukuliwa kukiwapo ripoti ya Umoja wa Mataifa, inayosema misitu ya nchi hiyo imepungua kutoka asilimia 35 katika karne iliyopita, hadi asilimia nne tu katika kipindi kilichopo.

Waziri wa nchi hiyo anayeshughulikia Ubunifu na Tenkolojia, Getahun Mekuria, aliripoti kupitia ukurasa wake wa mtandao wa kijamii, kwamba kiwango hicho kimepandwa ndani ya saa 12 za kampeni, lengo kufikia miti bilioni moja.

Ni kampeni iliyowashirikisha hata watumishi wa Umoja wa Mataifa jijini hapa, pia asasi za kimataifa.



Mtoto akipanda mti nchini Ethiopia. **PICHA: MTANDAO.**

AFYA

# Kilio kisichoisha wazee wanaodai kunyimwa haki ya kutibiwa

## • Shinyanga Vijijini: Vitambulisho kwetu 'donda ndugu'



Mtaalamu wa taasisi ya TPRI akitoa elimu kwa washiriki kuhusu vifungashio vya viuatilfu na athari zake kwa wakulima. **PICHA ZOTE: MARY MOSHA**

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

SERA ya Wazee ya Mwaka 2003 inatamka kwamba wazee wote wenye umri kuanzia miaka 60 na kuendelea, wanahitajika kupewa huduma za bure za matibabu katika vituo vyote vya afya, kuanzia zahanati, vituo vya afya na hosptali.

Licha ya kuwapo sera hiyo ya wazee, kuna madai kwamba bado hali hairidhishi na hawana sheria maalum yua kuwasimamia.

Kuna kilio cha hali mbaya katika huduma za matibabu kutoka maeneo mbalimbali nchini, ikiwamo Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga Vijijini.

Hiyo inatokana na wastani wa miaka 16 sasa imepita, kuwapo kusuasua kutekelezwa kwa changamoto zao. Sasa wamekuja na madai kwamba, itungwe sheria ya wazee itakayoboreshwa kusimamia haki zao za kisheria.

Wazee wa Shinyanga Vijijini, kama ilivyo kwa baadhi ya wenzao katoka maeneo mengine wanaokabiliwa na changamoto za ukosefu wa matibabu bure, sababu kuu ni kwamba hawana vitambulisho maalum vya kutumia .

> "Pia ataanza kujipanga na utoaji kadi za Bima ya Afya ya Jamii (CHF) iliyoboreshwa ili kuwarahisishia upatikanaji wa matibabu.



Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga Vijijini, Hoja Mahimba, akitoa ufafanuzi wa mkakati wake kwa wazee. **PICHA: MARCO MADUHU.**

Pia, ndani ya halmashauri hiyo, kunaelezwa hakuna madirisha maalum ya kuhudumia wazee, madaktari bingwa wa kuwatibu, pia uhaba wa dawa hasa zinazohusu magonjwa yao.

**VIONGOZI WAZEE**

Katibu wa Baraza la Wazee wa Shinyanga Vijijini, Boniface Boazi, anasema wapo jumla ya wazee 12,922, kati yao wanaume 6,173 na wanawake 6,749.

Katika orodha, lakini wenye vitambulisho vya matibabu bure ni 5,563 na waliosalia 7,359 hawana vitambulisho hivyo, hali ambayo imekuwa ikiwapatia ugumu wa matibabu.

Anasema licha ya kuwapo na uchache wa vitambulisho hivyo, lakini wanapokuwa wakifika kupatiwa matibabu bure kwenye zahanati na vituo vya afya, inapofikia wakati wa kupewa madawa huambiwa hakuna dawa, bali wakanunue kwenye maduka ya dawa ya watu binafsi na kuambulia kupewa dawa za maumivu tu.

"Sisi wazee ndio hazina ya taifa hili tumepigania uhuru wananchi, lakini tunasikitika kuendelea kukabiliwa changamoto ya ukosefu wa matibabu bora, licha ya viongozi wa serikali kutoa matamko ya wazee kupewa kipaumbele kwenye huduma za afya, lakini inapofikia hatua ya kupewa dawa tunaambiwa hazipo,"anasema Boazi.

"Ukiangalia sisi wazee tunakabiliwa na changamoto ya kipato. Sasa unapotuambia tukanunue madawa yanayohusu magonjwa ya wazee kwenye maduka ya dawa ya watu binafsi, hapo unakuwa hujatutatulia tatizo, bali ni kutupaka mafuta kwa mgogo wa chupa," anaongeza.

Edward Lupimo, ni Mwenyekiti wa Baraza la Wazee wa Wilaya ya Shinyanga Vijijni, anasema changamoto zote zinazowakabili na kushindwa kutatuliwa, zinatokana na ukosefu wa sheria ya wazee, hivyo wanashindwa kutekelezewa mambo yao kwa mujibu wa sheria.

"Sisi Baraza la Wazee Wilaya ya Shinyanga Vijijini, kwanza tunampongeza Rais John Magufuli, kwa kutuingiza wazee kwenye Wizara ya Afya ya Maendeleo ya Jamii,

AFYA

# Kilio kisichoisha wazee wanaodai kunyimwa haki ya kutibiwa

Jinsia, Wazee na Watoto. Ameonyesha nia ya kutusaidia matatizo yetu, hasa kwenye masuala ya matibabu.

"Kutokana na Rais Magufuli kuonyesha nia ya kutusaidia sisi wazee, sasa tunamuomba atoe msukumo wa kutungiwa Sheria ya Wazee, ambayo ndiyo itakuwa kinga kwetu sisi katika kutatuliwa matizo yetu kwa mujibu wa sheria, na siyo kwa sasa ambapo tunaishi kwa sera tu ambayo haina nguvu," anaongeza.

Lupimo anataja magonjwa yanayowakabili wazee kuwa ni: Tezi dume, moyo, macho, kisukari, figo, kibofu cha mkojo, miguu, kupoteza kumbukumbu na magonjwa nyemelezi yanatokana na umri wao kuwa mkubwa.

**USTAWI JAMII**

Ofisa Ustawi wa Jamii wa Halmashauri hiyo, Agnes Ginethon, anasema kutokana na wazee kukabiliwa na changamoto hiyo ya ukosefu matibabu bure, halmashauri imeshatenga Sh. 4,750,000 kwa ajili ya kuwapatia vitambulisho vya matibabu kwa wazee 7,359 waliosalia.

"Changamoto ambayo imekuwa ikitukabili kugawa vitambulisho vya matibabu bure kwa wazee, inatokana na uhaba wa fedha. Mikakati iliyopo ni kuendelea kutenga fedha kupitia mapato ya ndani, ili kuweza kutatua matatizo hayo ya wazee,"anasema Ginethon.

**MGANGA MKUU**

Mganga Mkuu wa Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga vijijini, Amosi Mwenda, anatoa ufafanuzi wa dai la uhaba wa dawa, kwamba kuna baadhi ya dawa haziruhusiwi kuwapo kwenye zahanati na vituo vya afya.

Anasema, ni sababu inayochangia hoja za wazee wanapoambiwa ama wakanunue dawa au waende hospitali za wilaya ambako zinapatikana, wanalalamika katika mtazamo 'dawa hakuna.'

"Halmashauri yetu tuna dawa asilimia 96, lakini kuna baadhi ya dawa haziruhusiwi kuwepo kwenye zahanati na vituo vya afya, kwa sababu hakuna wataalamu wa kutoa huduma hizo, ikiwa tunakabiliwa na upungufu wa watumishi asilimia 68," anasema.

Dk Mwenda anaongeza:"Hiyo ndiyo maana wazee huambiwa wakanunue dawa zao au waende kwenye hospitali kubwa za serikali....izingatiwa na kuwepo na umbali mrefu wa kufuata dawa kwenye hospitali za wilaya na mkoa, ndipo hukata tamaa na kuamua kutafuta mbadala mwingine wa matibabu."

Pia, anatoa ufafanuzi la kutokuwapo madirisha ya wazee, kunatokana na uhaba wa watumishi wakiwamo madaktari bingwa wa magonjwa ya wazee.

Dk, Mwenda anafafanua kwamba kinachofanyika sasa ni kuan-



Mwenyekiti wa Baraza la Wazee Wilaya ya Shinyanga Vijijini, Edward Lupimo, akizungumzia kilio chao.

> **"Ni sababu inayochangia hoja za wazee wanapoambiwa ama wakanunue dawa au waende hospitali za wilaya ambako zinapatikana, wanalalamika katika mtazamo 'dawa hakuna.'**



Katibu wa Baraza la Wazee Wilaya ya Shinyanga Vijijni, Boniface Boazi, akitoa hoja kuhusu ukosefu wa vitambulisho vyao.



Mganga Mkuu wa Wilaya ya Shinyanga Vijijini, Amosi Mwenda, akitoa ufafanuzi wa malalamiko yanayowahusu wazee kupatiwa kipaumbele cha matibabu.

dikwa vibao vya 'mzee apewe kipaumbele kwanza kwenye huduma za matibabu.'

Kwa mujibu wa malengo ya Mkakakti wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umasikini Tanzania (Mkukuta), unaelekeza kuwapo huduma za afya kwa umbali usiozidi kilomita tano, ili kutoa fursa ya upatikanaji huduma za afya kirahisi, hususan kwa wazee.

Hilo linaelelezwa bado halijafanikishwa katika maeneo meng na wazee wanashindwa kupata huduma bora za kiafya.

**DED ATAMKA**

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga Vijijini, Hoja Mahimba, anaahidi kuzifanyia kazi changamoto zinazowakabili wazee kwa hatua na hadi sasa tayari ameshaanza kutenga fedha kwa ajili ya kuwapatia vitambulisho vya matibabu bure.

Anasema, pia ataanza kujipanga na utoaji kadi za Bima ya Afya ya Jamii (CHF) iliyoboreshwa ili kuwarahisishia upatikanaji wa matibabu.

"Natambua umuhimu wa wazee katika taifa hili hivyo pale nitakapokuwa na uwezo napo, lazima niwatatulie changamoto zenu kupitia utengaji bajeti kwenye mapato ya ndani ya halmashauri, ili muweze kufaidi matunda ya nchi hii ambayo mlipigania," anasema.

"Kuhusu suala la utungwaji sheria yenu (Sheria ya Wazee), hilo ondoeni shaka. Rais wetu msikivu John Magufuli atalifanyia kazi na imani hawezi kuondoka madarakani. Atakuwa tayari ameshasukuma msukumo wa kutungiwa sheria na ndio maana ameanza kuwaingiza kwanza kwenye Wizara ya Afya,"anaongeza.

**OFISA MIRADI**

Winnie Hinaya, ni Ofisa Mradi kutoka shirika binafsi la Tawlae, linalotetea haki za wazee mkoani Shinyanga. Anataja baadhi ya majukumu ya mradi wao wa kutetea haki za wazee, ni kupigania wazee kuingizwa kwenye mipango yao halmashauri ya utengaji wa bajeti, ili wapate kutatuliwa changamoto zao, hasa matibabu bure.

Anasisitiza haja ya kutolewa msukumo, kwani wazee wamekuwa wakisahaulika kutekelezewa mahitaji yao, kutokana na kuishi kwa sera, badala ya kuwa na sheria masusi inayowasimamia, kuwaondolea changamoto zinazowakabili.

Mtazamo wa dai hilo la kisheria, ni kuwapo matibabu ya bure, upatikanaji wa dawa za magonjwa yanayowakabili, yote kswa jumla inawaodolea wazee adha.

AFYA

# Safari ya kuutokomeza Ukimwi kuitafuta lengo 'sifuri tatu'




Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, akizungumza kwenye Maadhimisho ya Miaka 15 tangu Kuanzishwa Mfuko wa Dharura wa Rais wa Marekani wa Kupambana na Kudhibiti Maambukizi ya Virusi vya Ukimwi (PEPFAR), kwenye Kituo cha Mikutano cha Kimataifa cha Julius Nyerere jijini Dar es Salaam, Mei 3 mwaka jana. **PICHA ZOTE: MTANDAO**

**Na Sabato Kasika**

NI kweli inafahamika kwa wengi. Huo ni ugonjwa unaopounguza kinga mwilini. Hiyo ndiyo sifa na madhara yake makuu.

Akizungumza mwaka jana, alipozindua mkakati wa maadhimisho ya miaka 15 ya kuanzishwa kwa Mfuko wa Dharura wa Rais wa Marekani wa Kupambana na Kudhibiti Maambukizi ya Virusi vya Ukimwi (PEF).

Katika marejeo ya taarifa za mwaka 2016 hadi 2017, maambukizi ya virusi vya ugonjwa huo nchini bado ni makubwa, katika ngazi ya kaya kwa mwaka.

Anataja takriban watu milioni 1.4 wanakadiriwa kuishi na virusi vya Ukimwi nchini, huku wengine 81,000 wakipata maambukizi mapya kila mwaka.

Waathirika wakubwa wa janga hilo, wanatajwa kuwa ni wasichana, huku baadhi ya mikoa ikitajwa kuongoza kwa kiwango cha maambukizi juu ya wastani wa kitaifa wa asilimia 4.7.

Mikoa aliyotaja na viwango vyake katika mabano, kwa mujibu wa miaka hiyo 2016/17 ni: Njombe (11.4%); Iringa (11.3%); Mbeya (9.3%); Mwanza(7.2%); Kagera (6.5%); Katavi na Shinyanga zote (5.9%); na Dodoma (5.0%).

Katika kupambana na ugonjwa huo, Desemba mwaka jana, serikali ilizindua Mkakati wa Nne wa Taifa wa Kudhibiti Ukimwi 2018/19 hadi 2022/23, unaotarajia kupunguza maambukizi mapya ya VVU kwa

> **Mtanzania hana budi kushiriki kikamilifu kutokomeza Ukimwi kuwa na ngazi 'sifuri' kwenye maambukizi mapya, vifo na ukomeshaji unyanyapaa'.**



Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu Sera, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na Watu wenye Ulemavu, Anthony Mavunde (mwenye miwani), akiongoza matembezi ya kilometa tano zilizofanyika katika viwanja vya The Green Kenyatta Drive, Oysterbay, jijini Dar es Salaam, Novemba 25, 2017, kuchangia udhamini wa UKIMWI. Mwenye kofia nyeupe ni Mkurugenzi Mtendaji wa Tacaids, Dk Leonard Maboko na kulia kwake, Mwenyekiti wa Serikali za Mtaa wa Oysterbay, Zefrin Lubuva.

asilimia 75 ifikapo mwaka 2020 na asilimia 85 ifikapo mwaka 2023.

Matokeo mengine yanayotarajiwa kufikiwa kutokana na mkakati huo, ni kupungua maambukizi mapya ya VVU kwa watoto chini ya asilimia tano, ifikapo mwaka 2023.

Katika uzinduzi aliyoufanya Majaliwa mwaka jana, unaoanisha na kupanga programu mbalimbali zinazosaidia mwitikio wa taifa, zikiwamo hatua zinazotekelezwa kupitia Mpango wa Dharura wa Rais wa Marekani wa Ukimwi (PEPFAR).

### ANACHOSISITIZA MAJALIWA

Kinachosisitizwa na Waziri Mkuu, ni kuimarisha mawasiliano na uratibu miongoni kwa wadau wote, sambamba na kufuata na kutekeleza vipaumbele vilivyoainishwa, ili kufanikisha mkakati huo.

Anasema matayarisho ya mkakati huo yamezingatia matokeo ya mapitio ya Mkakati wa Tatu wa Taifa wa Kudhibiti Ukimwi 2013/14 hadi 2017/18, lengo linakuwa kupunguza kasi ya vifo nchini vinavyotokana na Ukimwi.

Mtazamo ni kupunguza kwa wastani wa asilimia 50 ifikapo mwaka 2020 na asilimia 70 ifikapo mwaka 2023.

Pia, katika sura ya kukabili kunalengwa kukabiliana na unyanyapaa, pia ubaguzi wa rangi ifikapo mwaka 2023, kuelekea ngazi ya kutokomeza kabisa maradhi ifikapo mwaka 2030.

Waziri Mkuu anawahimiza viongozi katika ngazi mbalimbali, waungane katika kuhamasisha jambo hilo, kwa vile vita dhidi ya VVU na Ukimwi inahitaji dhamira ya dhati na tafakuri ya kina kujilinda dhidi ya maambukizi mapya.

"Serikali ya Awamu ya Tano itaendelea kutekeleza na kuboresha huduma za upimaji wa virusi vya Ukimwi, kuzuia maambukizi ya kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto, matibabu ya magonjwa nyemelezi na kupiga vita unyanyapaa wa aina zote kwa wenye Ukimwi," anasema Majaliwa.

### UKIMWI KWA VIJANA

Takwimu zilizotolewa Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Watu Wenye Ulemavu, Anthony Mavunde, Desemba mwaka jana zinaonyesha kuwa wasichana wenye umri kati ya miaka 15 hadi 24 hapa nchini, huambukizwa virusi vya Ukimwi (VVU) kila siku.

Mavunde alitoa takwimu hizo Desemba mwaka jana katika kilele cha shughuli za vijana kuelekea kwenye Maadhimisho ya Siku ya Ukimwi Duniani na anasema, hao ni miongoni mwa vijana 90 wenye umri wanaopata maambukizi mapya kila siku moja.

Anafafanua kuwa takwimu hizo zilitokana na utafiti wa viashiria vya Ukimwi wa mwaka 2016/2017, zinaonyesha kuwa vijana hao 90 wanapatikana kutika kundi la vijana 225 wanaoambukizwa Ukimwi, kila siku nchini.

Kwa mujibu wa naibu waziri huyo, ni kwamba takwimu hizo zinaahirisha kuwa iwapo jamii haitachukua hatua za kukabiliana na hali hiyo haraka iwezekanavyo, maambukizi yataendelea kuongezeka kila mwaka.

"Hali hiyo inaweza kurudisha nyuma juhudi za serikali za kutaka ifikapo mwaka 2030 kusiwe na maambukizi mapya ya VVU. Pia, kuwapo kwa takwimu hizo ni changamoto kwa malengo ya 2030," anasema Mavunde.

### KUELEKEA 'SIFURI TATU'

Mwaka 2010 hadi 2018, serikali ilikuja na mkakati iliyouita 'sifuri tatu' ililenga kukabiliana na Ukimwi, ili kupunguza kiwango cha vifo vitokanavyo na Ukimwi, kuzuia maambukizi mapya ya VVU na kukomesha unyanyapaa.

Aliyekuwa Mkurugenzi wa Sera, Mipango na Utafiti wa Tume ya Taifa ya Kudhibiti Ukimwi (Tacaids) 10 wakati huo, Dk. Raphael Kalinga, alitaja tohara inachangia kunusuru maambukizi ya virusi vya Ukimwi, kati ya asilimia 60 hadi 80.

Hivyo katika dhana ya sifuri tatu kwa upande wa kupunguza vifo vitokanavyo na Ukimwi iliendeshwa tohara nchini na pia kuhakikisha wenye VVU wanapatiwa matibabu ya dawa za kupunguza makali ya Ukimwi (ARV).

Aliweka wazi kuwa mbinu za kupunguza vifo vitokanavyo na Ukimwi zinafanana kwa kiasi kikubwa na upunguzaji maambukizi mapya ya Ukimwi.

Ni mbinu inayotajwa kujumuisha utoaji dawa za kufubaza virusi vya Ukimwi katika vituo vya afya vilivyopo nchini, hasa kwa wanaolazimika kufanyiwa hivyo, kwa vile siyo kila mwenye virusi anatakiwa kunywa dawa.

Kwa mujibu wa Dk. Kalinga, kilichokusudiwa ni asilimia 80 ya wenye virusi waandikishwe katika matunzo na matibabu, kisha vituo vyote vya afya viwe na vinatoa huduma za matunzo na tiba (CTC) kupunguza vifo vitokanavyo na Ukimwi.

Kuhusu unayanyapaa, Tacaids inasisistiza kwamba una madhara mengi, waathirika kukosa huduma zote hasa za Ukimwi, ambazo ni tiba na nyingine zinazosababisha waendelee kuambukizana na kupoteza maisha.

Akibainisha kuhusu sera ya afya, anasisitiza kwamba haiwatengi, bali watu ndio wamekuwa wakijinyanyapaa.

Dk. Kalinga anasema, mzizi wa unyanyapaa uko katika namna jamii ilivyopokea ugonjwa huo, katika mtazamo kwamba Ukimwi unasababishwa na ngono tu, jambo linalowafanya baadhi ya walioathirika kuwa na mwonekano wa kuwa wakosefu.

Mtaalamu huyo anasema, wakati mkakati wa kukabili unyanyapaa ulianza kwa kiwango cha asilimia 40, mtazamo ulilenga kupunguza kufikia asilimia 10 na kuifuta kabisa hali hiyo.

### UKIMWI UMESHINDIKANA?

Sasa ni zaidi ya miaka 30 tangu ugonjwa huo kuwapo nchini, serikali imekuwa ikijitahidi kukinga na kutoa tiba kwa watu wenye Ukimwi kwa ajili ya kunusuru uhai wa Watanzania.

Juhudi hizo za serikali pamoja wadau mbalimbali zinakwenda sambamba na utoaji wa elimu inayohusu madhara ya Ukimwi, kinga dhidi ya virusi vya Ukimwi na tiba kwa wenye maambukizi ya ugonjwa huo.

Kama ambavyo Waziri Mkuu anasisitiza kwamba viongozi katika ngazi mbalimbali waungane kuhamasisha vita dhidi ya VVU na Ukimwi, ni muhimu kila Mtanzania kushiriki kikamilifu.

Ni kweli kwamba vita hiyo inahitaji dhamira ya dhati na tafakuri ya kina katika kujilinda dhidi ya maambukizi mapya ya Ukimwi ili kuhakikisha maambukizi yanapungua na hatimaye kumalizika.

> **Kama ilivyo kwa (virusi) Ukimwi, virusi vya homa ya ini pia huambukizwa kwa njia ya kujamiiana, mate, jasho na mwingiliano wowote ule wa damu.**

Waziri Mkuu anaweka wazi kuwa serikali ya Awamu ya Tano itaendelea kutekeleza na kuboresha huduma za upimaji wa virusi vya Ukimwi, kuzuia maambukizi ya kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto.

Mbali na hayo anasema matibabu ya magonjwa nyemelezi na kupiga vita unyanyapaa wa aina zote kwa wenye Ukimwi ni mambo muhimu, hivyo hatua hiyo ni ya kuunga mkono ili kuokoa vijana ambao ni nguvukazi ya taifa.

Takwimu zilizotolewa na Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Watu Wenye Ulemavu, Anthony Mavunde, ni kwamba wasichana wenye umri kati ya miaka 15 hadi 24 nchini, huambukizwa Ukimwi kila siku.

Kwamba hao ni miongoni mwa vijana 90 wenye umri huo wanaopata maambukizi mapya kwa siku moja, kwa hiyo ili kunusuru kizazi hiki kila Mtanzania hana budi kushiriki kikamilifu kutokomeza Ukimwi kuwa na ngazi 'sifuri' kwenye: maambukizi mapya, vifo na ukomeshaji unyanyapaa.

## Watafiti: Ongezeko hili la joto halijapata kutokea



Hali halisi ya uharibifu wa mazingira. **PICHA: MTANDAO.**

HIVI sasa duniani kuna malalamiko makubwa kuhusiana na kasi kubwa ya ongezeko la joto duniani, huku katika sura ya pili kukiwapo hatua kubwa inayoendelea kuchukuliwa na mazingira, kudhibiti hali hiyo.

Watafiti wa kimataifa wanasema kiwango kilichofikiwa kimeweka rekodi katika miaka 2000 iliyopita na wanaongeza kwamba kiwango vigezo vinavyotumika sasa vimepitwa na wakati.

Wanatoa mfano katika zama za 250 AD hadi 400 AD, hakukuwapo ongezeko la joto lisilo la kawaida barani Ulaya, lakini baada ya karne nyingi hadi kufikia zama za miaka 1300, joto hilo lilipungua sana.

Kwa kurejea mfano huo, wanautumia kama marejeo ya kupanda na kushuka kwa joto la duniani. Mapinduzi ya viwanda duniani yaliyofanyika kwa mara ya kwanza duniani, yanaelezwa kuwa na mchango mkubwa katika mabadiliko ya hali hewa.

Pia, kuna malalamiko kwamba hakuna hatua kubwa iliyofanyika kukabili madhila hayo ya kimazingira na watafifi wanavieleza vigezo vilivyokuwapo katika miaka 2000 iliyopita, kwamba ni batili

"Tumepata joto kubwa zaidi lililowahi kutokea katika millenia mbili zilizotokea katika kipindi cha karne ya 20, ikigusa asilimia 98 ya dunia," ilitangaza taarifa moja ya kiserikali.

Watafiti katika maono yao ya usomi wa sayansi ya mazingira, ni kwamba chanzo kikuu cha mageuzi hayo ya hali ya hewa kinaguswa na volkano.

Mtafiti Dk. Raphael Neukom, kutoka Chuo Kikuu cha Bern, nchini Uswisi inapingana na hoja zinazoelekeza chanzo katika kuwapo jua kali duniani, hata mwanadamu nafasi yake ni ndogo zaidi, mzizi mkuu ukibakia katika volkano.

Watafiti hao bado wanatoa angalizo kwamba, hawajachukulia kilichogunduliwa ni tamko rasmi, ila takwimu zinawapa ushahidi mkubwa kusimamia nafasi hiyo

"Wamefanya haya (ukusanyaji takwimu) zaidi ya mara 700 katika kipindi cha miaka 2,000 years," anatamka Profesa Daniela Schmidt, kutoka Chuo Kikuu cha Bristol nchini Uingereza

Anaendelea kwa kuwasifu kwamba watafiti hao wamekuwa makini sana katika kutathmini takwimu na vigezo husika, hali inayofanya kiwango cha ubora wa klazoi zao kuwa katika ngazi ya juu zaidi.

Mtazamo unaotolewa na wataalamu wengi wa hali ya hewa hivi sasa ni kwamba, miongozo inayorejewa katika mifumo iliyopo katika mifumko ya hali ya hewa, imekuwa ikipotosha katika miongo mingi iliyopitiwa.

"Waraka huu mwishowe utawasimamisha wanaopinga mabadiliko ya hali ya hewa, wanaodai kwamba mabadiliko ya hali ya hewa duniani ni sehemu ya mabadiliko ya asili ya hali ya hewa," anasema Profesa Mark Maslin, kutoka Chuo Kikuu cha London, Uingereza, ambaye hata hivyo hakushiriki utafiti unaojadiliwa.

Anaongeza:"waraka huu unaonyesha tofauti kati ya mabadiliko ya hali ya hewa kwa ukanda na maeneo yanayohusika.

**• Ni mijadala iliyochapishwa katika majarida ya kitaaluma ya sayansi na mazingira.**

AFYA

UGUNDUZI USIOTARAJIWA...

# Wajawazito wanaoumwa kisukari hatarini kujifungua 'vichanga'njiti

• Wa kiume waongoza kwa idadi • 'Mabonge' nao wakae chonjo



Madaktari wakiwahudumia watoto njiti wodini. **PICHA: MTANDAO**

WANAWAKE wenye ugonjwa wa kisukari wanaelezwa kuwa jirani na uwezekano mara nne wa kujifungua watoto njiti, kulinganisha na wenzao wasio na maradhi hayo.

Kitaalamu, uzao wa namna hiyo unaelezwa kwamba unakaribisha hatari ya watoto hao kushindwa kuishi muda mrefu zaidi, kuliganishna walio mbali na hatari hiyo tajwa.

Watafiti kutoka Chuo Kikuu cha Glasgow, nchini Scotland, walitathmini rekodi za karibu za wanawake 4,000 wa Uskochi wenye ugonjwa wa kisukari na kubaini kuwa viwango vya juu vya sukari mwilini miongoni mwa wanawake wajawazito wenye maradhi ya kisukari iliwaweka hatarini kupata watoto njiti.

Kiwango cha unene wa mwili (BMI) cha mwanamke mwenye ugonjwa wa kisukari, pia ni kigezo kikubwa cha utafiti husika.

**KUJIFUNGUA MAPEMA**

Dk. Sharon Mackin, aliyefanya utafiti huo anasema:"Ni muhimu kwamba sisi kama wataalamu wa

> **Viwango vya kabla ya ujauzito vikiwa muhimu sana katika ubashiri wa uzazi wa watoto njiti miongoni mwa waliokuwa na aina ya pili ya ugonjwa wa kisukari.**

huduma ya afya, tutafute njia bora za kuwasaidia wanawake wakati wanapokuwa na umri wa kupata ujauzito kudhibiti uzito wao na viwango vya sukari mwilini."

Anasema, hiyo inawasaidia wajawazito hao kupanga uzazi wao, hali inayopunguza hatari za matokeo mabaya.

"Ni muhimu kwa wanawake wenye kisukari wawe watu wenye kujali hili na wawe na uwezo wa kupata ushauri nasaha wa awali kabla ya kupata ujauzito, hata kama ikiwezekana wapange ujauzito.

"Wanawake wenye ugonjwa wa kisukari, pia wanapaswa kuwasiliana na kliniki zao za kisukari mapema iwezekanavyo mara wanapotambua kuwa ni wajawazito, ili tuweze kuwaona na kuwasaidia mapema," anaeleza

Unatajwa kuwa ugunduzi usiotarajiwa, kwani mtazamo wa awali ulionyesha kwamba watoto njiti walikuwa wa kiume zaidi kuliko wa kike, katika kundi la kinamama wenye aina mbili za kisukari tajwa

Utafiti umebaini kwamba kujifungua mapema kunaweza kuangaliwa kama chaguo linalowa-



Mama mjamzito.

vutia wengi, lakini bado utafiti zaidi unahitajika kabla ya kuliidhinisha hilo kuhusu upangaji umri wa kujifungua.

Dk. Mackin anahoji:"Swali linapaswa kuwa ni ikiwa kujifungua mapema kwa wanawake wote wajawazito wenye ugonjwa wa kisukari kunaweza kuwazuia kujifungua watoto njiti ".

Anaongeza:"Hatufahamu jibu kuhusu hili. Muda sahihi wa kujifungua wa ujauzito wa aina hiyo haujulikani."

Utafiti ulibaini kuwa watoto wachanga 5,392 walizaliwa kutoka kwa kinamama 3,847 wenye kisukari wa Uskochi, mnamo Aprili 1998 hadi Juni 2016.

Kinamama wenye aina ya kwanza ya kisukari walikuwa na uwezekano mara tatu wa kupata watoto njiti, huku wenye aina ya pili, walikuwa na uwezekano wa kuwapata watoto mara nne.

Viwango ya njiti waliozaliwa ni wastani wa watoto 16.1 (1.61%) kutoka wazazi 1,000. Hao ni kinamama wenye aina ya kwanza ya kisukari.

Pia, kwa wenye aina ya pili ya kisukari, kuna wastani wa watoto 22.9 kutoka kundi la kinamama 1,000, ikiwa wastani wa asilimia 2.29.

Kutoka kwenye ulinganishi huo unaunda wastani wa jumla kwa wanawake wote wenye kisukari kwamba, kutoka kwenye kundi la wanawake 1000 kunakuwapo watoto 4.9 wanaojifungua watoto njiti au sawa na asilimia 0.49

"Wanawake wenye aina ya kwanza ya ugonjwa wa kisukari waliokuwa na uzazi wa watoto njiti walikuwa na kiwango cha juu ya wastani wa sukari katika damu yao kwa kipindi chote cha ujauzito wao," anasema.

Anaongeza:'Viwango vya kabla ya ujauzito vikiwa muhimu sana katika ubashiri wa uzazi wa watoto njiti miongoni mwa waliokuwa na aina ya pili ya ugonjwa wa kisukari.'

Pia, utafiti huo uliochapishwa na jarida maalumu la kisayansi kuhusu ugonjwa wa kisukari (Diabetologia Journal), unaeleza kuwa watoto wachanga wenye uzito wa juu au chini, walikuwa hatarini zaidi.

Dk. Emily Burns, Mkuu wa Mawasiliano na Utafiti wa Kituo cha Utafiti wa Ugonjwa wa Kisukari nchini Uingereza (Diabetes UK), anaeleza: "Wanawake wengi wenye ugonjwa wa kisukari wana ujauzito wenye afya na watoto wachanga wenye afya.

"Lakini, utafiti huu unahimiza umuhimu wa kuwasaidia wanawake kudhibiti viwango vyao vya sukari katika damu zao, pale wanapopanga kupata ujauzito, ili kupunguza hatari ya matatizo kadri wawezavyo.

"Utafiti pia umeonyesha kuwa kupunguza uzito wa ziada kwa wanawake wenye aina ya pili ya ugonjwa wa kisukari ambao wana uzito wa mwili kupita kiasi, wanaweza kusaidia kupunguza hatari." **BBC**

AFYA

# Daktari afunguka hatari ya afya kukimbizia mtoto kituo cha malezi

Jaliwason Jasson, BABATI

- Tabasamu, mkono, kauli ya mzazi lulu
- Ustawi wa jamii, wazazi wafunguka yao



Watoto wa kituo cha kulea watoto cha Yeyo Care Centre, mjini Babati, wakicheza na mwalimu wao. **PICHA ZOTE: JALIWASON JASSON**

KUNA mjadala kuhusu kuwapo vituo vya kulelea watoto kutwa maarufu kama 'Day Care Centre. Kuna mitazamo, kwamnba wanaohisi wazazi na walezi anakosea kuwapeleka katika vituo hivyo na wengine wanaunga mkono, kuwa msaada kutokana na majukumu yao.

'Day care Centre'ni vituo vinvyoanzishwa ama na watu binafsi au taasisi, kuwapokea na kuwalea watoto wadogo, wakati wazazi wao wana majukumu mengine ya kimaisha na wanawafuata jioni.

**AONAVYO DAKTARI**

Daktari Anna Akaro, kutoka Kitengo cha Watoto, Hospitali ya Rufani Mkoa wa Manyara, anaiambia Nipashe kuwa mazingira ya mtoto kujifunza si lazima apelekwe kwenye vituo vya malezi, bali wazazi wenyewe wanaweza kuwaandalia mazingira rafiki ya kucheza.

Anamuelezea mtoto tangu anazaliwa hadi umri wa miezi mitatu, anapotarajiwa shingo yake imekaa vizuri na baada ya hapo kufika miezi sita, anatarajiwa kiafya atakuwa amefungua macho, awe anacheza na vitu vya rangi na awe anamudu kukaa.

Kwanini mtoto anapenda kucheza na vitu vya rangi?

Dk. Akaro anafafanua kuwa, ni hulka ya asili mtoto anapenda kucheza na vitu vya rangi, kwa kuwa lenzi yake inakuwa inaboreshwa na ndio anaviona zaidi.

Hivyo anasema, wazazi au walezi wanaowapeleka watoto kwenye vituo vy malezi, maana yake ni kwamba watoto wao wanaweza kukosa fursa za kuziona hizo rangi kwa wanazopaswa kuziona.

"Mtoto anapoona vitu vya rangi utambuzi wake wa vitu unatanuka. Inamsaidia mzazi kujua mtoto anaona au haoni, hivyo wazazi wanatakiwa kuweka vitu vya rangi tofauti, ili watoto wadogo wavione na kufungua ufahamu wao wa kuangalia,"anaeleza Dk. Akaro

Mtaalamu huyo wa afya anasema, wazazi wanatakiwa kuwavalisha nguo za rangi mbalimbali, akitoa mfano mama anaweza kuvaa nguo za rangi na mtoto anapomuona, anafurahi sana apoona rangi tofauti kwake anajifunza.

"Mtoto akiona rangi ubongo wake unazidi kukua na mtoto anapoona rangi kwake ni chakula cha ubongo, pale anapokuwa na miezi mitatu hadi miezi sita, mtoto rangi zinamfanya achangamke au wazazi wanaweza kuwapa vikalagosi vya rangi tofauti, ili ubongo uchangamke," anasema

**'DAY CARE' JE?**

Katika hilo, Dk Akaro ana hoja zenye sura mbili. Moja ni kwamba upande mmoja wako sahihi na mwingine hawako sahihi.

> **Ukimzoesha mtoto wako ni wa kiume wewe unampa midori au kioo ajiangalie atafikiri maisha yake yake yote vitu hivyo vinafaa kutumiwa naye.**



Mtoto wa kituo cha malezi, amelala mchana baada ya kupewa chakula.

Analifafanua hilo kuwa mtoto wa miaka miwili hadi mitano anatakiwa awe karibu na wazazi kujifunza mengi, kama vile vituo, jambo linalotakiwa kuwapatia upendo wa pekee na muda wa kutosha kucheza na watoto, jambo lenye mchango katika uelewa wao.

Mtaalamu huyo wa watoto anawatahadharisha wazazi wanaowapeleka watoto 'daycare centre' watambue kuwapo tatizo la vitendo vibaya dhidi ya watoto, baadhi wanabakwa, kupigwa na wenzao wanaowazidi umri na kuna baadhi ya wafanyaji kazi, hawana mioyo mizuri, hawawapatii watoto chakula na malazi sahihi.

Katika hilo, Dk. Akaro anasema wanaowapeleka watoto wao katika vituo hivyo vya malezi, wasiwe na uhakika wa ubora wa huduma wanayoitarajia na kutumia fursa wanaporudi, kuwataka wazazi au walezi kuwahoji mengi yanayojenga ubongo wao

**VIFAA VYA MICHEZO**

Dk. Akaro anawatetea wazazi wanaowanunulia midori watoto wa kike na watoto wa kiume kuwanunulia magari au baskeli, kwamba ni hatua sahihi na anatambua kuwa mtoto jinsia yake na kinyume katika kuwapa vifaa visivyoendana na jinsia zao, hasa ikizingatiwa ni kuwajengea tabia hasi au chafu.

"Ukimzoeleshа mtoto wako ni wa kiume wewe unampa midori au kioo ajiangalie atafikiri maisha yake yake yote vitu hivyo vinafaa kutumiwa naye," anasema na kuongeza:

"Mtoto wa kike kumpa vifaa vya kiume, mwishowe atakuwa na tabia za kiume na anaweza kuja kushindwa kuendesha maisha yake ya uhalisia wa kike akiwa mkubwa na hivyo kuathiri mambo mengine ya kijamii."

Hivyo anasema wazazi wanatakiwa kuwaandalia vifaa vya michezo watoto wao vinavyotakiwa ili watoto wacheze na kiataalamu anasema mtoto anatakiwa acheze saa 12, maana ile michezo inamsaidia katika ukuaji wa ubongo huku akidai mtoto ambaye hapati muda wa kutosha wa kucheza ni tofauti kwenye suala la uelewa na yule mtoto anayecheza.

**KUWALAZIMISHA KULALA**

Dk. Akaro anapingana na wazazi wanaolazimisha watoto kulala, badala yake wanatakiwa waachwe walale baada ya kucheza na wanalala bila ya kulazimishwa, jambo lenye umuhimu katika ukuaji wao inawasaidia kiafya katika ukuaji.

Mtaalamu huyo wa watoto anaiambia Nipashe kuwa umri sahihi wa kuanza kuambiwa masuala ya shule ni miaka mitano, hivyo wazazi wanapaswa kuwapeleka chekechea na siyo

INAENDELEA UK.20

AFYA

# Daktari afunguka hatari ya afya kukimbizia mtoto kituo cha malezi

vituo vya malezi, kuwawahisha watoto wanakosa mapenzi na malezi ya baba na mama, ambayo ni muhimu kwa hatua za awali.

### WAZAZI WANAZUNGUMZIA

Mkazi wa Mwada, Dativa Nanai, anasema mzazi anayempeleka mtoto wake katika 'Day Care Centre' anakuwa ametawaliwa na utandawazi na anakosa msaidizi mlezi, hivyo si mahali sahihi katika malezi.

Mkazi wa Hydom Mbulu, John Samo, anasema watu wanaowapeleka watoto kulelewa na vituo vya malezi na kuwarudisha jioni, ni wanaotawaliwa na anachokiita siyo wote kwamba wamekosa walezi wengine wana 'jeuri ya fedha' na 'fahari.

Husna Tluway, mkazi wa Gallapo, anasema wazazi wanaowapeleka watoto kulelewa na watu wengine na kurudishwa jioni, wanatakiwa kutimiza wajibu wao wa kulea, huku mwingine, mkazi wa Babati Pendo Nkulungu, naye ana maoni yake.

Anasema, wanaowapeleka watoto wao katika 'Day Care Centre' hawana wasaidizi na wamebanwa, ila anatahadharisha kuwa wafanyakazi majumbani wana mapungufu katika kuhudumia watoto majumbani, kuliganisha ilivyo kwa wazazi, akija kasoro kama mtoto kunyimwa uji, maziwa na kutosafishwa.

Mama huyo anasema, zamani walikuwa wanawalea na wanapokosa walezi waliendesha shughuli zao binafsi za kijamii na kiuchumi, wakiwa na watoto wao.

Anatoa mfano binafsi, kwamba amewalea watoto wake wote kwa kipindi cha miaka mitatu hadi mitano, akitumia mbinu nyingi kukuza ubongo wao.

Katibu wa Baraza Kuu la Waislamu mkoa wa Manyara, Juma Mkola, anaeleza mbinu ya kulelewa ni kupitia wazazi, sehemu kuu ni wazazi.

"Mtoto baadaye anaweza kushindwa na wazazi na kama mtoto anapelekwa shule ya awali, ni lazima tuangalie anajifunza nini, hivyo ni lazima wazazi tuwe karibu na watoto na tuwalee wenyewe na siyo kuwapeleka kwa watu wengine,"anaisema Mkola

Mkola ana maoni kwamba, wanaoshindwa kuwalea watoto wao mbele ya safari wanawaandaa kuja kuwa na maadili mabaya ila wakiamua kuwalea wenyewe watoto hawawezi kuwashinda wazazi badala yake labda wazazi wanawaachia muda mrefu kukaa na watu wengine ambao wana malezi tofauti.

Msaidizi wa kisheria kutoka shirika la Bapace, Said Mnyaruge, anasema kwa upande mmoja hivi vituo vya kulelea watoto kwa kutwa vinasaidia ila upande mwingine havisaidii na havina msaada kutokana na vitendo vya ukatili



Watoto katika kituo cha malezi yao wakicheza.

> **Mtoto baadaye anaweza kushindwa na wazazi na kama anapelekwa shule ya awali, ni lazima tuangalie anajifunza nini, hivyo ni lazima wazazi tuwe karibu na watoto na tuwalee wenyewe na siyo kuwapeleka kwa watu wengine.**

vinavyotokea na watu wanaowafanyia unyama watoto ni watu wao wa karibu.

Aidha, anawataka wazazi kupunguza ubize ili waweze kuwaangalia watoto na kuwalea inavyotakiwa na anajiuliza je, wazazi wanawakagua watoto wao anadai wajibu mkubwa upo kwa wazazi ili watoto wawe salama?

"Mtoto kule ukimpeleka akiwa hajitambui mtoto huyo hawezi kuwa na mapenzi na upendo na wazazi wake kwa kuwa mtoto anahitaji kuwa karibu sana na wazazi wake ili ajifunze vitu ambavyo vitamsaidia kwenye maisha,"anasema Mnyaruge

### WADAU MALEZI

Mshauri wa Malezi, Makuzi na Maendeleo ya Awali ya Mtoto, Davis Gisuka kutoka shirika la Children in Crossfire(CIC) linalohusika na malezi na makuzi ya mtoto, anasema wazazi halisi na walezi wasikwepe majukumu yao ya msingi.

"Ukiwa karibu na mtoto si tu kwamba unaboresha afya ya makuzi ya mtoto, bali pia unamjengea uwezo wa kujiamini ili kadri anavyokua aweze kuchangamana na wenzake na ndipo anapata fursa ya kujifunza,"anasema Gisuka

Anasema, tofauti kubwa kati ya mtoto anayelelewa na mwingine, asiye kwa mzazi anakosa ukaribu wa mzazi, ambao ni wa asili.

Gisuka anataja mapungufu anayoweza kupata mtoto ni kutomudu lugha au msamiati sahihi, uwezo wa kuchangamana na wenzake na kujimudu katika baadhi ya mabo kama kula chakula na kujisaidia.

Mratibu Malezi, Makuzi na Maendeleo ya Awali ya Mtoto wa CIC, Frank Samson, anawashauri waliotingwa na majukumu kumtumia hata muda mfupi wanaopata, kukaa na watoto ili kujenga mwingiliano kati yao.

" Kama kuna wikiendi uko nyumbani, basi ifanye kuwa siku za 'full time' (kutwa) na mtoto mbebe mgongoni ukiweza , mwogeshe, mlishe, mbadilishe nguo na cheza naye na toa taarifa ofisini siku za kuhudhuria kliniki na zitumie vizuri kama siku maalumu ya mtoto,"anasema Samson, akisisitiza mawasiliano ya simu na mtoto hayatoshi.

### WALIMU DAY CARE

Mwalimu wa kituo cha kulelea watoto cha Yeyo Ccare Day Centre, kilichopo Babati, Rehema Laizer, anasema kituo hicho kinapokea watoto kuanzia mwaka mmoja hadi miaka mitano, wanaowaweka kwenye makundi.

Anataja kundi la kwanza ni wale watoto wenye mwaka mmoja miwili, malenzi yao yakijumuisha kuwavalisha nguo, kuwalisha na kuwafundisha kuongea, huku akifafanua kwamba wana kibali cha kuwapokea kuanzia umri wa miezi tisa.

Mwalimu Rehema anasema, wanawafundisha namna ya kufanya kazi ndogo kwa kutumia vifaa vyao vya kuchezea, mfano maji wanapewa makopo na vifaa vingine vya kuchezea kama midori na fagio, wakiwafundisha kutokana na uelekeo wa mtoto siku hiyo.

Anasema, kuna watoto wenye miaka mitatu wanaowapokea na wanaanza kuwafundisha kusoma na kuhesabu kwa kufuata vitendo, ili imuingie akilini na kujengewa ubongo kukua.

Anakiri kuna watoto 'wanaonogewa' hata wanapofuatwa na wazazi wao wanagoma, kutokana na kwamba muda mrefu wanakuwa kituoni kunakobeba dhamana ya malezi na wana muda mrefu wa kucheza, kuliko darasani.

Rehema anaiomba serikali kuwapunguzia masharti ya kupata usajili, akiyataja wanachopangiwa na serikali ni kigumu, ikiwamo mtaji kati ya Sh. milioni 10 hadi 16 kwenye akaunti yake benki.

Anasema, kituo chake kina watoto na changamoto waliyo nayo ni kucheleweshewa usajili, japo wanahakikishiwa imeshakuwa tayari' kutoka mamlaka ya kiserikali.

Mwalimu Lucy Welwel, anataja changamoto nyingine ni baadhi ya watoto hawawezi kujisaidia au kuongea na wengine wanaletwa wakiwa 'wamedekezwa' kitabia na inakuwa tabia kwao kuchangamana na wenzao, ili kuendana na taratibu zilizopo.

Pia, Mwalimu Recho Mussa, kutoka kituo tofauti, anasema kuna ugumu kutoka watoto wanaowapokea, kwani kuna wakati wanachofundishwa ni tofauti na kile kutoka kwa wazazi wao.

Ushauri wake, ni wazazi wajipange kuwalea watoto katika miaka ya kwanza, kisha ndio wahamie kwenye kituo cha malezi.

### USTAWI JAMII

Ofisa Ustawi wa Jamii wa Halmashauri ya Wilaya Babati Mathias Focus, anasema mtoto anayetakiwa kupelekwa kituo cha malezi anapaswa kuanzia miaka mitatu, japo anadai umri pia ndio stahiki kwa malezi ya baba na mama, kuhusu kile kinachofaa na kisichofaa.

Anakiri, vituo vingi vya kulelea watoto wanaajiri walimu wasiofaa, kwani mwalimu sahihi wasifu wake ni kwamba awe amehitimu katika chuo kinachotambuliwa na serikali, pia hata uzoefu stahiki.

Focus anasema, halmashauri yake ina vituo vitatu, ila vyote amebaini havijasajiliwa na viko kinyume na sheria, hivyo amevifungia kutoa huduma, baada ya kuvikagua.

Anataja vigezo vya sifa ni mmiliki kuwa na uwezo wa kuwalipa wafanyakazi wake, awe ana nyumba yake inayotosha na ana hati yake au kama ni nyumba ya kupanga awe na mkataba sahihi.

Focus anarejea mwongozo unaotumika ni Sheria ya Mtoto ya Mwaka 2009, inayoelekeza mtoto apelekwe kwenye malezi akiwa na umri miaka mitatu hadi mitano.

MWISHO.



# Matatani usajili laini kinyemela

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

MAMLAKA ya Mawasiliano Tanzania (TCRA), Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, imewafikisha kwenye vyombo vya sheria watu wanane wanaodaiwa kusajili holela laini za simu.

Mkuu wa TCRA Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, Mhandisi Asajile John, alisema hayo juzi jijini hapa wakati wa usajili wa laini za simu kwa mfumo wa alama za vidole kwenye Chuo Kikuu cha Mzumbe Tawi la Mbeya.

Mhandisi John alisema wamefanya ukaguzi kwa watu wanaojihusisha na usajili wa laini za simu na kubaini baadhi yao kutozingatia kanuni na sheria za kazi hiyo.

Alisema ukaguzi huo ulifanyika kwa kushirikiana na kampuni za simu za mkononi na Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA), ili kuhakikisha uhalifu kwenye sekta ya mawasiliano unakwisha.

"Ukaguzi wa laini za simu ni endelevu na tumeweka utaratibu wa kutembelea maeneo mbalimbali ya mkoa wa Mbeya ili kuangalia namna utoaji huduma ulivyo. Lakini pia tunawapa tahadhari wanaosajili kuzingatia maadili ili kuepukana na vitendo vya wizi," alisema Mhandisi John.

Pia aliishauri jamii kuacha tabia ya kusajili laini mitaani badala yake watumie kampuni za simu kwa usalama wao. Naye Ofisa Usajili wa Vitambulisho vya Taifa (NIDA) Mkoa wa Mbeya, Alavuya Ntalima, alisema mwitikio wa wananchi kusajili vitambulisho ni mkubwa kwa kuwa mpaka sasa umefikia kwa asilimia 80.

Alisema licha ya usajili wa vitambulisho kufanikiwa kwa kiwango kikubwa bado kuna changamoto ya wananchi kujiandikisha zaidi ya mara moja.

Aliwataka wananchi kufuata matakwa ya usajili wa vitambulisho vya taifa ambayo yanahitaji mtu kujiandikisha mara moja ili kurahisisha kazi hiyo.



Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano (sekta ya ujenzi), Elius Kwandikwa, akikata mfuko wa saruji aliposhiriki kazi ya kusambaza saruji katika ujenzi wa barabara ya Njombe - Moronga yenye urefu wa km 53.9 ambayo ni sehemu ya barabara ya Njombe–Ndulamo-Makete km 107.4 inayojengwa kwa kiwango cha lami, mkoani Njombe juzi. **PICHA: WUUM**

# Mil. 9/- zaokolewa ununuzi maji tiba

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

SHILINGI milioni tisa zinaokolewa kila mwezi kwa ajili ya kununulia maji tiba katika Hospitali ya Rufani Kanda Mbeya baada ya kuanzishwa kiwanda cha kutengeneza maji hayo.

Mkurugenzi wa Hospitali ya Rufani ya Kanda ya Mbeya, Dk. Godlove Mbwanji, alisema hayo jana wakati wa ziara ya Kamati ya Siasa ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) Wilaya ya Mbeya Mjini ili kujionea miradi mbalimbali inayotekelezwa.

Dk. Mbwanji alisema kiwanda hicho kimerahisisha utoaji wa huduma kwa wagonjwa kulinganisha na awali ambapo serikali ilikuwa inatumia gharama kubwa kuagiza maji hayo nje ya nchi.

Mkurugenzi huyo aliongeza kuwa kiwanda hicho kwa siku kinazalisha chupa 480 zenye ujazo wa nusu lita kila moja ambazo zinatosheleza mahitaji ya hospitali hiyo. Alisema kiwanda hicho kimesaidia kukabiliana na uhaba wa maji tiba hospitalini hapo na kwamba ziada ya maji hayo itauzwa maeneo mengine yenye uhitaji ili kujiongezea kipato.

"Hospitali yetu ilikuwa inatumia Sh. milioni tisa kwa ajili ya ununuzi wa maji tiba. Baada ya kuanzisha kiwanda cha kutengeneza maji hayo, fedha hizo zinatumika kwenye mahitaji mengine. Lengo letu ni kuhakikisha tunaongeza uzalishaji ili kuwafikia wahitaji wengi nje ya wagonjwa hospitalini hapa," alisema Dk. Mbwanji.

Alisema kiwanda hicho kimekuwa cha mfano kwa sababu hospitali mbalimbali za rufani hutembelea hapo kwa lengo la kujifunza na kwamba Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, ilipongeza uanzishwaji utengenezaji maji tiba.

Pia alisema katika kuhakikisha hospitali inaboresha utoaji huduma, ikiwamo miundombinu, wameanzisha huduma ya kipimo cha CT Scan na ufungwaji wa mashine za kisasa na X- Ray.

Mwenyekiti wa CCM Mbeya Mjini, Afrey Msomba, alisema ameridhishwa na huduma zinazotolewa pamoja na utendaji wa kazi wa uongozi wa hospitali hiyo.

# Wanawake washauriwa kujiunga kwenye vikundi

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

WANAWAKE mkoani Mbeya wametakiwa kujiunga na vikundi vya ujasiriamali ili kunufaika na fursa mbalimbali zinazotolewa na serikali, ikiwamo mikopo ya halmashauri ambayo ni asilimia 10 ya mapato ya ndani ambayo hutolewa kwa wanawake, vijana na watu wenye ulemavu.

Ushauri huo ulitolewa jana na Ofisa Biashara wa Wilaya ya Mbeya, Elizabeth Iyombe, wakati akizungumza na Nipashe juu ya mwamko wa wanawake katika kuzichangamkia fursa mbalimbali za kiuchumi zinazotangazwa.

Iyombe alisema kwa sasa kuna fursa nyingi za wanawake wajasiriamali hasa ambao tayari wamejiunga kwenye vikundi kwa madai kuwa kwa sasa kila anayetaka kuwasaidia anataka wawe kwenye vikundi.

Pamoja na kwamba serikali imetenga asilimia nne ya mapato ya ndani ya halmashauri kwa ajili ya wanawake, mwamko wa kundi hilo kujitokeza kukopa fedha hizo ni mdogo kutokana na kutojiunga na vikundi.

"Nawaomba wanawake kutumia vizuri fursa zinazotolewa, lakini kutumia vyema elimu ya ujasiriamali iliyotolewa ili kuinua kipato cha familia zao na kuwa na uwezo wa kujitegemea katika maisha yao, huku biashara zao zikiendelea kustawi," alisema Iyombe.

Baadhi ya wajasiriamali ambao wameanzisha biashara zao, Amina Mwambopo, ambaye ni mfanyabiashara wa mitumba katika Soko la Sokomatola jijini Mbeya, alisema mara nyingi wanawake wanashindwa kuendelea kwa sababu wanakuwa na tamaa ya kununua kila kitu.

Alisema wakati mwingine wanajikuta wanatumia fedha za biashara kwenye matumizi mengine ikiwamo kununua nguo na vyakula.

Mwambopo aliwashauri wajasiriamali wenzake kurasimisha biashara zao kwa kuwa na leseni za Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) na kwa wale ambao mitaji yao bado midogo, wawe na vitambulisho vya wajasiriamali vilivyotolewa na Rais.



HABARI DODOMA

# Watumishi wa afya kero kuchukuliwa hatua

**Na Mwandishi Wetu,** CHAMWINO

SERIKALI imewaagiza waganga wakuu wa mikoa na wilaya kuwafuatilia na kuwachukulia hatua stahiki watumishi wa afya ambao wamekuwa kero kwa wananchi kutokana na lugha chafu kwa wagonjwa.

Sambamba na hilo, Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Chamwino, ameagizwa kuchukua hatua stahiki za kiutumishi dhidi ya mtumishi Claude Chilala wa Kituo cha Afya Mpwayungu, anayetuhumiwa na wananchi kukiuka maadili ya kiutumishi na kuwa kero sugu kwa wateja.

Naibu Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi) anayeshughulikia afya, Dk. Dorothy Gwajima, alitoa maagizo hayo juzi alipokuwa akikagua ujenzi wa miundombinu na utoaji huduma kwenye Kituo cha Afya cha Mpwayungu, wilayani hapa.

Hatua hiyo ya Dk. Gwajima ilitokana na wananchi wa eneo hilo kuwalalamikia baadhi ya watumishi kuwa bado wanatumia lugha chafu ambazo haziwavutii wananchi kupata huduma. Kutokana na kero hiyo, Dk. Gwajima aliwataka waganga hao kufanya ufuatiliaji wa kero za wananchi kwenye vituo vya afya na kuchukua hatua stahiki pindi itakapobainika kuna mtumishi ametumia lugha chafu kwa mteja.

Aidha, aliwaagiza wakurugenzi wa halmashauri kuhakikisha wanachukua hatua stahiki kwa wakati pale wanapowasilishiwa malalamiko na si kukaa miezi sita bila kuchukua hatua kama ilivyotokea kituoni hapo.

"Nakuagiza Mkurugenzi wa Halmashauri ya Chamwino kuhakikisha unafanyia kazi malalamiko ya wananchi na kuchukua hatua stahiki za kiutumishi dhidi ya mtumishi Claude Chilala ambaye anatuhumiwa na wananchi kukiuka maadili ya kiutumishi na kuwa kero sugu kwa wateja," aliagiza.

Dk. Gwajima alisema ukosefu wa hatua stahiki dhidi ya kero zinazoripotiwa na wananchi ni moja ya mambo yanayowakwaza wananchi na kuamua kutotumia vituo husika.

"CHMT na RHMT hakikisheni mnafuatilia na kusimamia utendaji kazi wa watumishi katika vituo vya kutolea huduma, kutoa msaada na ushauri wa kitaalamu pia, kusikiliza kero za wananchi dhidi ya huduma na katika kila jambo, kuchukua hatua stahiki kwa wakati na bila kuonea upande wowote ule. Msisubiri hadi Wizara itembelee ndiyo iibue hizi kero wakati mpo huku," alisema.

Naibu Katibu huyo aliwataka watumishi kutoiga tabia ambazo zinakiuka maadili ya utumishi wa umma.

Awali, wananchi wa Mpwayungu walisema pamoja na jitihada za serikali kuwajengea miundombinu ya afya kwenye eneo hilo, lakini bado kuna changamoto ya lugha chafu kwa wagonjwa.

Akizungumza kwa niaba ya wananchi hao, Mwenyekiti wa Kamati ya Usimamizi wa Kituo hicho, Chibwele Magubika, aliiomba serikali ihakikishe watumishi wa kada hiyo wanakuwa na lugha nzuri kwa wateja ili wananchi wavutiwe kupata huduma.



Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, DK. Ave Maria Semakafu, akizungumza wakati wa kufunga mafunzo ya wiki mbili ya Habari, Teknolojia na Mawasiliano (Tehama) kwa wakufunzi wa vyuo vya ualimu nchini, yalifanyika Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM), jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Elimu bure yaipaisha Tanzania SDG

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MPANGO wa utoaji elimu bila malipo ambao umechangia kuongeza udahili wa watoto wengi kupata fursa ya kupata elimu, umeisaidia Tanzania kupiga hatua kubwa katika utekelezaji wa Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDG).

Hayo yalibainishwa jana na Mbunge wa Viti Maalum, Fatuma Toufiq, ambaye pia 'champion' wa masuala ya SDG bungeni, alipokuwa akizungumzia mrejesho wa mkutano aliohudhuriwa wa 'high level political forum' uliofanyika Umoja wa Mataifa (UN) hivi karibuni.

Toufiq ambaye pia ni Mkurugenzi wa Shirika linalojishughulisha na Wanawake na Watoto (Wowap), alisema katika mkutano huo ambao alipelekwa kwa ufadhili kutoka Shirika la Equal Measure 2030 la Marekani, imeelezwa kuwa Tanzania imepiga hatua kubwa katika kufikia maendeleo endelevu.

Alibainisha kuwa shirika hilo linalojihusisha na masuala ya usawa wa kijinsia, linasaidia nchi zinazoendelea kufikia malengo hayo ili kuhakikisha kunakuwa kuna usawa kwenye mambo mbalimbali ikiwamo elimu.

Mbunge huyo alisema kwenye suala la udahili wa wanafunzi kwa shule za msingi Tanzania ndio inayoongoza kwa Bara la Afrika.

"Mkutano huo ulikuwa wa utoaji taarifa jinsi nchi ilivyofanya katika utekelezaji wa SDGs, na Tanzania ndio ilikuwa mara yake ya kwanza kutoa ripoti yake na ripoti iliwasilishwa na Waziri wa Fedha Dk. Philip Mpango ambaye alikuwa mkuu wa msafara na kwenye mkutano ule, tumeonyesha tulivyopiga hatua hali ambayo hatukupata maswali mengi," alisema.

Pia alisema yeye alikwenda kwenye mkutano huo kuzungumzia masuala ya elimu ambayo Tanzania imepiga hatua kubwa kwenye sekta ya elimu kupitia mpango wake wa elimu bure.

Alifafanua lengo la nne la malengo ya maendeleo endelevu linalozungumzia ubora wa elimu limeonyesha Tanzania ilivyotekeleza kwa kiwango kikubwa.

"Imeonyesha namna ambayo sisi tuna sera ya elimu bure ambapo uandikishaji wa wanafunzi ni asilimia kubwa hivyo imetoa fursa ya watoto kupata elimu," alisema.

Pamoja na hayo, Toufiq alisema pia kwenye lengo linalohusu masuala ya mazingira, upatikanaji wa haki kwa raia wake ambapo mifumo ya kisheria ipo na mahakama zimejengwa.

# Wizara sasa kuboresha ufundishaji kwa Tehama

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

NAIBU Katibu Mkuu wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Dk. Ave Maria Semakafu, amesema katika mpango wa ununuzi mwaka huu, watahakikisha wananunua kompyuta mpakato (laptop) na kuzisambaza katika vyuo vya mafunzo ya ualimu ili kuwezesha ufundishaji kwa teknolojia ya habari na mawasiliano (Tehama).

Dk. Semakafu aliyasema hayo jana alipokuwa akifunga mafunzo ya wiki mbili ya Tehama kwa wakufunzi 367 wa vyuo mbalimbali vya ualimu nchini.

Alisema wizara yake inamkakati wa kuongeza kompyuta katika vyuo mbalimbali ili kusaidia kasi ya matumizi ya Tehama katika kufundishia na kujifunza.

Pia alisema mafunzo hayo yalitolewa kwa wiki mbili chini ya wizara yake vyuo vya ualimu vinatakiwa kwenda kuyafanyia kazi ili kuboresha ufundishaji katika maeneo yao.

"Kila chuo kiende kikaweke mkakati wa namna ya kuendeleza mafunzo haya na kuwawezesha watu wengine ambao hawakubahatika kupata fursa hii na sisi kama serikali tutaweka mkakati wa kuyafanya kuwa endelevu ikiwezekana yawe yanatolewa kila mwaka," alisema Dk. Semakafu

Alisema kutokana na dunia ya sasa kubadilika matumizi ya Tehama yatasaidia katika ufundishaji hasa katika kukabiliana na uhaba wa vitabu.

"Katika dunia ya leo sitegemei kusikia mkufunzi au mwanafunzi anasema kuwa tunauhaba wa vitabu wakati ukiingia katika mitandao mbalimbali unapata vitabu vya bure pamoja na vile vingine vya kulipia," alisema.

Aidha, Dk. Semakafu alisema atamshauri katibu mkuu wa wizara hiyo ili kuachana na ununuzi wa kompyuta za mezani ambazo zimekuwa katika mpango wa ununuzi hivi sasa badala yake, zinunuliwe kompyuta mpakato.

Mmoja wa washiriki wa mafunzo hayo mkufunzi kutoka Chuo cha Ualimu Tandara mkoani Njombe, James Mwandepu, alisema mafunzo hayo yamekuwa muhimu sana kutokana na kuhusisha ufundishaji kwa njia ya Tehama ambao utasaidia kufikisha ujumbe kwa njia nyepesi kwa wanafunzi.



# Waziri awapa neno waliosoma ughaibuni

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Riziki Pembe Juma, amewataka wanafunzi wanaosoma na waliomaliza vyuo vikuu nchini China, kuitumia fursa waliyoipata kuwaelimisha vijana wengine ili nao waombe nafasi za masomo nje ya nchi na hatimaye kuleta maendeleo ya taifa.

Alisema hayo jana katika mazungumzo na wanafunzi hao yaliyofanyika ofisini kwake Mazizini Mjini Unguja.

Katika mazungumzo hayo, Waziri Riziki aliagiza kuitumia fursa hiyo kwa kuwa baadhi ya vijana wanashindwa kuomba nafasi hizo kwa kuhofia kutojua lugha ya Kiingereza.

Alisema katika nafasi hizo, kumekuwapo mchanganyiko wa nchi mbalimbali na makabila tofauti na baadhi yao hawajui Kiingereza na kwa kiasi kikubwa wanazichangamkia fursa hizo.

Pia alisema kuna tabia baadhi ya watu hutumia mitandao ya kijamii kuzituma nafasi hizo za masomo za nje ya nchi ambazo wakati mwingine zimeshapita muda au kutokuwapo kabisa nchi husika, hivyo kusababisha kuwapotezea muda na mwelekeo kwa wanaoomba nafasi hizo.

Alisema Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar imekuwa ikiziweka wazi nafasi mbalimbali za masomo za nje ya nchi kupitia tovuti yake ili kuwasaidia wote wanaohitaji kuomba nafasi hizo.

Aidha, aliwataka kuwa wazalendo na nchi yao kwa kurejea nchini watakapomaliza masomo yao ili kulitumikia taifa lao, kwani bado Zanzibar inahitaji wasomi katika kuleta maendeleo ya kila fani.

Akizungumza kwa niaba ya wanafunzi wenzake, Salum Mohammed Ramia, alimwomba waziri huyo kuandaa siku maalum ya utamaduni kwa vyuo vya Zanzibar kwa kuwa kufanya hivyo kutasaidia kuvitangaza vyuo hivyo nje ya nchi pamoja na kukuza Kiswahili ambacho ni sehemu ya utamaduni wao.

Pia aliishauri kufanya kongamano la vijana litajalowashirikisha wanavyuo wote wa ndani na nje ya nchi kujadili masuala ya elimu kwa ujumla ili kuleta ufanisi wa elimu nchini.

# Ataka utunzaji vyanzo vya maji

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MAKAMU wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Balozi Seif Ali Iddi, amewataka wananchi kutunza vyanzo vya maji vilivyo katika maeneo yao ili kurahisisha upatikanaji wa huduma ya maji safi na salama.

Balozi Iddi aliyasema hayo jana wakati wa uzinduzi wa mradi wa majisafi na salama katika nyumba mpya za askari wa Jeshi la Polisi, Mahonda, Mkoa wa Kaskazini Unguja.

Alisema baadhi ya wananchi hawatunzi vyanzo hivyo vya maji jambo ambalo husababaisha ukosefu wa huduma hiyo katika maeneo mengi.

Kwa mujibu wa Balozi Iddi, kumekuwapo na tabia ya kukata miti ovyo katika vyanzo vya maji kwa matumizi ya kuni, mkaa na shughuli za ujenzi katika vyanzo vya maji na kusababisha kwa kiasi kikubwa kukosekana upatikanaji wa maji safi na salama kutokana na vyanzo kukauka.

"Uharibifu wa vyanzo vya maji umekithiri kwa kiasi kikubwa sana. Watu wanakata miti huku wengine wanajenga makazi ya kudumu katika vyanzo hivyo, jambo linalosababisha upatikanaji wa huduma kusuasua katika maeneo husika na hata kukauka kwa vyanzo hivyo," alisema.

Aidha, aliwataka wananchi kuitunza miradi hiyo ya maji inayotolewa na wahisani kwa kuwa imewapunguzia tatizo la majisafi na salama ambalo wamekuwa wakikumbana nalo hapo awali. Naye Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Hamad Masauni, alisema mradi huo hautasaidia Jeshi la Polisi pekee baada ya nyumba hizo kukamilika, bali hata wananchi wanaoishi katika eneo hilo pia.

Alisema kukamilika kwa mradi huo, kutawapunguzia wananchi tatizo la maji wanaokabiliana nalo kwa muda mrefu.

Mradi huo wa visima vitatu vya maji safi na salama katika maeneo mbalimbali umefadhiliwa na Shirika la Direct Aid na umegharimu Dola za Kimarekani 6,000.



Mkazi wa Jiji la Dar es Salaam akiperuzi vitabu vinavyouzwa kando ya Barabara ya Bibi Titi Mohamed, jirani na Chuo cha Elimu ya Biashara, jijini Dar es Salaam jana. Kwa mujibu wa muuzaji huyo, mwamko mdogo wa watu kujisomea vitabu umesababisha biashara hiyo kuwa ngumu. **PICHA: JOHN BADI**

# Tadea yampa tano JPM kwa uthubutu

**Na Rahma Suleiman,**ZANZIBAR

CHAMA cha Siasa cha Tadea, kimempongeza Rais John Magufuli kwa ujasiri wake wa utekelezaji wa mradi mkubwa wa kufua umeme katika Mto Rufiji.

Makamu Mwenyekiti wa chama hicho, Juma Ali Khatib, alisema hayo juzi alipozungumza na Nipashe na kupongeza juhudi hizo ambazo zinatokana na ujasiri na uthubutu katika kuleta maendeleo.

Alisema chama hicho kinamuungamkono Rais Magufuli katika utekelezaji wa mradi huo ambao ni mkombozi kwa Tanzania katika upatikanaji wa umeme wa uhakika na kutosheleza mahitaji ya ndani na kwa nchi jirani.

Alisema wakati Tanzania ikiwa katika mikakati yake ya kuelekea katika nchi ya viwanda, umeme ni nishati muhimu inayohitajika katika kufikia azma hiyo.

"Huwezi kuyafikia malengo ya nchi ya viwanda kama huna umeme wa kutosha. Umeme kutoka Mto Rufiji ndilo suluhisho la mwisho la Tanzania kuwa na nishati yake ya uhakika," alisema.

Khatib pia alisema utekelezaji wa mradi huo utaleta unafuu mkubwa kwa Zanzibar ambayo nayo iko katika mikakati ya kuelekea katika uchumi wa viwanda vya kati ambao matumizi ya nishati ya umeme yanahitajika.

"Mradi huu ukifanikiwa, utekelezaji wake utaleta unafuu mkubwa kwa Zanzibar ambayo nayo ni moja ya watumiaji wakubwa wa umeme wa gridi ya taifa," alisema.

Sambamba na Rais Magufuli, alimpongeza Rais wa Zanzibar, Dk. Ali Mohamed Shein, kwa uongozi wenye hekima na busara ambao umelenga kuleta maendeleo makubwa kwa wananchi wa pande mbili za Muungano.

Alisema uongozi wao wa busara umeifanya Tanzania kuwa kimbilio la viongozi mbalimbali wa Afrika Mashariki na Kati kufika nchini na kuchota busara zinazotokana na utulivu na amani.

Aliwataka viongozi wengine wa vyama vya upinzani kuwaunga mkono viongozi hao ili waiongoze Tanzania na kuleta neema kubwa kwa wananchi wote.

Mradi wa kufua umeme kutoka Mto Rufiji uliwekwa jiwe la msingi hivi karibuni na Rais Magufuli. Hadi kukamilika kwake mwaka 2022, utakuwa na uwezo wa kuzalisha megawati 2,115.

Mradi huo ni ndoto ya Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Nyerere ya miaka ya 1970 ambayo sasa imetimizwa na Rais Magufuli.

# Programu tano kilimo kuzinduliwa Nanenane

**Na Happy Severine,** SIMIYU

WAZIRI wa Kilimo, Japhet Hasunga, amesema jumla ya programu tano za kimkakati za kuboresha sekta ya kilimo na mazao yake zitazinduliwa rasmi wakati wa Maonyesho ya Sikukuu ya Wakulima (Nanenane) kitaifa inayofanyika viwanja vya Nyakabindi mkoani Simiyu.

Hasunga, aliyasema hayo jana wakati akizungumza na waandishi wa habari kwenye viwanja hivyo baada ya kukagua maandalizi ya maonyesho hayo.

Alisema serikali imedhamiria kuifanya sekta ya kilimo kuwa mkombozi wa uchumi wa nchi.

Vile vile, programu hizo zitazinduliwa na viongozi wakuu wa kitaifa, wakiwamo Rais John Magufuli, Makamu wa Rais, Samia Suluhu na Waziri Mkuu Kassim Majaliwa na kati ya programu hizo upo mfumo wa kudhibiti upotevu wa mazao ya wakulima.

Programu nyingine itakayozinduliwa ni bima ya mazao ikiwa na lengo la kuwasaidia wakulima na wawekezaji kwenye kilimo endapo watapata hasara kwa mazao yao kukumbwa na mafuriko, ukame na magonjwa.

Pia programu nyingine ni uzinduzi wa mfumo wa soko la bidhaa ambao utakuwa wa kielektroniki utakaosaidia kupata masoko na kuuza mazao kwenye soko la dunia, pamoja na kuzinduliwa mfumo wa kielektroniki unaolenga kuboresha biashara ya mazao ya wakulima.

"Mfumo huu wa kielektroniki wa tatu umelenga kuondoa vikwazo kwa wafanyabiashara ambao wanauza mazao yetu nje ya nchi katika kupata vibali na leseni, tunataka sehemu popote walipo waweze kupata vibali hivi kwa njia ya mtandao," alisema.




Balozi wa Uturuki nchini, Ali Davutoglu (katikati) na Mkurugenzi wa Shirika la Ndege la Uturuki, Ahmet Sahin (kushoto), wakimkabidhi Mkurugenzi wa Vodacom Business Unit, Arjun Dhillon, mfano wa ndege kuashiria uzinduzi rasmi wa huduma ya malipo kwa M-Pesa ambayo wateja wao watapata punguzo la bei kwa asilimia 15 pindi wanaponunua tiketi ya ndege kutoka shirika hilo, kuanzia leo hadi Desemba Mosi, mwaka huu. Ofa hiyo ilitangazwa katika hafla fupi iliyofanyika ofisi za Ubalozi wa Uturuki jijini Dar es Salaam, jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Watahadharishwa nyamapori kuepuka ebola

**Na Lilian Lugakingira,** BUKOBA

WAKAZI wa Mkoa wa Kagera wametahadharishwa kula nyamapori au yoyote ambayo haijapimwa kitaalamu ili kuepuka kupata maambukizi ya ugonjwa hatari wa ebola ambao umethibitika kuwapo katika baadhi ya nchi jirani ikiwamo Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo.

Tahadhari hiyo ilitolewa na Mganga Mkuu wa Mkoa wa Kagera, Dk. Marco Mbata, wakati wa mkutano wa kuzindua zoezi la kuigiza hali halisi ya utayari wa kukabiliana na mlipuko wa homa ya virusi vya ebola na mazoezi ya utayari yatakayofanyika katika mikoa ya Kagera na Kigoma kuanzia Julai 29 hadi Agosti 9, mwaka huu.

Dk. Mbata alisema dawa kwa ajili ya kutibu ugonjwa huo zipo na suala muhimu ni wananchi kuchukua tahadhari na kutoa taarifa mapema wanapoona mtu wanayemtilia shaka ili hatua za haraka za kumpeleka katika vituo vilivyoandaliwa zifanyike.

"Kikubwa ni kuwaelimisha wananchi ili kuepuka vitu ambavyo hawapaswi kugusa mfano jasho, damu, majimaji, wasile popo, wasile nyamapori au yoyote ambayo haijapimwa kitaalamu kuhakikisha kuwa iko salama," alisema.

Kwa upande wake Katibu Tawala wa Mkoa wa Kagera, Profesa Faustine Kamuzora, aliwataka wananchi, watendaji na viongozi kila mmoja kwa nafasi yake, kushiriki kikamilifu kuzuia ugonjwa huo usiingie katika mkoa huo unaopakana na nchi nyingi zikiwamo za Rwanda, Burundi, Kenya na Uganda, lakini pia ni rahisi kwa watu kutoka Kongo kuingia kupitia Omurusagamba wilayani Ngara.

Profesa Kamuzora alisema mkoa kupakana na nchi nyingi ni fursa kubwa kiuchumi, lakini inapotokea magonjwa hatari kama ebola katika nchi hizo ni hatari kwa mkoa na taifa.

"Wale ambao wana jukumu la kupokea wageni, lazima wafahamu wanatoka wapi na afya zao zikoje, wasipofanya kazi zao vizuri wanaweza kuuweka mkoa na nchi katika hatari, tunachoomba ni wananchi wote lazima tujielimishe jinsi tunavyoweza kutambua wagonjwa wa ebola," alisema.

Akizungumza wakati wa mkutano huo mtaalamu wa masuala ya dharura kutoka Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Faraja Msemwa, alisema baada ya kuzuka kwa ugonjwa huo nchini DRC mbali na Kagera kuna mikoa mingine minane ilifanyiwa tathmini ikihofiwa kuwa katika hatari na kutaja mikoa mitatu ya Kagera, Kigoma na Mwanza.

"Mikoa mingine ni Katavi, Rukwa, Songwe, Mbeya, Dar es Salaam na Dodoma ambao kwa sasa umeonekana kuwa na mwingiliano mkubwa, ndiyo maana tuko hapa Kagera maana tumeanza mazoezi katika mikoa ambayo tuliona iko katika hatari zaidi na baada ya hapa tutakwenda Kigoma," alisema Dk. Msemwa.

Alisema kwa takriban mwaka mmoja, wamekuwa wakiendelea na mazoezi ya namna ya kujikinga na ugonjwa huo na kuwa kinachofanyika sasa ni kupima utayari ili kuona kwa sasa watumishi wa afya wako katika kiwango gani cha kufuata miongozi iliyoandaliwa, hasa katika maeneo ya mipakani.

Kufuatia zoezi hilo jopo la wataalamu kutoka Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Ofisi ya Waziri Mkuu kitengo cha maafa, Shirika la Afya Duniani (WHO), Shirika la Misaada la Marekani (USAID) na Shirika la Chakula Duniani (FAO) na wadau wengine wako mkoani Kagera kwa muda wa siku tano kuanzia Julai 30 hadi Agosti 3, mwaka huu.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na mwakilishi wa WHO katika mkutano huo Dk. Refaya Ndyamuba, mnamo Julai 21 mwaka huu kesi 2,592 na vifo 1,743 viliripotiwa nchini Kongo na kufanya viwango vya hatari vya vifo kufikia asilimia 67.

# Mchimbaji mdogo ajitolea kujenga zahanati

**Na Mohab Dominick,** KAHAMA

WANANCHI wa Kijiji cha Kakola Namba Tisa, Kata ya Bulyanhulu, Halmashauri ya Msalala wilayani Kahama, wamefurahishwa na kitendo cha mchimbaji wa dhahabu, Husein Mwananyanzara, kujitolea kujenga zahanati ili kuokoa vifo vya mama na mtoto.

Walisema Mwananyanzara ambaye ni mchimbaji mdogo anayesimamia mgodi mdogo wa Namba Tisa ameanza kuonyesha msaada mkubwa katika kusaidia shughuli za maendeleo kwa jamii.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti na waandishi wa habari hivi karibuni wananchi hao walisema kuwa kwa sasa zahanati inayotarajiwa kujengwa na mchimbaji huyo itakuwa msaada mkubwa kwa wanawake waliokuwa wakitembea umbali wa zaidi ya kilomita 30 kwenda kujifungua.

Pia walisema wengine hulazimika kwenda katika kituo cha afya Mwingilo kilichopo katika Halmashauri ya Nyanghwale, mkoani Geita ili kupata huduma za matibabu pamoja na kujifungua kutokana na ukosefu wa huduma za afya kijijini kwao.

Ester Thomas na Salome Nhalima, wakazi wa kijiji hicho wakionyesha furaha yao, walisema kitendo cha kujengwa zahanati katika maeneo yao ni kuwasogezea huduma za afya na watakuwa wamepunguziwa kutembea umbali mrefu kufuata huduma za matibabu.

Naye mchimbaji huyo Mwananyanzala, aliwaambia waandishi hao kuwa ameguswa na hali ya wanakijiji hao kutokana na kukosekana kwa huduma za matibabu katika eneo lao licha ya kuwa msimamizi wa mgodi huo.

"Nitashirikiana na serikali katika ujenzi wa zahanati katika kijiji hiki cha Namba Tisa ili kuwaondolea adha ya kutembea umbali mrefu wa kwenda kupata huduma za matibabu nje na kijiji chao binafsi pamoja na kuguswa na usumbufu wanaopata kinamama wanaotaka kujifungua pia ninatekeleza ombi la Mkuu wa Wilaya ya Kahama, Anamringi Macha, tuache alama kijijini hapa kwa kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo," alisema.

Kwa upande wake Mwenyekiti wa Serikali ya Kijiji hicho, Emmanuel Nkenze, alikiri mchimbaji huyo kujitolea kujenga zahanati ili kunusuru vifo vinavyotokana na uzazi.

Alisema mchimbaji huyo pia ameshiriki katika ujenzi wa ofisi ya kijiji chake kwa kuungana na kikundi cha Igemelo kilichopo namba mbili na kuongeza kuwa serikali ya kijiji na wilaya kwa ujumla walikwisha toa baraka ya kutekeleza suala la miradi ya maendeleo katika kijiji hicho.

## HABARI KIMATAIFA

# Shule zafungwa baada ya mauaji

**KHARTOUM,** Sudan

BARAZA la kijeshi Sudan limeamuru shule zote nchini humo kufungwa kwa muda usiojulikana kufuatia maandamano ya wanafunzi kupinga kuuawa kwa waandamanaji sita, wakiwamo wanafunzi watano mjini Al-Obeid siku ya Jumatatu.

Siku ya Jumanne mamia ya wanafunzi waliandamana katika mitaa ya mji wa Khartoum, wakiwa wamevalia sare za shule huku wakipeperusha bendera za Sudan na kukariri maneno wakisema: "kuuwa mwanafunzi ni kuuwa taifa."

Maandamano ya hayo ya wanafunzi yalifanyika pia katika sehemu nyingine za Khartoum na miji mingine.

**Kilichotokea mjini al-Obeid na kila kitu kilichotokea kabla ni mambo yanayosikitisha.**

Katika maandamano hayo wanafunzi watano wa sekondari walipigwa risasi na kuuawa na wengine zaidi ya 60 walijeruhiwa na wanajeshi walipoandamana mjini Al-Obeid kupinga uhaba wa mafuta na mkate.

Juzi kamati ya madaktari wanaoegemea vuguvugu la maandamano ilisema mwandamanaji mwingine alifariki dunia baada ya kupigwa risasi kichwani. Lakini halikusema kama alikuwa mwanafunzi.

Waandamanaji walikituhumu kikosi kinachoogopwa cha Rapid Support Forces (RSF) kwa kuauwa wanafunzi hao. Shirika la Habari la Serikali ya Sudan (SUNA) limesema kuwa baraza la kijeshi limewaagiza magava wa majimbo yote kuzifunga shule za chekechea, msingi na sekondari kuanzia jana hadi itakapotolewa taarifa nyingine.

Mauaji hayo yalitokea siku moja kabla viongozi wa maandamano kufanya mazungumzo na majenerali wa baraza la kijeshi juu ya masuala yaliosalia kuhusu kuundwa kwa serikali ya kiraia baada ya pande mbili kusaini makubaliano ya kugawana madaraka mwanzoni mwa mwezi huu.

Lakini viongozi wa maandamano hao walifuta mkutano uliokuwa ufanyike Jumanne.

Mkuu wa Baraza la kijeshi, Adel Fattah al-Burhan alisema katika mahojiano yaliotangazwa juzi usiku kuwa mauaji ya wanafunzi hao yalikuwa ni ya kusikitisha na kutoa wito wa kurejea haraka kwenye meza ya mazungumzo kukamilisha mchakato wa mpito wa kisiasa.

"Kilichotokea mjini al-Obeid na kila kitu kilichotokea kabla ni mambo yanayosikitisha. Hakuna anayekubali vifo au mauaji ya raia yeyote wa Sudan, na hii inaweza kuwa mojawapo ya sababu zinazotusukuma kusaini makubaliano haraka iwezekanavyo kurejesha maisha katika hali ya kawaida," alisema Adel Fattah al-Burhan.

Maandamano ya kuipinga serikali yalianza mwishoni mwa mwaka uliopita ambapo waandamanaji walikuwa wakishinikiza kuhitimishwa kwa utawala wa kiongozi wa muda mrefu wa nchi hiyo, Omar al-Bashir. **DW**



Wananchi wa Sudan wakiwa kwenye maandamano kupinga hatua ya Jeshi la nchi hiyo kuchukua madaraka ya uongozi. **PICHA: REUTERS**

## Ghasia zazuka, waandamanaji 44 wakamatwa

**HONG KONG,** China

WAANDAMANAJI wanaotetea demokrasia nchini Hong Kong wamekabiliana na Polisi, juzi baada ya wenzao 44 kukamatwa na kufunguliwa mashtaka ya kuzua ghasia.

Hii ni mara ya kwanza mashtaka kama hayo kufunguliwa tangu maandamano yalipoanza Juni, mwaka huu.

Polisi wametumia mabomu ya kutoa machozi kuzuia vurugu na kuwatawanya waandamanaji waliojitokeza nje ya kituo cha polisi katika wilaya ya Kwai Chung.

Hata hivyo, katika ghasia hizo waandamanaji walijibu kwa kuwarushia polisi chupa za plastiki na miavuli.

Juzi, waandamanaji walisababisha kukwama kwa huduma za usafiri wa treni ya chini ya ardhi na kuwazuia wasafiri kutoka kwenye treni. **VOA**

## Jeshi lakataa masharti ya wapatanishi

**ALGIERS,** Algeria

MKUU wa Jeshi la Algeria, Ahmed Gaïd Salah amekataa hatua za kuafikiana zilizoombwa na jopo la wapatanishi ili kuanzisha mazungumzo kuhusu mfumo wa uchaguzi wa urais nchini humo.

Mazungumzo hayo yanalenga kufanya uchaguzi wa urais mapema iwezekanavyo.

Kwenye hotuba yake, Gaïd Salah alisema kuwa msimamo huo sio mpya, pamoja na kushutumu jitihada za mazungumzo.

Alisema maombi ya hatua za kuafikiana ni ukoloni mamboleo na fikra potovu ambazo hutoka kwa kile alichokiita kundi, neno alilotumia kwa kumaanisha wafanyabiashara wakuu walio na ukaribu na familia ya Abdelaziz Bouteflika.

Ahmed Gaid Salah alisema hatua hizo za kuafikiana ni pamoja na kuachiliwa kwa watu waliowekwa kizuizini kwa kuvaa bendera iliyopigwa marufuku na kutotumia nguvu zaidi wakati wa maandamano.

Wakati jopo la wapatanishi likiendelea kukosolewa vikali, hoja kuu ya wajumbe wake saba ni kwamba hatua hizo za kuafikiana zilikuwa zimepokelewa vizuri na Makamu wa Rais, Abdelkader Bensalah.

Taarifa ya Mkuu wa Jeshi ilieleza kuwa hatua hiyo inadhoofisha jopo la wapatanishi dhidi ya wapinzani na waandamanaji.

Juzi mmoja wa wajumbe hao ambaye ni mtaalamu wa uchumi, Smail Lalmas alisema anafikiria kujiondoka kwenye jopo hilo la wapatanishi. **RFI**

## EU waipunguzia Kenya fedha

**NAIROBI,** Kenya

UMOJA wa Ulaya (EU) umepunguza nusu ya kiwango cha fedha zilizotengewa Kenya katika mapambano yake dhidi ya kundi la Alshabaab nchini Somalia.

Takwimu mpya zinaashiria kuwa serikali ya Kenya ilirejeshewa Sh. bilioni 4.3 kwa mwaka wa fedha uliokamilika ambazo ni nusu ya kile ilichotarajia. Kwa mwaka huu mpya wa fedha Kenya inasubiria Sh. bilioni tano tu ya kiasi ilichoomba.

Hata hivyo, EU umeahidi kuendelea kuunga mkono ujumbe wa Umoja wa Afrika (AU) nchini Somalia (AMISOM) kwenye harakati zake za mwaka wa fedha wa 2019/20.

Mchango wa EU unagharamia malipo ya vikosi na jeshi, wahudumu na operesheni za kila siku.

Kwa upande wa pili ofisi ya Umoja wa Mataifa ya usaidizi nchini Somalia (UNSOS) inachangia nyenzo kwenye operesheni za vikosi vya AMISOM na wanajeshi wa Somalia. **DW**

# TRA yakusanya Tril. 15.9/-

**Na Mwandishi Wetu**

MAMLAKA ya Mapato (TRA) imekusanya Sh. trilioni 15.9 kati ya Sh. trilioni 18 ilizotakiwa kukusanya kwa mwaka wa fedha 2018/19.

Mkurugenzi wa Huduma na Elimu kwa Mlipakodi wa TRA, Richard Kayombo, katika mkutano na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana, alitaja vikwazo vitatu vilivyosababisha washindwe kufikia lengo lililowekwa kwa kipindi hicho.

Alivitaja vikwazo hivyo kuwa ni kuwapo kwa pingamizi za kikodi mahakamani, udhibiti wa mianya ya ukwepaji kodi na na wateja ambao bado hawajafikiwa na hawajawa na utayari wa kulipa kodi kwa hiari.

Kayombo alisema changamoto hizo zinafanyiwa kazi kuhakikisha wanafikia malengo yanayowekwa na serikali.

Alibainisha kuwa katika robo ya nne ya mwaka huo wa fedha, yaani kipindi cha kuanzia Aprili hadi Juni 2019, TRA ilikusanya Sh. trilioni 1.1 (Aprili), Sh. trilioni 1.2 (Mei) na Sh. trilioni 1.5 Juni.

"Kwa namna ya kipekee kabisa, TRA inawashukuru walipakodi na wananchi wote kwa ujumla kwa ushirikiano," alisema.

Kayombo aliongeza kuwa kwa kipindi hicho, serikali ilianzisha Mfumo wa Stempu za Kodi za Kielektroniki (ETS) ambao utekelezaji wake umefanyika kwa awamu mbili. Alisema awamu ya kwanza iliyoanza Januari 15, mwaka huu, ilihusisha bidhaa za sigara, mvinyo, pombe kali, bia na aina zote za vileo na kwamba imeendelea vizuri na sasa wanaandaa awamu ya pili.

"Awamu ya pili itajumuisha bidhaa za vinywaji baridi, maji, juisi na CD/DVDs. Mfumo huu wa ETS kwa awamu hii ya pili utaanza rasmi Agosti Mosi mwaka huu (leo)," alibainisha.

Kwa mujibu wa Kayombo, lengo la kubandika stempu hizo za kielektroniki ni kuongeza usimamizi na ufanisi wa ukusanyaji wa ushuru wa bidhaa ikiwa ni pamoja na kupata taarifa sahihi za uzalishaji viwandani ili kukusanya mapato stahiki.

"TRA inaamini wazalishaji, waingizaji, wasambazaji, wauzaji wote wa bidhaa zinazotozwa ushuru wa bidhaa pamoja na umma kwa ujumla wataendelea kutoa ushirikiano ili kufanikisha utekelezaji wa mfumo huu kwa kila mmoja kutimiza wajibu wake kwa mujibu wa sheria, kanuni na taratibu zilizopo," alisema.




Mkurugenzi Mkazi wa Ceed Tanzania, Atiba Amalile, akizungumza katika mafunzo ya ujasiriamali yaliyoandaliwa na kampuni hiyo, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: BEATRICE SHAYO**

# JKT waingia barabarani kufanya usafi

INATOKA UK.3

jiji hilo lina mkanganyiko wa watu wa daraja la chini wanaoishi katika mazingira ya uchafu kulingana na utendaji wao wa kazi.

"Mfano wa shughuli za mmachinga wa Kariakoo ambaye anashinda juani kutwa nzima na jasho linamtoka wakati wote anaweza vipi kuwa katika hali ya utanashati wakati wote," Omary alihoji.

Makonda alitangaza operesheni hiyo mapema Jumatatu wakati akizindua kampeni ya usafi wa jiji la Dar es Salaam ikiwa ni moja ya maandalizi ya mkutano wa 39 wa SADC unaotarajiwa kufanyika hapa nchini Agosti 17 na 18, mwaka huu.

"Tabia ya kuja mjini hujafua, hujaoga usitutie aibu kama umezoea kuja mjini hujaoga wala kufua nguo baki nyumbani walau huu mwezi wa nane uishe, tunataka sio usafi tu wa mazingira, usafi pia wa wananchi wetu, watu wamejaa chawa tu hapa," Makonda alisema.

Aliwaonya wananchi wenye tabia ya kutupa taka ovyo wakiwa kwenye vyombo vya usafiri hususani daladala kuwa watashushwa na kupewa adhabu kali ikiwa ni pamoja na kufanyishwa usafi.

Pia, Makonda ameagiza mtu yeyote mwenye gari atakayetupa takataka barabarani asitozwe faini badala yake apewe eneo la kufanya usafi. Alisema baadhi ya watu hao wana jeuri ya fedha, hivyo kwao faini siyo adhabu.

Mwenyekiti wa kamati ya usafi ambaye pia ni Mkuu wa Wilaya ya Kigamboni, Sarah Msafiri, alisema shughuli ya usafi itafanywa na vijana 130 JKT na mgambo 300 katika maeneo mbalimbali ya jiji.

# Marehemu 193 watumika

INATOKA UK.2

anayechukua Sh. 52,000 za kodi ya pango kila mwezi, anajiita mnufaika wa Tasaf," Ole Sabaya alisema.

Mkuu wa Wilaya huyo pia alisema wamebaini baadhi ya wanufaika wa Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini ni wastaafu ambao wanapokea kiinua mgongo, hivyo hawapaswi kunufaika na mpango huo.

Alibainisha kuwa katika upigaji huo, wamo pia mtumishi wa serikali, madiwani wawili na wenyeviti wa vijiji tisa ambao wote wanaitwa wanufaika wa Tasaf. Ole Sabaya aliendelea kueleza kuwa wamekuta watu wengine 813 ambao kwenye orodha hawapo wilayani, lakini wanavyo vitambulisho na wanapewa pesa.

"Kamati yangu pia imewakuta watu saba ambao wao wanazo akaunti mbili tofauti, moja ikiwa katika Kijiji cha Uswaa na nyingine Kijiji cha Kware," alisema.

"Kamati pia ilibaini watu wengine watatu ambao walifariki dunia Novemba mwaka jana, wakafufuka Januari mwaka huu, wakaandika mirathi, mtu fulani aende kuchukua fedha hizo za Tasaf."

Ole Sabaya alibainisha kuwa mpaka sasa, mpango huo una jumla ya wanufaika 3,887, lakini 1,045 hawastahili kabisa kunufaika nao kwa sababu hawakidhi vigezo.

**DC ACHARUKA**

Kutokana na ufujaji huo wa fedha za umma, Ole Sabaya aliamuru kukamatwa kwa Mratibu wa Tasaf wa Wilaya ya Hai, Erick Marsham na watendaji waratibu wasaidizi wanane ili wakalisaidie Jeshi la Polisi na Takukuru kujua zilikokwenda fedha hizo.

"OCD na Takukuru, kwanza Mratibu wa Tasaf wa Wilaya (Marsham) ambaye anajua fedha hizi zilikuwa zinakwenda wapi, Erick unajua wewe ni kati ya watu ninaowaheshimu, wanaofanya kazi vizuri, lakini katika hili umenitibua.

Hadi jana saa 12 jioni, watu 24 walikuwa wamekamatwa na Jeshi la Polisi kuhusiana na ufujaji wa fedha za mpango huo. Ili kudhibiti mianya ya upigaji huo, Ole Sabaya alitangaza kuzivunja kamati zote za usimamizi wa fedha vijijini 62.

# Upandikizaji vifaa vya kusikia wapunguza gharama 60%

**Na Beatrice Shayo**

KUANZISHWA kwa huduma ya kupandikiza kifaa cha kusikia katika Hospitali ya Taifa ya Muhimbili (MNH) kumesaidia kupunguza gharama kwa asilimia 60 kwa wagonjwa waliokuwa wanapelekwa nje ya nchi.

Huduma hiyo ilianzishwa mwaka 2017 baada ya watoto waliokuwa wanapelekwa nje ya nchi kupatiwa huduma hiyo kutibiwa kwa gharama ya kuanzia Sh. milioni 60 hadi 100 nchini India.

Akizungumza na waandishi wa habari jana jijini Dar es Salaam wakati wakiendelea na upasuaji wa kupandikiza kifaa cha kusikia katika sikio, Daktari Bingwa wa Magonjwa ya Masikio, Pua na Koo katika Hospitali ya MNH, Edwin Liyombo, alisema huduma hiyo inatolewa kwa aliyefanyiwa vipimo na kubainika hana uwezo wa kusikia na kumpandikiza kifaa hicho ambacho kinagharimu Sh. milioni 35.

"Kuna kifaa cha kusaidia kusikia cha kuvaa na kuna kifaa kingine cha kusaidia kusikia kwa njia ya upandikizaji ambacho kinawekwa kwa njia ya upasuaji hicho ndio tunakifanya leo kupandikiza kifaa cha kumwezesha kusikia," alisema.

Alisema tatizo hilo likimpata mtoto mwenye umri mdogo anashindwa kuongea na ndio maana programu yao imeangalia watoto zaidi waliopo chini ya umri wa miaka sita kuliko watu wazima.

"Lengo letu ni kuwaokoa watoto wadogo ambao wanazaliwa na matatizo ya kusikia kwa kuwa hushindwa kujifunza kuongea, hivyo ukimwacha kama alivyo atakuwa kiziwi," alisema.

Dk. Liyombo alisema tangu mwaka 2012 serikali ilikuwa inapeleka watoto kwenda kutibiwa nje ya nchi kwa sababu hapakuwa na utaalamu huo nchini.

Alisema utaalamu huo ni wa hali ya juu na matibabu yake ni ya gharama kubwa tangu mwaka 2012 hadi 2016 jumla ya watoto 50 walitibiwa katika hospitali mbalimbali nchini India. Alisema kumekuwa na changamoto mbalimbali kwa kuwa mzazi anapokwenda na mwanawe hukaa si chini ya miezi mitatu kusubiri matibabu na gharama zake zilikuwa ni kubwa kati ya Sh. milioni 60 hadi 100 kwa familia moja.

"Vile vile akienda huko nje ya nchi haendi mara moja anatakiwa kurudi kama mara mbili au tatu mpaka mgonjwa awe ameimarika," alisema Dk. Liyombo.

Alisema serikali ilifanya utafiti na kuona kwa nini wasitoe huduma hiyo wakawezeshwa kuanzisha upasuaji mwaka 2017.

"Hii ni mara ya nne tunafanya na mpaka sasa hivi mgonjwa wa 24 ndio anafanyiwa upasuaji zoezi hili likimalizika wiki hii tutakuwa tumewafanyia jumla ya wagonjwa 30," alisema na kuongeza:

"Mwaka 2012 hadi 2016 walifanyiwa wagonjwa 50 sisi mwaka 2017 hadi sasa tumewafanyia wagonjwa 30, hivyo ni zaidi ya asilimia 60 ya wagonjwa hao ambao walipelekwa nje ya nchi tumejitahidi kufanikiwa katika hilo."

TANGAZO


# MATANGAZO MCHANGANYIKO


NIPASHE NI JIBU LAKO

NJOO UTANGAZE NASI BIDHAA

YAKO KWA BEI NAFUU SANA


## KUPOTELEWA NA CHETI/RESULT SLIP



**BENITHA BENJAMINI RWAITAMA** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye **index namba S.1404/0013** kilichotolewa na **LORD BADEN POWELL SEC. SCHOOL CENTRE mwaka 2016** pamoja na **Result Slip.**

Yeyote atakayeviona atoe taarifa kituo cha polisi.
Taarifa ya polisi:
**DAR/KIG/RB/174942/2019.**

115354002

## KUPOTEA KWA CHETI



**Judith Frederick Marunda** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index **namba S328/17** kilichotolewa na Baraza la Mithihani la Taifa mwaka 1986 katika shule ya Sekondari Mawenzi Moshi.

**Yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.**
**Polisi Taarifa: MOS/RB/10633/2016**

215353602

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**ROSE M. KASHINZO,**
Anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya Suzuki Carry yenye jina Salim Said Salim Yenye namba za usajili **T 301 BLV.** Yenye chassis No. **DC51B511209 No.** injini na **F6AEAA1209.**

Yeyote atakayeviona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
Taarifa ya polisi:
**MOS/TR/RB/404/2019.**

115355302

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KUITWA SHAURINI MDAIWA**
**(MCA/84)**

**Mahakama ya Mwanzo ya Kindi**
**Wilaya ya Moshi**
**Mirathi nambari 14 ya 2018**

**Wasimamizi 1. Sulemani Sadick (2) Jimmy Sadiki**
**Mdai**
**Wasimamizi (1) Sulemani Sadick (2) Jimmy Sadick kwa Jimmy Sadick wa Dar Es Salaam**

**Kwa kuwa mdai /Wadai ameleta /wameleta madai yake /yao kwamba /Eleza hapa habari ya madai )**

**Malalamikoo dhidi ya mgao wa mali.**

Kwa hiyo " Unahitajiwa /Mnahitajiwa kuhudhuria binafsi katika Mahakama hii siku Jumatatu Tarehe 5/08/ 2019 saa 3:00 Asubuhi/alasiri kwa kujibu Madai hayo Na. kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kukatwa shauri hilo ni lazima kuleta mashahidi wako/wenu na hati zote zinazohusu shauri hilo kwa ajili ya kujitetea katika shauri hilo

Angalia kama hukuhudhuria /hamkuhudhuria siku iliyotajwa hapo juu. Mahakama ikithibitisha kama umepokea /Mmepokea kutwa shauirini hii itaweza kutoa hukumu kuwa umeshindwa /mmeshindwa Hati hii yatolewa kwa amri yangu na chapa ya Mahakama hii leo tarehe 29/07/2019.

115355502

**SHERIA YA UANDIKISHAJI WA ARDHI (SURA 334)**

**KUPOTEA KWA HATI YA KUMILIKI ARDHI**

**HATI YA NAMBA: 959- MBYLR**

**MMILIKAJI: HADIJA JEKI MGOGO P.O BOX, MBEYA,**

**ARDHI: L.O.NO. 102155, kiwanja Na.25, Kitalu 25, Nonde Street, Mbeya mjini,**

**ENEO: 2684, Futi za Mraba**

**TAARIFA IMETOLEWA** Kwamba hati ya kumiliki ardhi iliyotajwa hapo juu imepotea na ninakusudia kutoa hati mpya badala yake iwapo hakuna kipingamizi kwa muda wa mwezi mmoja toka tarehr ya taarifa itakpotangazwa katika Gazeti la Serikali. Hati ya asili ikionekana irudishwa kwa Msajili wa hati Msaidizi Mkuu, S.L.P2984, Mbeya.

115355102

**UYOLE HOSPITAL LIMITED**
**NAMBA YA KAMPUNI : 28839**

## TANGAZO LA KUFUNGA KAMPUNI

Bodi ya wakurugenzi na wanahisa wa **UYOLE HOSPITAL LTD** imeamua kufunga shughuli zake za biashara kuanzia tarehe **20/06/2019.**

Kwa tangazo hili watu wote ambao wanaidai Uyole Hospital Ltd wapeleke madai yao ndani ya siku 90 kuanzia tarehe ya tangazo hili katika ofisi za **Uyole Hospital Ltd.**

**Mawasiliano :**

**Dk.Nkunja K.Sijabaje (0754056102)**
**au Ndg.Erasto M.Sijabaje (0754094773).**

115354402

**IN THE HIGH COURT OF TANZANIA**
**AT SONGEA**
**MSC LAND APPLICATION NO. 11 OF 2019**
**(From the decision of the District land of Housing Tribunal)**
**Of Songea District in land Appeal No. 243 of 2016 and Original Ward Tribunal of....Ward in Application No. ....20...**
**DR. WADE ASYUKILE KABUKA..........................APPLICANT**

**ASUMAN RASHID AND 3 OTHERS.........**RESPONDENTS

TO:
ASUMAN RASHID

## NOTICE OF DATE OF MENTION

**TAKE NOTICE** that above case has been fix for mention on **06th** Day of **August, 2019 at 9:00** noon before **Hon. I. Arujani** JUDGE

YOUR ARE required to appeal in this court on the fixed date without fail.

GIVEN under my hand and the seal of the court this **11th day July, 2019.**

115354202


Kwa Habari Motomoto

usikose Gazeti lako la Nipashe

kila siku Tupigie 0767 223 311

Kwa Habari Motomoto

usikose Gazeti lako la

Nipashe kila siku

NJOO UTANGAZE

BIDHAA YAKO

KWA BEI NAFUU SANA



OFISI ZA MATANGAZO
MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,
PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.
E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com



TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# Joao: Nataka kuwa kama Ronaldo

**MADRID,** Hispania

MSHAMBULIAJI wa Atletico Madrid, Joao Felix, ambaye amekuwa akitajwa na wengi kuwa ni "Cristiano Ronaldo mpya" ameiambia ESPN kwamba anataka kuwa na mafanikio makubwa kama mchezaji mwenzake huyo wa timu ya taifa ya Ureno.

Felix alikuwa kwenye kikosi pamoja na Ronaldo wakati Ureno ikitwaa taji la Ligi ya mataifa ya Uefa, kabla ya kununuliwa kwa euro milioni 126 kwenda Atletico.

"Cristiano Ronaldo ameshinda mara tano Ballon d'Or na hii ni ndoto ya kila mchezaji," alisema Joao katika mahojiano maalumu na ESPN. "Kwa uhakika kabisa nataka kuwa kama Cristiano."

Kulikuwa na timu nyingi zilizokuwa zinamtaka Felix kipindi hiki cha majira ya joto, lakini aliamua kujiunga na Atletico kutokana na rekodi yao ya kuzalisha washambuliaji wakubwa duniani.

Sergio Aguero, Diego Forlan, Fernando Torres na Radamel Falcao wote wamefurahia muda mzuri wa kucheza katika klabu hiyo yenye maskani yake mji mkuu wa Hispania na Felix amesema anataka kuwa kama wao.

"Niliwaona washambuliaji ambao Atletico walikuwa nao na walikuwa wachezaji wakubwa, washambuliaji bora,"aliongeza. "Nataka kuwa zaidi ya wao na ndio maana nilichagua kuja hapa."

Felix tayari ameonyesha kiwango cha kuvutia kwa kufunga bao moja na kutoa pasi ya mabao mawili wakati Atletico wakiibuka na ushindi wa mabao 7-3 dhidi ya wapinzani wao Real Madrid kwenye mechi za maandalizi ya msimu mpya wa Ligi Kuu.





# RONALDO AWAPIGA KIJEMBE BARCA

**MADRID,** Hispania

MCHEZAJI wa zamani wa Real Madrid, Cristiano Ronaldo, amewapiga kijembe wapinzani wake wa zamani, Barcelona kwa kuwaambia fedha haiwezi kununua mafanikio kwenye Ligi ya mabingwa Ulaya.

Ronaldo, ambaye alikuwa mjini Madrid kutunukiwa tuzo ya Marca Leyenda, ana matumaini ya kuwa mchezaji wa pili kushinda taji la ligi ya mabingwa Ulaya na Klabu tatu tofauti.

Kwa sasa Clarence Seedorf ndiye anayeshikilia rekodi ya kushinda taji la ligi ya mabingwa Ulaya na klabu tatu tofauti. Alishinda mara moja akiwa na Ajax mwaka 1995, akashinda tena na Real Madrid mwaka 1998 na alishinda mara mbili na AC Milan mwaka 2003 na 2007.

"Mara zote ni mwaka wa Juventus, wa Madrid, wa Barca," alisema akiliambia gazeti la Marca wakati alipoulizwa kama Bianconeri walikuwa na wanapewa nafasi ya kushinda taji hilo.

"Kwenye mashindano kama ya Ligi ya mabingwa Ulaya, timu moja tu inaweza kushinda.

"Nitatumia mfano wa Barcelona: Angalia kiasi gani cha fedha walichowekeza ndani ya miaka mitano iliyopita na hawajashinda kombe la Ligi ya mabingwa Ulaya. Hivyo ndivyo ilivyo.

"Juve kwa sasa imefanya usajili mkubwa wa kuimarisha kikosi chake na ni timu ambayo inataka kupambana kushinda taji, kama ambavyo mara zote wamekuwa wakifanya hivyo.

"Lakini kwa yote hayo inategemea na mambo mengi: droo ya kwenye kundi, hali ya majeruhi na bahati pia. Lakini mara zote kama ninavyosema kushinda ligi ya mabingwa Ulaya sio kazi rahisi.

# *Pochettino: Sijui kuhusu usajili Tottenham Hotspur*

**LONDON,** England

KOCHA wa Tottenham Hotspur, Mauricio Pochettino, amevijia juu vyombo vya habari na kusisitiza kwamba, yeye kazi yake ni ukocha na hivyo hana mamlaka ya kujibu juu ya usajili wa wachezaji, kwani hajui chochote kuhusu nani anasajiliwa na nani anaondoka.

Alikuwa akiishuhudia timu yake ikiichapa Real Madrid bao 1-0 shukrani kwa Harry Kane aliyefunga, Pochettino aliulizwa kuhusu majaliwa ya beki wake wa kushoto, Danny Rose na alijibu kwamba suala hilo linawezakutolewa ufafanuzi na mwenyekiti, Daniel Levy.

"Sijui chochote kuhusu hali ya wachezaji wangu," alinukuliwa na gazeti la The Guardian.

"Kuuza, kununua na kusainisha wachezaji mikataba sio kazi yangu, nafikiri halipo kwenye mikono yangu, lipo chini ya klabu na mwenyekiti Daniel Levy.

"Klabu labda inibadilishie cheo, lakini kwa sasa sina mamlaka hayo. Jukumu langu ni kutoa mipango ya kikosi changu kulingana na wachezaji nilionao, lakini huko kwingine sio kazi yangu. Leo mimi ni kocha tu."

Spurs kwa kipindi hiki cha majira ya joto imekamilisha usajili ulioweka rekodi klabuni hapo kwa kumsajili kiungo wa Ufaransa, Tanguy Ndombele kutoka Lyon.



# ICARDI AKARIBIA KUTUA NAPOLI




**MILAN,** Italia

MAURO Icardi hatimaye anaweza kuondoka Inter Milan na kujiunga na Napoli baada ya kuripotiwa kwamba klabu hizo mbili zinakaribia kufikia makubaliano ya usajili wa mshambuliaji huyo matata.

Napoli inataka kutoa ofa ya pauni milioni 73 kwa ajili ya mshambuliaji huyo wa kimataifa wa Argentina na rais Aurelio De Laurentiis amekutana na wawakilishi wa Milan kukamilisha mazungumzo, kwa mujibu wa Corriere dello Sport.

Icardi alipokonywa unahodha pale kwenye dimba la San Siro msimu uliopita baada ya mke wake, Wanda Nara ambaye pia ni wakala wake kuushutumu uongozi wa klabu hiyo namna unavyomtendea mume wake.

Na baadae alikataa kucheza kwenye mchezo wa kombe la Europa dhidi ya Rapid Vienna kabla ya kurudi dimbani Aprili, ikiwa ni miezi miwili baadae.

Usajili wa Icardi umekuwa ukisuasua kwa muda kipindi hiki cha majira ya joto, huku Juventus ilikuwa ikiongoza kwenye mbio za kumuwania, baada ya kuachwa na Inter kwenye ziara ya maandalizi ya msimu mpya wa ligi.

Wiki iliyopita, gazeti la Daily Mail liliripoti kwamba, Icardi alikuwa anataka kujiunga na Juventus kwa sababu mke wake ni mjamzito na hataki kuondoka nchini Italia. Nara ni mjamzito kwa mara ya sita na ameonyesha nia yake ya kutaka watoto wake wote wazalie nchini Italia.

# *Arsenal njia nyeupe kumtwaa Tierney*

**LONDON,** England

ARSENAL wanakabiria kufikia makubaliano ya kumsajili beki wa kushoto wa Celtic, Kieran Tierney baada ya kuiboresha ofa yao ya pauni milioni 25.

Mpango huo ulikwama wiki iliyopita baada ya Arsenal kukataa kuongeza ofa yao ya awali na ilikuwa pungufu ya pauni milioni 5 iliyokuwa inatakiwa na Celtic.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 22 ameiambia klabu yake ya Celtic kwamba anataka kwenda kucheza kwenye Ligi Kuu ya England na mabingwa hao wa Scotland wapo tayari kumuachia kwenda Arsenal.

Unai Emery, ambaye alimshuhudia mchezaji waliyemsajili kwa rekodi ya klabu hiyo ya pauni milioni 72, Nicolas Pepe akiwa amewasili kufanyiwa vipimo vya afya yake juzi Jumanne, anahitaji kukiboresha kikosi chake baada ya nahodha wake, Laurent Koscielny kutokuwa tayari kuichezea klabu hiyo tena na analazimisha uhamisho wa kwenda kujiunga na Rennes.

Sasa kocha huyo raia wa Hispania anataka kutafuta beki wa kushoto kwa ajili ya kuimarisha safu yake ya ulinzi.

Arsenal inakabiliwa na majeruhi kwenye safu yake ya ulinzi, huku beki Hector Bellerin anatarajiwa kuukosa mwanzo wa msimu huu.




# Kauli ya kocha yamkera bosi

**MUNICH,** Ujerumani

KOCHA wa Bayern Munich, Niko Kovac, ameonekana kumkwaza Ofisa Mtendaji wa klabu hiyo, Karl Heinz-Rummenigge kwa kauli yake ya kusema anajiamini Leroy Sane atajiunga nao.

Winga huyo wa Manchester City kwa muda mrefu amekuwa akiwaniwa na Bavaria hao na Kovac alisema wiki hii kuwa ana imani kubwa watamsajili mchezaji huyo kipindi hiki cha majira ya joto.

Jumapili alisema: "Utawala wetu umejiimarisha vizuri. Sio rahisi kwa siku hizi, lakini ninajiamini tutampata na tutamsajili."

Lakini Heinz-Rummenigge ameiambia televisheni ya ZDF: "Sikupenda kile alichokisema, ni maneno ambayo hayakutakiwa kutamkwa na kocha."

Halafu akaelezea kwanini kuzungumzia usajili wa pauni milioni 90 haikuwa sahihi kwa Kovac.

"Tuna mahusiano mazuri na Manchester City na kocha wetu wa zamani, Pep Guardiola," aliongeza.

"Sane bado ana mkataba pale. Hata kama ameonyesha nia ya kutaka kuondoka sisi hatukupaswa kulizungumzia hili."

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 23 anawaniwa kwa udi na uvumba na Bayern kipindi hiki cha majira ya joto, baada ya kuondoka kwa Arjen Robben na Franck Ribery mwishoni mwa msimu uliopita.



# DONDO SOKA
## MAGAZE LAYA




# DYBALA, LUKAKU SASA KUPISHANA JUVE, UTD

●●● Bila shaka, tunafanyia kazi kuhusu mmoja ama wawili, kuna siku nyingine 10 kabla...

**MANCHESTER,** England

MANCHESTER United na Juventus zimekubaliana mpango wa kubadilishana wachezaji ambao unawajumuisha Paulo Dybala na Romelu Lukaku, kwa mujibu wa Sky in Italy.

**Aidha, mpango huo kwa sasa umebaki kwa upande wa Dybala kukubaliana malipo binafsi na Man United na inafahamika kwamba wakala wake yupo London tayari kwa mazungumzo na miamba hiyo ya Old Trafford ili kufanikisha dili hilo.**

Dybala anathaminishwa na euro milioni 100 (pauni milioni 91.8) na yupo tayari kubaki Juve, lakini anataka kukutana kwanza na Maurizio Sarri wakati atakaporudi kutoka likizo leo Alhamisi kabla ya kufanya uamuzi wa mwisho, kwa mujibu wa Sky in Italy.

Kocha wa United, Ole Gunnar Solskjaer, akizungumza Jumanne baada ya kushinda mechi ya maandalizi ya msimu mpya dhidi ya Kristiansund, hakuwa tayari kufunguka dhidi ya mpango huo wa Dybala, lakini akathibitisha kwamba ujio wa nyota mpya upo njiani.

"Sipo hapa kwa ajili ya kuzungumza kuhusu tetesi yoyote ama fununu kuhusu wachezaji wa timu nyingine," alisema Solskjaer.

"Lakini bila shaka, tunafanyia kazi kuhusu mmoja ama wawili, kama nilivyosema hapo kabla.

"Kuna siku nyingine 10 kabla hatujaanza ligi na ninatumai tunaweza kutangaza sura mpya ama mbili."

Juventus lazima imshawishi Dybala kukubali kuhamia Manchester, kama United itahitaji kufanya mbadala wa Lukaku. Kama Dybala hatakuwa tayari kukubaliana malipo binafsi ya kutua Old Trafford, mshambuliaji wa Lyon, Moussa Dembele pia yupo katika orodha ya kuziba pengo la Lukaku.

Hata hivyo, kama straika huyo wa kimataifa wa Argentine atakataa kuondoka Turin, Juve itapaswa kwenda na fedha taslimu mkononi lakini bado itahitajika kuuza mchezaji mmoja ama zaidi kati ya washambuliaji wake wa sasa.

Pavel Nedved, Makamu wa Rais wa Juve, Jumatatu alihoji kuhusu Dybala na Lukaku kupitia Sky in Italy.

Alisema: "Tunayo ofa kadhaa kwa Paulo Dybala, lakini tutasubiri kuamua kuhusu mustakabali wake wa baadaye. Lukaku? Mara zote tunajaribu kupata wachezaji, lakini sitaki kuzungumza kuhusu Lukaku ama wengine."

Juventus inafahamika kuhusu kuongeza kasi mbele ya Inter Milan katika mbio za kuinasa saini ya Lukaku, Sky Sports News inalitambua hilo. Mkurugenzi wa Inter, Giuseppe Marotta anasisitiza kuwa klabu hiyo ya Serie A "bado inafanyia kazi" dili hilo la kuipata saini ya Lukaku.

Pia alisema Inter imefanya "haki na ofa muhimu kulingana na thamani ya mchezaji", lakini inafahamika kuwa ofa ya pauni milioni 54 haraka ilikataliwa na United mapema mwezi uliopita.

## ZISIKUPITE

### PSG, BARCA KUMJADILI NEYMAR

MABINGWA wa Ufaransa, Paris St-Germain watakutana na maofisa wa Barcelona kujadili mpango utakaomuwezesha nyota wa kimataifa wa Brazil, Neymar, kurudi kwa mara nyingine Camp Nou. ***(Mundo Deportivo, via Express)***

### UMTITI AIVUTIA UNITED

Manchester United inavutiwa kuipata saini ya beki wa kati wa Barca na Ufaransa, Samuel Umtiti, 25. ***(Le10 Sport - in French)***

### TIERNEY AKARIBIA ARSENAL

Arsenal inakaribia kukamilisha dili la kuinasa saini ya beki wa kushoto wa Celtic na Scotland, Kieran Tierney, 22. ***(Mail)***

### ICARDI ANUKIA NAPOLI

MSHAMBULIAJI wa Inter Milan na Argentina, Mauro Icardi, 26, anaweza akatua Napoli kwa dau la euro milioni 80 (pauni milioni 73). ***(Corriere dello Sport - in Italian)***

### SABABU ARSENAL KUTOSWA

MSHAMBULIAJI wa Juventus, Moise Kean, 19, amekataa kujiunga na Arsenal na kutoa nafasi ya kutua Everton kwa sababu 'Gunners' hawakuweza kumhakikishia straika huyo wa Italia nafasi katika kikosi cha kwanza. ***(Mail)***

### SANE AIVURUGA BAYERN

MWENYEKITI wa Bayern Munich, Karl-Heinz Rummenigge, amesema hajui kwa nini kocha Niko Kovac amesema klabu hiyo inaamini itamsajili winga wa Manchester City, Mjerumani Leroy Sane, 23. ***(Bild - in German)***

### ZIDANE AMTAJA RODRIGUEZ

KOCHA wa Real Madrid, Zinedine Zidane, amesema hajui kama kiungo mshambuliaji, Mcolombia James Rodriguez, 28, atakuwapo katika klabu hiyo ya Hispania msimu ujao. ***(Marca)***

### MUSTAFI HATOTUA ITALIA- BABA

BABA na wakala wa beki wa kati wa Arsenal, Shkodran Mustafi, amekanusha kuwapo kwa mpango wa mchezaji huyo wa kimataifa wa Ujerumani kutua klabu ya Italia. ***(Romanews - in Italian)***

### MOURINHO AJIWEKA SOKONI

KOCHA wa zamani wa Chelsea na Manchester United, Jose Mourinho atarudi kibaruani endapo tu atapata ofa sahihi. ***(Sky Sports)***

### KOKE AMTABIRIA USTAA FELIX

KIUNGO wa Atletico Madrid, Koke, amesema mshambuliaji wa Ureno, Joao Felix, 19, atakuwa "mmoja wa wachezaji bora duniani". ***(ESPN)***

### WOODMAN ATUPIWA JICHO

KIPA wa Newcastle na England U-21, Freddie Woodman, 22, anawindwa na Celtic na Arsenal, pamoja na klabu mbili za Championship ambazo hazikutajwa. ***(Chronicle)***

HABARI MICHEZO

## Tanzania mwenyeji tamasha la JAMAFEST

**Na Sabato Kasika**

SERIKALI imesema kuwa tamasha la muziki wa 'Cigogo' lililofikia tamati jana kwenye viwanja vya Chamwino Ikulu jijini Dodoma ni mwendelezo wa heshima ya nchi na maendeleo ya sanaa kwa Ukanda wa Afrika Mashariki na kati.

Kaimu Mkurugenzi wa Idara ya Sanaa, Joyce Fisoo, alisema katika tamasha hilo la 11 kuwa heshima nyingine ambayo Tanzania imepata ni kuwa mwenyeji wa tamasha la Afrika Mashariki liitwalo JAMAFEST litakalofanyika kuanzia Septemba 21 hadi 28 mwaka huu jijini Dar es Salaam.

Fisoo alisema kuwa tamasha la JAMAFEST ni kichocheo cha ukuzaji sanaa na uchumi wa nchi wanachama, na kuwataka wadau mbalimbali wa sanaa nchini kuitumia vema fursa ya tamasha hilo linalokuja.

Aidha, Fisoo ambaye alikuwa Mtendaji Mkuu wa Bodi ya Filamu Tanzania, alisema kutokana na utendaji uliotukuka wa waandaaji wa tamasha la Cigogo, Kituo cha Sanaa Chamwino (CAC), anajipanga kuandaa cheti maalum kwa ajili ya kutambua na kuthamini mchango wa taasisi hiyo.

Aliongeza kuwa kutokana na ukubwa wa tamasha hilo, anajiandaa kuishawishi serikali kuongezea nguvu kwa sababu ya maudhui yake.

Naye mwenyekiti wa tamasha hilo, Dk. Kedmon Mapana, aliwataka wadau kujiandaa kulitumia tamasha la JAMAFEST kama sehemu ya fursa kwa ajili ya maendeleo.

## Mshindi M-bet kujisomesha TIA

**Na Mwandishi Wetu**

SHABIKI wa mabingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Simba na mwanafunzi wa Taasisi ya Uhasibu (TIA) tawi la Mbeya, Msafiri Shafii, ameibuka mshindi wa kitita cha Sh. milioni 157.2 cha mchezo wa kubahatisha wa Perfect 12 unaochezeshwa na Kampuni ya M-BET, imeelezwa.

Msafiri, mkazi wa Mbeya anayeishabikia Simba na Manchester United ya England, ameibuka mshindi baada ya kubashiri kwa usahihi mechi 12 za ligi mbalimbali duniani na kuwa mshindi wa saba wa mwaka huu.

Meneja Masoko wa M-BET Tanzania, Allen Mushi, alisema kuwa ushindi wa Msafiri unaifanya kampuni yao kutumia zaidi ya Sh. bilioni moja kwa ajili ya kutoa zawadi kwa washindi wake tangu walipoanza shindano hilo mapema mwaka huu.

Mushi alisema kampuni yao inaendelea kuwa nyumba ya mabingwa na kuwaomba wadau mbalimbali wa mchezo huo wa kubahatisha wenye umri kuanzia miaka 18 wasisite kujaribu bahati yao.

Aidha, aliwaomba wadau kuendelea kushiriki hasa baada ya msimu wa ligi za nchi za Ulaya na mataifa mengine kutarajiwa kuanza mwezi huu.

# NDAYIRAGIJE MATUMAINI KIBAO STARS KUFUZU CHAN

**Na Shufaa Lyimo**

KAIMU Kocha Mkuu wa timu ya Taifa (Taifa Stars), Etienne Ndayiragije, amesema hana wasiwasi wowote na kikosi chake kinachojiandaa na mchezo wa marudiano wa kuwania kufuzu fainali za Kombe la Mataifa Afrika kwa Wachezaji wa Ndani (CHAN), dhidi ya Kenya (Harambee Stars), utakaochezwa Jumapili jijini Nairobi nchini Kenya.

Taifa Stars inahitaji ushindi ama sare ya mabao yoyote ili iweze kusonga mbele katika mashindano hayo yanayoandaliwa na Shirikisho la Soka Afrika (Caf) kufuatia sare tasa katika mchezo wa awali uliopigwa wiki iliyopita Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam.

Akizungumza na gazeti hili jana, Ndayiragije, alisema ameyafanyia kazi makosa yaliyojitokea katika mchezo wa kwanza na sasa wako tayari kupambana kuhakikisha wanapata ushindi kwenye mchezo huo wa marudiano.



**Ndayiragije alisema Watanzania wanatakiwa kutokata tamaa na badala yake kuendelea kuipa ushirikiano timu hiyo ili iweze kufanya vema katika mashindano hayo.**

"Sina wasiwasi na wachezaji wangu, naamini Mungu akipenda tutarudi na matokeo mazuri, tunaendelea kujiimarisha kwa sababu tunataka kurudi nyumbani na matokeo mazuri, naomba Watanzania wazidi kutuombea," alisema Ndayiragije.

Mrundi huyo aliongeza kuwa anaridhishwa na nidhamu inayoonyeshwa na wachezaji wake wakiwa ndani na nje ya uwanja kwa muda mfupi ambao amekaa nao.

"Wachezaji wana nidhamu nzuri, wapo makini ninapokuwa nawafundisha, jambo ambalo linanipa faraja, kila mmoja anaonyesha ana kiu ya kufanya vema," alisema kocha huyo.

Pia alivishukuru vyombo vya habari kwa kutumia nguvu ya juu katika taaluma yao kuhamasisha Watanzania kuipenda timu hiyo ambayo mara ya mwisho kushiriki fainali za CHAN ilikuwa ni mwaka 2008.

"Nawashukuru waandishi wa habari kwa kutumia nguvu nyingi kuhamasisha Watanzania kuisapoti timu yetu ili tuvuke hatua hii," Ndayiragije alisema.



Mshambuliaji mpya 'mwili jumba' aliyetua kukamilisha usajili Yanga kutoka DR Congo, David Molinga (pichani kushoto) ambaye aliwasili jijini Dar es Salaam jana. **NA MPIGAPICHA WETU**

## *Tanzanite yafuata mafanikio bondeni*

**Na Mwandishi Wetu**

TUKO imara, hayo ni maneno ya Kocha Mkuu wa timu ya Taifa ya Wanawake ya umri chini ya miaka 20 (Tanzanite), Bakari Shime, kuelekea mashindano ya Cosafa yanayotarajiwa kuanzia leo hadi Agosti 11, mwaka huu nchini Afrika Kusini.

Kikosi cha Tanzanite chenye wachezaji 20 na viongozi sita akiwamo Mjumbe wa Kamati ya Utendaji ya Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), Sarah Chao, kiliondoka nchini jana asubuhi kuelekea mjini Port Elizabeth kushiriki michuano hiyo.

Akizungumza na gazeti hili jana kabla ya kuanza safari, Shime alisema wachezaji wake wote wako salama na amewataka Watanzania wawe na amani kwa sababu kila mchezaji wa timu hiyo anafahamu kiu ya mafanikio waliyonayo.

Shime alisema kikosi chake kimepata maandalizi yanayostahili na anaamini kila mchezaji aliyepata nafasi ya kuwamo kwenye timu hiyo atatimiza vema majukumu yake ili wapate ushindi.

Naye Esther Mabanza, mchezaji wa timu hiyo, alisema wamefanya maandalizi mazuri na kila mchezaji alikuwa anajituma kwenye mazoezi ya timu hiyo.

"Tunaimani tutaenda kufanya hivyo, tutaenda kujituma kwenye mashindano hayo, tuko vizuri kimwili, kiakili na hata kimatendo pia, tunawaambia Watanzania huko tunafata ushindi," alisema Mabanza.

# Michezo



Alhamisi Agosti 1, 2019

Nipashe

**Icardi akaribia kutua Napoli**

UKURASA 29

**WAMEKUBALI...**



Mshambuliaji wa Tottenham Hotspur, Harry Kane, akizamisha mpira kimyani dhidi ya kipa wa Real Madrid, Keylor Navas, wakati wakiibuka na ushindi wa bao 1-0 juzi kwenye mechi ya nusu fainali ya Kombe la Audi iliyopigwa katika Uwanja wa Allianz Arena, Ujerumani, kwa ushindi huo Spurs sasa itakutana na Bayern Munich fainali kufuatia Wajerumani hao kuichapa Fenerbahce mabao 6-1. **PICHA: MTANDAO**

## Simba Day kipimo kuiua UD Songo

**Na Mwandishi Wetu**

WAKATI Simba imeingia mkataba wa miaka miwili na Kampuni ya Romario ya jijini Dar es Salaam kwa ajili ya kutoa huduma ya vifaa mbalimbali vya michezo, Kocha Mkuu wa timu hiyo, Mbelgiji Patrick Aussems, amesema anatarajia siku ya Simba Day itakuwa "bomba" na muhimu kwao kufanya vizuri.

Aussems alisema siku hiyo ndiyo itakuwa ya mwisho ya kukipima kikosi chake kuelekea mchezo wa kwanza wa Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya UD Songo ya Msumbiji, ambayo itachezwa ugenini.

Mbrazil huyo alisema anatarajia kuona idadi kubwa ya mashabiki wanajitokeza uwanjani ili kushuhudia wachezaji wao wapya huku pia nyota wake waliokuwa kwenye kikosi cha Timu ya Taifa (Taifa Stars) wakiungana na wenzao mapema Jumatatu.

Wakati huo huo, Simba imeingia mkataba wa miaka miwili na Kampuni ya Romario UhlSport kwa ajili ya kusambaza vifaa mbalimbali vya michezo na jezi zitakazotumiwa na timu hiyo kwa msimu mpya wa Ligi Kuu Tanzania Bara na mashindano ya kimataifa.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa Simba, Crescentius Magori, amesema mkataba huo ambao wamesaini una thamani ya Sh. milioni 600 na klabu hiyo kila mwaka itakuwa inapokea vifaa vya michezo vyenye thamani ya Sh. milioni 200 na fedha taslimu Sh. milioni 100 kwa ajili ya kusaidia shughuli za uendeshaji wa klabu hiyo.

"Msimu huu Simba itakuwa na jezi za aina tatu, nyekundu kwa mechi za nyumbani, nyeupe tutakapokuwa ugenini na kijivu ambayo ni jezi huru kwa mujibu wa kanuni mpya za Caf (Shirikisho la Soka Afrika)," alisema Magori.

Mkurugenzi wa Romario UhlSport, Minhal Dewji, alisema wanaahidi kufanya kazi na Simba kwa ushirikiano mzuri na anawataka mashabiki na wanachama wa klabu hiyo kuhakikisha wananunua jezi halisi.

# *Straika mwili jumba atua Yanga*

## Ni Molinga kutoka FC Lupopo, safari ya Kindoki kuondoka yaiva, mabeki Ligi Kuu sasa...

**Na Somoe Ng'itu**

JESHI la Yanga kwa ajili ya kushiriki Ligi Kuu Tanzania Bara na mashindano ya kimataifa msimu ujao, limekamilika baada ya jana kumpokea mshambuliaji mpya, David Molinga mwenye 'mwili jumba' kutoka FC Lupopo ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), imefahamika.

**Usajili wa Molinga utakamilisha idadi ya wachezaji 10 wa kigeni wa Yanga ambao itawatumia kwenye mashindano mbalimbali watakayoshiriki.**

Yanga italazimika kumwacha mchezaji mmoja endapo itakamilisha usajili wa mshambuliaji huyo, huku golikipa Mkongomani Klaus Kindoki akionekana amekalia kuti kavu ili kumpisha nyota huyo.

Hata hivyo, mbali na kulipa faini ya Dola za Marekani 500 kutokana na kuchelewa kumsajili Molinga, kanuni za Shirikisho la Soka Afrika (Caf), zitawataka Yanga kusubiri hadi mechi za raundi ya pili ili kumtumia mshambuliaji huyo.

"Ni kweli tumempokea mchezaji mpya, kama ambavyo kocha wetu (Mwinyi Zahera), alivyosema kuwa usajili wake ulikuwa unahitaji straika mmoja ili afunge dirisha," alisema kiongozi mmoja wa klabu hiyo.

Wachezaji wengine wa kigeni ambao wamesajiliwa na Yanga mbali na Kindoki ni pamoja na Papy Tshishimbi kutoka DRC, Mkenya Farouk Shikalo, Sadney Urikhob (Namibia), Lamine Moro (Ghana), Juma Balinya (Uganda), Issa Bigirimana, Patrick Sibomana (Rwanda), Mustapha Selemani (Burundi) na Mzambia Maybin Kalengo.

Wakati huo huo, kikosi cha Yanga kinatarajia kurejea jijini kesho kikitokea mkoani Morogoro, ambapo waliweka kambi ili kujiandaa na msimu mpya.

Mratibu wa timu hiyo, Hafidh Saleh, aliiambia gazeti hili jana kuwa walitarajia kukamilisha programu yao ya mazoezi jana jioni na leo watatumia muda mwingi kupeana mwongozo na misingi ya klabu hiyo.

"Tutarudi Dar es Salaam Ijumaa, kwa upande wa mazoezi ya uwanjani kila kitu kimekamilika, kilichobakia ni maelekezo ya kawaida ambayo mara nyingi hutolewa kabla ya kuanza msimu," alisema mratibu huyo.

Katika Siku ya Wananchi, Yanga itaikaribisha Kariobangi Sharks kutoka Kenya katika mchezo wa kirafiki wa kimataifa utakaochezwa Jumapili kwenye Uwanja wa Taifa jijini.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002